**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Nane - Tarehe 18 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA NA MUUNGANO:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo tena ni siku ya Alhamisi, tunaingia kwenye Maswali kwa Waziri Mkuu. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani swali kwa Waziri Mkuu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI YA UPUNZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la kwanza kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu, Nina imani wewe binafsi na Bunge lako Tukufu linatambua vizuri kwamba uchaguzi ni jambo muhimu katika Taifa, na kwamba panapokuwepo hofu kwa wadau wanaohusika na masuala ya uchaguzi katika Taifa basi inawezekana sana na ikawa rahisi kutokea machafuko ambayo yangeweza kuepukika.

Tunavyozungumza hivi sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeanza mchakato wa kujiandaa kuweka utaratibu wa *biometric* katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Utaratibu huu wa *biometric* wa kutambua wapiga kura kwa maana ya alama za mwili kama *finger tips* na macho pamoja na kwamba haupo katika sheria inayosimamia *Permanent Voters Register (PVR)* ni utaratibu ambao umechafua uchaguzi wa Nchini Ghana na Nchini Kenya katika siku za karibuni na ni utaratibu ambao unafanyika kwa hali ambayo wadau wengi wa siasa hawajawashirikishwa wala Bunge lako Tukufu halijawahi kutoa Baraka hizo.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu sijui utaliambia nini Taifa kuhusu kauli hiyo, kama kweli Tume ya Taifa ya Uchaguzi kama ambavyo amekaririwa Mwenyekiti wa Tume akidai kwamba ameshaanza mchakato, kweli utaratibu huo unafanyika na unafanyika kwa sheria ipi, bila wadau kufahamishwa? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi kidogo leo sauti yangu siyo nzuri sana nimepata kidogo *flu*.

Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kutoa ufafanuzi kidogo kuhusu suala ambalo Mheshimiwa Mbowe ameliuliza. Ni kweli uchaguzi ni jambo kubwa na ni jambo la msingi sana na ndiyo maana nchi zote zinajitahidi kuhakikisha kwamba chaguzi zinaendeshwa kwa utaratibu ambao utawapa wananchi imani kwamba matokeo yake ni yale ambayo kweli Watanzania watakuwa walidhamiria.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba iko mifumo mbalimbali ambayo nchi mbalimbali zinatumia, hapa nyumbani tumekuwa zaidi tunategemea kuhesabu kwa mikono, jambo ambalo nalo limekuwa likizua mjadala mkubwa sana. Kwa hiyo, baadhi ya nchi zimetumia mifumo ya sasa ambayo ni ya teknolojia ya kisasa kujaribu kuona kama inaweza ikasaidia kutatua hilo tatizo. Lakini ni kweli vile vile kwamba si kila mahali wamefaulu sana, kwa sababu linaweza likatokea jambo lolote na likawaleta mushkeli katika utaratibu mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi imani yangu ni kwamba nia ya Tume ni nzuri ya kujaribu kutumia mfumo huo. Lakini napenda niamini vile vile watakuwa vile vile na mfumo au utaratibu ambao ni mbadala endapo jambo fulani litatokea maana hata Kenya juzi tuliona walijaribu lakini ilibidi warudi kwenye utaratibu fulani, lakini nia ni nzuri. Kwa kweli kama mfumo huo utaweza kutupa matunda mazuri ni utaratibu ambao unaweza ukatuondolea malalamiko kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi sina *details* za namna walivyojiandaa kwa mfumo mbadala lakini naamini watakuwa nao. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI YA UPUNZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Waziri Mkuu, mfumo huu wa kisasa wa kiteknolojia kama nilivyosema umejaribiwa katika nchi mbili katika Bara la Afrika katika miaka miwili iliyopita kwa maana ya Ghana na Kenya, na kote mfumo huu umewaletea matatizo.

Lakini kikubwa zaidi ni kwamba mfumo huu usiposhirikisha wadau wengi tangu katika hatua zake za mwanzo kabisa za msingi za kutengeneza *software* ya kusimamia mfumo huu. Mfumo huu hauwezi kuja kuaminika kwa wadau wengine dakika za mwisho kama hawakushirikishwa katika *process* nzima ya kiutalaam.

Waziri Mkuu, sasa utakuwa tayari kwa niaba ya Serikali kutoa kauli ya Serikali kwamba sasa Tume isimamishe mara moja kuendelea kutengeneza mfumo huu hadi pale kwanza sheria itakapoangaliwa kwa sababu sheria bado hairuhusu na baada ya marekebisho hayo kufanyika na wadau kushirikishwa Taifa likubaliane kutumia mfumo wa *biometric* badala ya kuamuliwa tu na Tume bila wadau Wakuu wa Uchaguzi kwa maana ya Vyama vyote vya Siasa kushirikishwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mbowe ni lile lile linalotokana na hofu katika mifumo hii mbalimbali. Imekuwepo hofu hata tunapohesabu kwa vidole tena hiyo ndiyo mbaya zaidi, jitihada hizi za Tume ndiyo maana nimesema nadhani zina nia nzuri sana. Kama kweli katika kuandaa utaratibu mwingine kama huu *purely* wa kitaalam wa kimfumo ni lazima wadau tushirikishwe katika kuandaa *software* mpaka uje uanze kutoa, sina hakika kama kweli vyombo hivi vitaweza kufanyakazi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine Tume hii ina watu wenye uwezo mkubwa na mchanganyiko wake ule ndiyo umetoa imani kubwa, mimi siamini kwamba katika Tume ile tume yenyewe watashindwa kuambizana ukweli juu ya mfumo huo na nini, utazaa matunda gani, na kujenga imani ambayo sasa hivi inaleta hofu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba tu Mheshimiwa Mbowe kwa niaba ya wengine wote hebu tuiamini Tume hii katika kazi hii. Lakini mimi nitakachofanya ni kuwasilisha hili wazo kwenye Tume kwamba liko hili wazo, lakini bado naamini wanachojaribu kufanya ni kuepusha malalamiko ambayo yamekuwa yakitokea kwa muda mrefu.(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea, nitamwita Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Waziri Mkuu, hivi karibuni ulilifahamisha Bunge hili azma ya Serikali ya kuundwa kwa mfuko maalum ujulikanao kama (*Price Stabilization Fund)* wenye nia ya kutoa *compensation* kwa Wakulima wa mazao ya kibiashara kama vile korosho na pamba pindi mfumo mzima wa soko unapoathirika na wananchi kukosa bei ile iliyotarajiwa. *(Makofi)*

Kwa kuwa, wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara wameathirika sana na bei ya korosho katika kipindi cha msimu huu.

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu kuwalipa fidia wananchi wote ambao Vyama vya Msingi vimeshindwa kuwalipa kutokana na kuanguka kwa bei ya zao la korosho katika mikoa ya Lindi na Mtwara?*(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika hotuba, hili ni eneo moja ambalo lina changamoto kubwa kwa upande wetu kama Taifa, kwa sababu tatizo hili siyo korosho tu, tatizo hili ni tumbaku, tatizo hili ni pamba, tatizo hili mazao mengine mengi tu ya biashara ambayo tumekuwa tukitegemea soko la nje. Mtakumbuka kilichotokea mwaka jana wakati tulipopata tatizo la pamba. Tulishindwa kutoa fidia kwa sababu hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Mtanda sasa anaizungumza. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tu niwaombe Watanzania kwamba suala la fidia au kulipa fidia au kutokulipa fidia si jepesi ambavyo linaonekana. Tumeshaziagiza Wizara zinazohusika kwa ajili ya tatizo hili la korosho na kama tulivyosema tumeanza vile vile kuzungumza na wadau wa pamba. Mimi nafikiri tusubiri tuone matokeo ya zoezi hilo kwa upana wake halafu tuone ni namna gani pengine matatizo haya ya sasa lakini kubwa yale ambayo yatatukabili baadaye yatawеza kutatuliwa. *(Makofi)*

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu hapa Dodoma wamekuja Wenyeviti wa Halmashauri kutoka Mkoa wa Lindi. Halmashauri ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathirika sana na suala hili la korosho.

Je, uko tayari kukutana nao leo ili kuweza kupata undani na taarifa ya kina kuhusu athari ya kuanguka kwa zao la korosho katika Mkoa wetu wa Lindi na maeneo mengine ya nchi hii?

**SPIKA:** Yaani ndiyo unaomba *appointment* kijanja?(*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nadhani kuwaona siyo tatizo, tatizo ni maelezo watakayopewa. Kwa hiyo, nikipata nafasi nitawaona tu. Lakini nitaomba basi na Waziri wa Kilimo kama yupo na yeye tukae pamoja pengine wataelezwa walipofikia mpaka sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na MheshimiwA Diana Chilolo atafuatia.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Waziri Mkuu, Bunge la Tisa Wabunge hapa tulipitisha usafiri wa pikipiki za miguu miwili na ile ya miguu mitatu kutumika kama vyombo vya usafiri barabarani, kwa maana ya kuruhusu kubeba abiria na kuruhusu kubeba mizigo. Tofauti na matarajio pikipiki ya miguu miwili imekuwa ni chombo kinachoteketeza maisha ya Watanznaia kila kukicha, kila siku watu wanakufa barabarani.

Waziri Mkuu, Serikali ina mkakati gani wa kuokoa maisha ya Watanzania wengi wanaopoteza maisha kwa ajili ya kutumia vyombo hivi vya pikipiki.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba boda boda zimefurika kila mahali, hata ukienda vijijini sasa ziko nyingi sana. Lakini ni kweli vile vile kwamba vijana wetu wengi sasa ama wanakufa kwa sababu ya ajali zinazotokana na pikipiki ama wanapata majeraha makubwa sana

kutokana na ajali. Si rahisi kusema tutapiga marufuku suala la boda boda kwa sababu upande mwingine lina manufaa limesaidia sana kwenye usafiri lakini limewasaidia vijana vile vile kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama Serikali tulichofanya tumeamua sasa kushughulikia suala zima la elimu kwa wale wote ambao wanataka kujihusisha na matumizi ya pikipiki aina ya boda boda.

Tumeshaanza maeneo kadhaa na tunaendeleza hili zoezi. Tumejaribu kushirikisha hasa *VETA,* upande wa Polisi lakini tunashukuru kwamba kuna hata *NGO's* ambazo zimejitokeza na mfano mzuri sana upo Korogwe Mkoa wa Tanga ambako kumejitokeza *NGO* moja ambayo inafanyakazi nzuri sana. Kwa hiyo, nadhani kubwa ni elimu ambayo ni lazima tuisisitize kwa nguvu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine niombe tu vijana wangu wote ambao wameingia katika kujiajiri kwa kutumia bodaboda na wenyewe wawe makini sana tu kwa sababu ni vyombo vizuri lakini ni vyombo ambavyo ni hatari sana. Wajaribu kufuata taratibu watakazokuwa wanashauriwa na Halmashauri, kwa sababu tumeziagiza Halmashauri zote zijaribu kuchukua jambo hili la mafunzo kwa uzito unaotakiwa.(*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na jibu zuri la Waziri Mkuu, kwa kuwa, waendeshaji wengi wa vyombo vya pikipiki wamekuwa hawafuati kabisa sheria za barabarani na wamekuwa ni wajeuri kweli kweli na tunawaona barabarani kwa jinsi ambavyo hata wakisimamishwa na *Traffic* hawafuati kabisa maelekezo yale.

Waziri Mkuu, huoni sasa kuna umuhimu wa Serikali kuanza kozi maalum kwa waendeshaji wote wa pikipiki hata ya miezi mitatu ili waingie darasani wawe *trained* ili wakitoka kule angalau waweze kuokoa maisha ya watu yanayopotea?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Dada yangu Sakaya unalolisema wala hatutofuatiani kimtazamo, lakini na kiuhalisia. Hiyo ndiyo hali halisi tuliyo nayo, kwa sababu vijana hawa wapo kila mahali. Ukienda Vijijini ambako wala hutegemei utawakuta wapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachohitaji sasa ni mfumo au utaratibu ambao umepangwa vizuri wa kuwaainisha huko huko waliko na kutafuta namna, maana mafunzo ya miezi mitatu unayoyasema unajua yana-*assume* kwamba ni kundi lipo, lipo tayari, lakini fikiria walivyotawanyika nchi nzima, vijiji vyote.

Ni lazima sasa tutafute utaratibu ambao utawafikia huko huko waliko, kwa hiyo kama ni mafunzo yafanyike huko huko ili tuweze kuwapata wote katika mazingira yao. Ndiyo maana tumeona tutumie njia mbalimbali, vyombo mbalimbali, *NGO's* kwa sababu *basically* ni suala la elimu zaidi upande wa sheria za barabarani, lakini na kuacha ule uchu maana sasa wengine suala la mshikaki ndiyo namna ya kubeba watu, anabeba watatu mpaka wanne wakipata ajali maana yake wote wale wanateketea.

Lakini la Pili, wengine hata sheria ya kuvaa *helmet* tu hawavai. Kwa hiyo, vyote hivi vinataka elimu ambayo kidogo iko chini ya utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna tulivyolianza nafikiri tutaenda tunapunguza hiyo kasi ya ajali pamoja na vifo ambavyo si vya lazima. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika ahsante. Waziri Mkuu, kwa kuwa wafanyakazi karibu nchi nzima wamekuwa wakilia na mishahara, hasa kada ya Ualimu pamoja na kuongezewa mishahara, kwa sababu ya makato wanayopata ya kodi ya Mapato kupitia mishahara yao na kufanya mishahara yao kuwa midogo.

Kwa mfano Mwalimu anayeanza kazi anapata shilingi laki mbili na sabini na saba, anakatwa kodi ya mapato asilimia 14, kiasi ambacho ni kikubwa kinafanya mshahara wake kuwa mdogo hata kama ataongezewa.

Je, Serikali haioni kuwa kuna kila sababu sasa, kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi hii ya mapato kwenye mishahara ya wafanyakazi na kuangalia eneo lingine kufidia makato hayo kwa kuwa nchi yetu imejaliwa maliasili nyingi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watumishi wote tu kwa ujumla wanakatwa kodi ya mapato na kwa hiyo Serikali inatumia mfumo huo kama ni namna nyingine ya kupata mapato yake Serikalini.

Lakini ni kweli vile vile kwamba makato yale yakiwa makubwa yanapunguza sana thamani ya hicho mnachokiita kwamba ni mshahara. Serikalini tumeshaanza kulitazama hilo ambalo Dada Chilolo analisema, matumaini yetu ni kwamba tutafika mahali tutaona namna nzuri ya kuweza kushughulikia hili suala la kodi kwa Watumishi kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri Mkuu kwa majibu yake mazuri, lakini napenda kuuliza.

Kwa kuwa, watumishi hawa ni binadamu kama binadamu wengine, hukopa mikopo maeneo mbalimbali ya mabenki kwa ajili ya kuendesha maisha yao, lakini mikopo hiyo pia imekuwa ni kero kwao kwa sababu ina riba kubwa.

Je, Serikali haiwezi kufikiria kwamba angalau basi wafanyakazi wawekewe kiwango chao cha riba kingine tofauti hata na wafanyabiashara, ili waweze kumudu mikopo hii ambayo sasa imekuwa ni kero kwao?(*Makofi*)

**SPIKA:** Swali lingine tena, haya. Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, litafuatana na swali la msingi, lakini. Ni kweli, riba kwenye mabenki ni kubwa, hata Wabunge hapa unaona, mara nyingi tumelisema sana na Serikali, kwa nyakati tofauti imekuwa ikitumia utaratibu wa kawaida wa kusimamia na kudhibiti suala hili la riba. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni lazima tuendelee kuwa tunalifanyia kazi kwa sababu, linahitajika karibu katika maeneo yote ya utumishi, lakini vilevile na shughuli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwangu, hili ni rahisi kidogo kuweza kusema tunaweza tukafanikiwa baada ya jitihada kubwa kufanyika. Lakini eneo ambalo ninataka niwaase tu watumishi kwa ujumla ni pale wanapokwenda kuchukua mikopo kutoka kwenye vyombo ambavyo ni nje ya vyombo kama mabenki; vyombo vingine hatuvijui, hatujui vinavyofanya kazi zake na wakati mwingine wanatozwa riba kubwa zaidi kuliko hata ile ya kwenye mabenki. Mwisho wa yote unakuta hawapati kile ambacho walikuwa wanategemea.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na kesi za namna hiyo. Niwaombe tu watumishi wote kwa ujumla hata kama wanataka kuingia kwenye mifumo hiyo ambayo ni tofauti na ya kibenki, ni vizuri basi kwanza mpate maelezo kutoka kwenye Serikali zenu za Halmashauri juu ya uhalali na uwezo wa vyombo hivyo. Maana vingine kwa kweli, viko pale kujitajirisha tu, badala ya kuwasaidia kwa maana ya mikopo. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii ya dhahabu, kumwuliza Waziri Mkuu, swali dogo sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa nini Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, akazuiliwa ziara Mkoa wa Mtwara, wakati Mawaziri wengine wa Jamhuri ya Muungano wameruhusiwa na wanafanya ziara na mikutano? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama kawaida Mheshimiwa Eng. Mohammed Mnyaa, anasema dogo sana. Swali lake sio dogo, linataka maelezo kidogo. Hatukuzuia ziara yake hata kidogo, aliomba kufanya ziara ya Kichama Mtwara.

Tulichomwomba kupitia Ofisi yake ni kwamba kwa muda hivi tulikuwa tumeamua kwamba, mikutano ya vyama isitishwe kwa pande zote Chama Tawala na Vyama vingine, ili tuendelee kushughulika na matatizo yaliyokuwa yamejitokeza pale ndani hadi hali itakapokuwa imerejea na kuwa shwari. Kwa hiyo, tukawasihi sana kwamba, watuelewe kwamba nia yetu ilikuwa ni nzuri tu hatukuwa na nia mbaya katika jambo hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini bado ni kweli, kama unavyosema. Inapokuwa ni jambo la Kiserikali, tunakwenda kufanya kitu Fulani, hilo hatulikatai; kwenda kufungua sijui nini, wanataka kwenda kuweka jiwe la msingi, na kadhalika. Tulisema halina tatizo hata kidogo. Matumaini yangu ni kwamba, ujumbe ulifika na nia hiyo ninayoisema kwa wakati ambao tulikuwa tumeomba lifanyike hivyo. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, vyama vya siasa vimeruhusiwa Kikatiba kufanya shughuli za siasa Tanzania, sasa ni lini kwa wastani hizi shughuli za Mtwara zitakamilika, ili vyama sasa viruhusiwe kufanya siasa? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ukiniuliza ni lini hasa, sio rahisi. Lakini imani yangu ni kwamba, hatutachukua muda mrefu kurejesha hiyo hali ya mikutano kama kawaida kwa sababu, jambo lenyewe tunaendelea kulishughulikia sasahivi. Tujaribu kuzungumza na wadau pale, tujaribu kuwaelimisha, ili waweze kujua nia ya Serikali katika jambo hili ni nini.

Kwa hiyo, ninataka nikuahidi tu huyu mzee haitachukua muda mrefu sana *indefinitely,* kabla hajaruhusiwa tu kwenda na viongozi wengine tu tutawaruhusu kwenda.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo waombaji walikuwa wachache. Kama tulivyosema utaratibu wetu bado hatukuutengeneza vizuri wa namna ya kuomba kuzungumza kwa sababu, tulikosa muda kwa sababu ya mambo mengine, lakini kama tulivyoahidi tutafanya hivyo.

Tukushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu mazuri kwa maswali yaliyoulizwa na wahusika wote. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. *(Makofi)*

Katibu tuendelee?

## MASWALI YA KAWAIDA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali. Na mwulizaji maswali ni...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Wakati wa Maswali, sitaki Mwongozo kwa sababu, haupo Mwongozo wowote. Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, kwa niaba yake Mheshimiwa Mhonga.

Na. 61

**Utafiti Juu ya Uwakilishi wa Wanawake Bungeni**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Nafasi za Ubunge wa Viti Maalum, zinaonekana kuwa zinatolewa kwa upendeleo na hazithaminiwi sana kama Wabunge wa Majimbo:-

Je, Serikali, ipo tayari kuzifadhili Taasisi za Wanawake zifanye utafiti maeneo mengine Duniani, ili kupata mfumo mzuri wa uwakilishi wa Wanawake Bungeni na kuondoa dharau iliyopo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Viti Maalum, wanachaguliwa kwa mujibu wa Ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kulingana na utaratibu, vyama vya siasa vinavyoshiriki Uchaguzi Mkuu na kupata walao 5% ya kura zote halali za Wabunge, vitapendekeza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, majina ya Wanawake ambao watateuliwa na Tume kuwa Wabunge wa Viti Maalum. Uteuzi huo utazingatia uwiano wa kura ambazo kila Chama kimepata katika uchaguzi wa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa, vina utaratibu vilivyojiwekea wa kuwapata wanawake wanaoteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kuwa Wabunge wa Viti Maalum.

Ni kweli, kumekuwa na malalamiko kuhusu upatikanaji wa majina ya Wabunge hawa. Hata hivyo, kwa kuwa, shughuli ya kuandaa Katiba Mpya inaendelea, Serikali, haioni umuhimu wa kufadhili taasisi za utafiti. Naamini Katiba Mpya, itatupa utaratibu mpya wenye heshima na mzuri wa namna ya kwapata Wabunge Wanawake. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ipo dhana inayoonekana kwamba, Wabunge wa Viti Maalum, hawathaminiwi na vilevile wanadharauliwa. Sasa naomba kuuliza maswali mawili. Kama kweli, Wabunge wa Viti Maalum, hawadharauliwi na wanathaminiwa kwa nini, Sheria ya Mfuko wa Jimbo imewabagua?

Serikali, haioni kuna haja sasa ya kuleta Sheria hiyo ili iweze kurekebishwa, ili nao waweze kupatiwa fedha za Mfuko wa Jimbo, kutekeleza ahadi zao kwa sababu, wanahudumia eneo kubwa ambalo ni Mkoa, tofauti na Jimbo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kama kweli hawadharauliwi na wanathaminiwa, kwa nini Wabunge wa Viti Maalum hawaruhusiwi kuingia katika Kamati za Fedha katika Halmashauri zao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijibu swali moja na swali jingine atajibu Mheshimiwa Mwanri, juu ya Kamati za fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba, hakuna dharau yoyote kwa Wabunge wa Viti Maalum, hakuna. Bunge hili haliwadharau na kama mnajua hata mambo yote hapa Bungeni hapa, wale waliokuwepo tangu mwaka 1995 Wabunge wa Viti Maalum, hamkuwa hivi. Yako mambo mlikuwa hampati hapa, Waheshimiwa akina Mary Nagu, wanajua.

Baada ya miaka 5 akina Mheshimiwa Sanya hawa wanajua, tuka *compromise* tukasema wote ni Wabunge kwa mujibu wa Katiba, wote ni Wabunge sawa mnapata vitu vingine sawasawa na Wabunge wa Majimbo, hakuna dharau. Serikali na Wananchi wanawaona ninyi ni Wabunge kama Wabunge wengine, naomba mjiamini wenyewe. Msijiamini kwamba, mnadharauliwa, hakuna dharau yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini juu ya Jimbo, kwanza twende tu Mheshimiwa Mhonga, tafsiri ya Jimbo ni nini?

Kwa mujibu wa Katiba yetu tafsiri ya Jimbo, ni eneo, lina ukubwa, lina watu. Kwa hiyo, twende kwa tafsiri tu, kwa tafsiri ya Jimbo ni kwamba, kuna Wabunge sasa ukirudi kwenye mchanganuo kuna Wabunge wa Majimbo kuna Wabunge wa Viti Maalum.

Sasa posho hii inayokwenda, inakwenda kwa kundi hili la wenye Majimbo ambaye anajulikana kwa eneo Kikatiba kwamba ni Wabunge wa Jimbo, hawa ndio wanahudumia. Wabunge wa Viti Maalum, ndio maana utaratibu huu umewekwa kwenye vyama kutokana na kura za uwiano. Ninyi mnachangia shughuli za maendeleo katika maeneo yale yale ambayo yana Majimbo tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatuna tuna mpango wa kuangalia wala wa kuwapa fedha Wabunge wa Viti Maalum, sitai-*commit* serikali, ila naweza nikasema labda, fedha hizi ziongezwe.

Kama uwezo wa Serikali, utaruhusu fedha hizi ziongezwe kwa sababu, wananchi wanahudumiwa kwenye Majimbo na wanapohudumiwa kwenye Majimbo ni wananchi wote. Tuliomba tu kwamba, wale Wabunge wa Majimbo, washirikiane na Wabunge wa Viti Maalum katika kupanga shughuli hizi za maendeleo wanazozitekeleza kwenye Majimbo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimeona tu nisimame, kwa sababu jambo hili mara nyingi linazua mjadala mkali sana hapa. Lakini siku za nyuma niliwahi kulieleza kwamba, mkisoma vizuri ile Sheria, inacho kipengele vilevile kinachoruhusu Viti Maalum, kutengenezewa utaratibu wa Kisheria kabisa wa uwezekano wa kuwa na Mfuko wa aina Fulani.

Ninaomba kwa msingi huo, hebu jaribuni kulianzia pale, tujenge hoja tuone namna ambavyo itavyopokelewa ndani ya Serikali. Lakini kwa sasa ilivyo haitawezekana kwa sababu, Mfuko ule ulitengenezwa mahususi kwa ajili hiyo, wakiamini kwamba, maeneo yale ambayo tuna mahusiano mazuri si tatizo hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na nilitoa mfano nikasema kama Jimbo langu mimi, *actually,* mara nyingine nakuwa sipo tu. Lakini Mbunge Viti Maalum, ndiye Mwenyekiti wa hiyo Kamati. Sasa inategemea kati ya Jimbo na Jimbo, lakini njia rahisi hebu mrudi mkaione ile Sheria, tafuteni kile kipengele, jaribuni kukitumia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanri, *part* ya pili ya swali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la pili la Mheshimiwa Mhonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii Kamati anayoizungumzia ya fedha, wakati mwingine inaitwa Fedha na Uchumi na Mipango, inategemeana na kama unazungumzia katika Halmashauri za Miji au unazungumzia katika Halmashauri za Vijijini, itategemeana.

Kamati hii, wanaoingia katika ile Kamati ni Wenyeviti wa kamati zile nyingine zote zilizoko katika Halmashauri pamoja na Wajumbe wengine wawili ambao wanateuliwa kupitia Mwenyekiti wa Halmashauri *in collaboration* na *District Executive Director* au kama ni *Municipal Director, whoever.*

Hawa wote kwa pamoja ndio wanashirikiana majina yale mawili yakishapatikana wanakwenda sasa katika Baraza na katika Baraza ndipo majina yale yanapopitishwa na Madiwani wote walioko katika ile Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa upande wa Viti Maalum kwa sababu haya yote ambayo mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyazungumzia, mara kwa mara *experience* imeonesha kwamba, tumemtaka Mbunge, *at least* aji-*identify* na Halmashauri moja.

Akishaji-*identify* kwa sababu huyu Mbunge tunayemzungumza huyu anakwenda Mkoa mzima, Akishaji-*identify* pale, yule Mwenyekiti pamoja na *DED* wakija na jina pale, wakasema ni huyu wa Viti Maalum tunataka tumwingize pale, hakuna mahali Sheria imekataa kwamba, asiingizwe pale, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tulishajibu mara nyingi sana hapa mimi anayenizaa ni mama, mke wangu ni mama, wewe Spika ni mama, hakuna mahali popote ambapo tuna-*look down upon women.* Kwanza, *actually,* tunashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pia, anaanza kuzungumzia hilo mimi nadhani kuna haja ya kukaa na kufikiri zaidi kwamba, tufanye nini katika suala hili, lakini *there is no problem at all;* sisi tunayapokea haya yote, tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Andrew John Chenge, si nilikuona? Kama hayupo basi, Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na kuwa jibu la msingi limeshajibiwa, lakini nilikuwa ninataka tu kuona kwamba, katika ule Mfuko wa Bunge, pia hata sisi tungekuwa tunaruhusiwa kuingia kwenye ule Mfuko wa Jimbo. Kwa sababu, hata kuingia kwenye ule Mfuko wa Jimbo, Mbunge wa Viti Maalum haruhusiwi kuingia, ni kwa nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria inasema Madiwani na Mbunge ni Diwani. Sasa kwa kweli, haya mambo ni ya ushirikiano tu. Sehemu nyingine Wabunge wa Viti Maalum, wanashirikiana na Mbunge, kuainisha mahitaji ya ile Wilaya, kama Mbunge wa Viti Maalum anajihusisha na Majimbo hayo unajua mambo haya ni ya kisiasa? Sasa kama Mbunge anajihusisha na Jimbo hilo kikazi, yule Mbunge wa Jimbo, anamhusisha katika mambo yake yote. Wanahusishwa, lakini nichotaka kusema ni kwamba, Sheria ile imeweka wazi kwamba, kuna Madiwani kadhaa, kuna Watendaji kadhaa wa Kata, ambao watateuliwa katika Mkutano ule wa *Full Council.*

Mheshimiwa Spika, sasa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama Sheria ile ya Mfuko ina utata, kwa sasa ndivyo ilivyosimama; tuzungumze, tuko hapa Bungeni, tuliotunga ni sisi. Tuone jambo gani linalowezekana kufanya mapitio na marekebisho tulirekebishe.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatufungulia hapa. Naomba tushirikiane kuangalia ile Sheria kama tulivyoshirikiana kuangalia ile Sheria kwa upande wa Zanzibar, tushirikiane kuangalia Sheria yote ya Mfuko wa Jimbo, ili tuone kama kuna mapungufu ambayo yanawabagua Wabunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Na. 62

**Kuchelewa kwa Mishahara ya Walimu Shule za Vijijini**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Walimu wanaoajiriwa katika Shule za Vijijini, huchukuwa miezi mitatu na zaidi bila kulipwa mishahara ambayo ni haki yao ya msingi.

(a) Je, Serikali, haioni kwamba, inawanyima Walimu hao haki yao ya Kikatiba?

(b) Je, Serikali, haioni kwamba, ugumu huu wa maisha husababisha Walimu hao kuondoka katika maeneo yao ya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, huwahudumia Walimu wapya wanaoajiriwa bila kujali wamepangwa katika shule za Vijijini au Mijini, ikiwemo kulipwa mishahara na stahili zao nyingine. Mishahara kwa waajiriwa wote hulipwa baada ya mwajiriwa kujaza fomu za ajira kuwasilisha taarifa binafsi, ikiwemo vyeti vya kitaaluma na kitaalam. Baada ya hatua hizo Halmashauri, huwaingiza katika mfumo wa malipo – *Lawson Version 9,* ambao hupeleka moja kwa moja majina hayo kwa njia ya mtandao Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuidhinishwa na maandalizi ya malipo ya mshahara katika mwezi husika. Mwalimu, akikosa mshahara na yupo kituoni, Mkurugenzi anawajibika kumhudumia.........

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuko Bungeni, naomba vikao vidogo vidogo mviondoe.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** ............. Mwalimu akikosa mshahara na yupo kituoni, Mkurugenzi anawajibika kumhudumia, ili aweze kujikimu. Aidha, Serikali, ipo tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, kupata taarifa za kuwepo Walimu ambao wameajiriwa, hawajaingia katika mfumo wa malipo na hawajahudumiwa na Mkurugenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi, wakiwemo Walimu, Serikali, imekuwa inatuma fedha za posho katika Halmashauri, kabla ya Walimu kuripoti.

Aidha, Serikali, inaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi watumishi, ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu, kupitia Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari *(MMES II).*

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya maeneo nchini kumekuwa na changamoto za mtandao kufanya kazi taratibu na hivyo kusababisha baadhi ya Walimu, kutoingia katika orodha ya malipo kwa wakati. Ninawasisitiza Wakurugenzi wa Halmashauri, kuhakikisha Walimu wote ambao hawajaingia katika orodha ya malipo wanahudumiwa ipasavyo wakati taratibu za kuwaingiza katika orodha ya malipo zinafanyika. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri na yenye ufasaha. Lakini naomba nimwulize maswali mawaili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza wakati nauliza swali hili ni tangu mwaka 2012, nilikuwa na ushahidi wa kutosha, lakini kwa sasa hawa wameshapatiwa malipo.

Lakini naomba niulize. Je, kwa sababu, mara nyingi yanatokea haya matatizo ya Walimu kucheleweshewa mishahara, pamoja na kwamba Waziri amesema haichelewi. Lakini bado kuna malalamiko mengi ambayo Walimu wanalalamika kwa kucheleweshewa mishahara, hasa Walimu walioko Vijijini.

Kwa nini, Serikali, isiajiri kipindi cha Julai, ambapo Bajeti yao imeshapitishwa tayari, wakaweza kupata mishahara yao kwa wakati maalum?

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunapoajiri walimu tunaajiri walimu wa kike na wakiume na tunawapeleka katika maeneo ya vijijini na huko kunakuwa na mazingira magumu pindi inapotokea mwalimu amecheleweshewa kupata mshahara au hata hiyo posho, Mkurugenzi kachelewa kumpatia ili aweze kujikimu.

Hatuoni kama mwanamke huyo tunamweka katika mazingira magumu na majaribu makubwa yeye kufuata posho huku kufuatilia kila wakati hatuoni kama tunamuweka mwanamke katika majaribu magumu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwalimu pale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu walimu wote ambao wameripoti kuanzia tarehe moja mpaka tarehe tisa wamepata mishahara yao kama kawaida na walimu walioripoti ni 16,000 na wote wamepata mshahara wao. Wale ambao wameripoti baada ya tarehe tisa na tulitoa tangazo maalum wale ndiyo waliokosa mshahara kwa sababu *process* ilifanyika kwa wale walioripoti mpaka tarehe tisa kwa taasisi zote.

Mheshimiwa Spika, swali la pili posho za kujikimu zilitangulia kabla walimu hawajafika. Zilitangulia katika Halmashauri zote na Hazina walitoa shilingi bilioni 8 kwa ajili ya posho za kujikimu.

Kwa hiyo ukiona mwalimu analalamika au hakupata mshahara wake ameripoti kwenye kituo ambacho siyo chake na akiripoti kwenye kituo ambacho siyo chake mfumo wetu wa *Human Capital Management Information System* unamkataa, unamtema. *(Makofi)*

Kwa hiyo walimu wengi ambao unaona wako mitaani sasa hivi hawataki kuripoti Kigoma, Nkasi na sehemu nyinginezo. Lakini sisi tuko imara tunahakikisha kwamba wote ambao tumewapangia katika sehemu husika hasa vijijini hatukupanga wengi kwenye manispaa, wote walioripoti wamepata mishahara yao na mimi ninaripoti hapa ya walimu wote ambao wameripoti na wamepata mshahara wao na wamepata marupurupu yao kwa wakati.

Kwa hiyo, niwaombe wale walimu ambao sasa hivi wanazunguka mitaani maana yake kibali kilikuwa cha walimu 28,000 walioripoti ni 16,000 hatutawabadilishia sehemu za kazi hata siku moja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru moja kati ya haki ya kikatiba ya mwalimu ili kumwezesha kupata kipato chake vizuri ni pamoja na kuongezwa ama kupandishwa daraja pale ambapo wanakidhi vigezo vya kupandishwa daraja sasa kumekuwa kuna matatizo makubwa ya walimu nchi nzima na *specifically* Wilaya yetu ya Kinondoni na jana nimepata kutoka Wilaya ya Mbinga Walimu wanalalamika tokea mwaka 2008 hawajapandishwa madaraja.

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anifahamishe ni lini tatizo hili la madaraja kwa walimu litakwisha na ni lini vile vile malimbikizo ya fedha za walimu ambazo zimetokana na kupandishwa daraja na kutokulipwa zitalipwa na hili tatizo kumalizika? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujafunga ule mfumo wa *Lowson nine* yaani wa taarifa za watumishi pamoja na mishahara tatizo la malimbikizo lilikuwepo lakini kuanzia mwaka 2011 mfumo ule ulivyoanza kufanya kazi mwalimu pindi anapopandishwa daraja mwezi huo huo akiingizwa kwenye mfumo wetu anapata malimbikizo yake kwa sababu yanajumuishwa kwenye mshahara.

Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba kuna matatizo ya huko nyuma hayo tunayamalizia walimu watalipwa haki zao na wanaopandishwa vyeo kuanzia sasa watakuwa wanalipwa mara moja bila kucheleweshewa. *(Makofi)*

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa walimu walio wengi hupenda sana kufanya kazi mijini na Wilayani kuliko sehemu za vijijini na kwa kuwa wapo walimu wengine ambao wangependa sana kufanya kazi vijijini hasa sehemu walimotoka.

Je, Serikali sasa inasemaje kuhusu kuwepo na utaratibu au Kanuni inaowapa kipaumbele walimu wanaomaliza masomo yao kupangwa wanamotoka hasa vijiji wanamotoka ili kuepukana na tatizo hili la walimu kutokuripoti?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwaiposa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo hilo tumeendelea kulipata na tunalishughulikia lakini walimu huwa wanaonyesha mapenzi yao ya wapi wanataka kwenda kufanya kazi wakati ule wanajaza fomu zile za kuomba ualimu wana-*indicate* na kwa ujumla tunafuata kwa kadiri

tunavyoweza mapendekezo ya mtu, chaguo la kwanza, la pili na la tatu na pengine tunazidi hapo kwa sababu wengi wanapenda yale maeneo ya mjini ambapo kuna walimu wengi.

Lakini pia tunapokuwa tumeshindwa kabisa tunapokea maombi yale ambayo yanaenda *specific* kwa kijiji alikotoka na kama nafasi ipo hapo tunampeleka na kufanya mabadiliko hayo mwanzoni kabisa kwenye uchaguzi lakini siyo baada ya tumesha-*post* kwa sababu tukifuata yale matakwa inaonyesha kwamba kuna Mikoa ambapo haitopata Walimu kabisa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwa mfano walimu wa Sayansi wasizidi watano ndiyo wamechagua kama chaguo la kwanza na la pili Mkoa mzima wa Lindi, wawili chaguo la kwanza, wawili chaguo la pili hatuwezi Mkoa wa Lindi tukapeleka walimu wa Sayansi na Hisabati wawili tu. Kwa hiyo, hili tatizo tunalo tunaendelea kutafuta suluhisho lakini ni gumu tutaomba tu Waheshimiwa Wabunge pamoja na walimu kwa ujumla watuelewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tumetumia muda mwingi sana kwa swali hilo moja, tunaenda Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Omari Nundu, atauliza swali hili.

Na. 63

**Ufufuaji wa Viwanda Tanga**

**MHE. OMARI R. NUNDU** aliuliza:-

Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010 inaitaka Serikali kuendeleza Viwanda Nchini na kwa msingi huo kuiomba Serikali kulirejesha Jiji la Tanga kuwa la Viwanda kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kabla ya viwanda vilivyokuwepo kubinafsishwa na kutekelezwa bila kufanya kazi:-

(a) Je, ni matayarisho yapi yanafanywa na Serikali kuweza kufikia azma hiyo katika kipindi cha mwaka 2010-2015?

(b) Je, ni nini hatma ya viwanda vya zamani vya sabuni vya mbuni, Foma, Gardenia na kadhalika, Kiwanda cha mashati cha Gosage na cha nguo cha *CIC;* kiwanda cha mbao cha *Sikh,* kiwanda cha chuma, kiwanda cha *Amboni Plastics* na kiwanda cha mbolea ambavyo vilimilikiwa na Serikali na vingine watu binafsi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari R. Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuufanya Mkoa wa Tanga kuwa Jiji la viwanda upo katika hatua nzuri. Kwa hivi sasa viwanda vipya vilivyojengwa na vinavyojengwa ni pamoja na kiwanda cha *Nil cant* cha kutengeneza chokaa, kiwanda cha *Rhino Cement* pamoja na kiwanda cha *Sungura Cement* kinachotarajiwa kujengwa.

Aidha Jiji la Tanga limeingia ubia na Kampuni ya Korea inayoitwa *Good PM* kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa kujenga viwanda kumi na tano katika eneo la hekari 73 huko Kongwe unaotarajia kuanza mwezi Mei mwaka huu 2013 chini ya utaratibu wa *Tanga Economic Corridor*.

Serikali kupitia mamlaka ya *EPZ* imetenga eneo lenye ukubwa wa hekta 1363 katika Mkoa wa Tanga kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na uthamini wa eneo husika umekamilika. Pamoja na eneo hilo *NDC* imetenga eneo lingine la hekta 50 huko Kange Mbugani, Tanga kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatma ya viwanda vilivyokuwa hapo zamani ni kama ifuatavyo. Kiwanda cha sabuni cha *Foma* kipo na kinaendeshwa na *Murzar Soap* na *Detergent Industries Limited,* kiwanda cha *Tip Soap* bado kipo na kinazalisha sabuni, kiwanda cha nguo cha *CIC* kinaendeshwa na *Afritex* na kinazalisha nguo.

Kiwanda kingine ni Kiwanda cha Chuma kinakarabatiwa na mazungumzo kati ya Mwekezaji na *CHC* yanaendelea ili kuweza kuanza kazi, Kiwanda cha Mashati cha *Gossage,* kiwanda cha siku nyingi, kiwanda cha *Gardenia* na kile cha *Amboni Plastic* vyote havifanyi kazi wakati kiwanda cha mbolea kimebadilishwa matumizi na sasa eneo hilo linatumika kama sehemu ya kihifadhi mafuta. *(Makofi)*

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, niipongeze Serikali kwa hatua hizo ambazo zimechukuliwa na uhusiano uliopo katika Wilaya na Halmashauri hasa Madiwani wa CCM kuhakikisha kuwa mambo haya ambayo ametaja yanatokea.

Lakini ukweli bado upo kwa kuwa hata viwanda ambavyo vinafufuliwa kwa maelezo ya Waziri mwenyewe vinasuasua havifufuliwi kwa kasi ile ambayo inayotakiwa. Sasa mimi nina maswali mawili.

(a) Serikali itakuwa tayari kufanya tathmini ya kina ili kuona vile viwanda ambavyo vinasuasua katika ufufuliwaji wake. Waswahili tunasema ni kama danganya toto tu wapewe wananchi wa Tanga ambao wako tayari kuviendeleza na pia kwa nchi nzima?

(b) Swali langu la pili linahusu kiwanda cha kiwanda cha mbolea ambacho hapa kinaelezwa kuwa kimebadilishwa matumizi. Kiwanda cha mbolea kama kiwanda cha mbolea ni sehemu ndogo tu haifikii hata hekari kumi lakini sasa hivi eneo ambalo limewekwa nikiambiwa kuwa litawekwa kwa ajili ya kuhifadhi mafuta katikati ya Jiji la Tanga sehemu ambayo ni *prime* ni hekari 136 na hakuna kinachoendelea ni msitu mkali ambao hata watu, maiti zimekutwa kule.

Sasa Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba ubadhirifu kama huu wa mtu kuchukua sehemu kubwa katikati ya Jiji, *prime area* asilifanyie chochote, aiweke tu irudishwe katika Halmashauri ya Tanga ili litumike kuliendeleza Jiji la Tanga ambalo halina hata sehemu ya watoto kuchezea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana kwa kutambua juhudi za Serikali na ya Mkoa ya kufufua. Kuhusu swali lake la kwanza kwamba kama Serikali iko tayari kufanya tathmini na kama ipo tayari kuwapa wananchi wa Tanga kufufua viwanda ambavyo bado wawekezaji waliopewa hawakufufua.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ninakubaliana kama kutakuwa na mtu wa Tanga ambaye anapenda kufufua kiwanda pale kwa manufaa ya Mkoa wa Tanga na baada ya kufanya tathmini kuona mwekezaji aliyepewa hachukui juhudi zinazotakiwa sidhani kama Serikali itasita kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kiwanda cha mbolea ambacho eneo lake matumizi yake yamebadilishwa kuwa mahali pa kuuzia mafuta na miti sasa na kwamba msitu umeota kule ninakubaliana naye kwamba lazima tuchukue hatua za haraka kuona kwamba msitu hauoti katikati ya mji na kwamba eneo lile linatumiwa kwa viwanda kama ilivyopangwa tangia awali, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, mimi ningependa tu kumwuliza kwamba kuna viwanda vingi sana hapa nchini ambavyo ni kama vimekufa havifanyi kazi. Sasa angenisaidia tangu Wizara yake ya uwezeshaji imeundwa ameshaweza kusaidia viwanda vingapi ambavyo vinafanya kazi sasa hivi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, huyu anajibu kwa niaba ya Waziri wa viwanda lakini jibu tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ni moja, kazi ya Waziri wa viwanda vinashamiri, kazi ya Waziri wa Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kutafuta na kuhamasisha wawekezaji wawekeze kwenye viwanda na maeneo mengine. Tutashirikiana sana na Waziri wa Viwanda na Biashara kufanya hivyo.

Lakini ni kweli kabisa kwamba Serikali imefanya tathmini na kuona kwamba ni viwanda vipi vilivyobinafsishwa vinafanya kazi na vipi ambavyo havifanyi kazi vizuri kwa ajili ya kuweza kuchukua hatua zinazofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwamba kuanzia miaka ya tisini, Tanzania imekubali kuwa nchi ya uchumi wa soko na kwenye uchumi wa soko ni jambo la kawaida kwa viwanda kuingia na kutoka biashara na wawekezaji wanaenda pale ambapo kuna faida na ambapo kiwanda hakitoi faida itakuwa ni jambo la kawaida kuona kwamba mfanyabiashara au mwekezaji anaondoka pale.

Ni kazi ya Serikali kuona kwamba kama kuna mahitaji makubwa basi na yenyewe inaingia pale, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, muda wenyewe unakuwa mdogo, Wizara ya Ujenzi Mheshimiwa Ester Bulaya, swali linalofuata.

Na. 64

**Zabuni ya Ujenzi wa Barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Serikali ilishaahidi kutangaza zabuni ya ujenzi wa barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya, lakini mpaka sasa bado zabuni haijatangazwa.

Je, Serikali itatangaza lini zabuni hiyo ili ujenzi wa barabara hii uanze?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mbunge viti maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya ni kiunganishi muhimu kati ya Wilaya ya Bunda Mkoa wa mara na visiwa vya Ukerewe Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa zabuni ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya, sehemu ya Kisorya-Bunda yenye urefu wa kilomita 82 imetangazwa tarehe 28 Machi, 2013. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na natambua jitihada za Serikali katika kuhakikisha zinaboresha miundombinu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii yote ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na tulitegemea zabuni itangazwe kwa yote lakini hapa zabuni imetangazwa kwa barabara ya Bunda-Kisorya kama *Lot Number Two.*

Sasa huwezi ukatangaza *Lot Two* kabla ya *Lot One* na katika vitabu inaonyesha kabisa Mkoa wa Mara umetengewe bilioni 8 tu na hizo ni kwa ajili ya ukarabati wa barabara ambazo zimeshatengenezwa.

Lakini haionyeshi Bajeti ya ujenzi wa barabara hizi Bunda-Kisorya, Nyamuswa Kisorya sasa nataka kujua katika Bajeti hii ni shilingi ngapi ambazo zimetengwa kwa ujenzi wa kiwango cha lami kwa vipande vyote viwili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili tunajua sasa hivi kuna upanuzi wa barabara unaendelea katika Mkoa wa Mara kutoka Mwanza kwenda Musoma sasa katika hiki kipande cha Bunda Musoma tayari tathmini imeshafanyika kwa wahanga ambao wamepitiwa na huo mradi nataka kujua ni lini sasa watalipwa wale wahanga ambao wameguswa na huo mradi na eneo la Bunda - Musoma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba tukupongeze Mheshimiwa Bulaya kwa namna unavyofuatilia maendeleo ya miundombinu katika Mkoa wa Mara. Barabara ya kutoka Nyamuswa mpaka Bunda mpaka Kisorya mpaka Nansio ni barabara moja, lakini tumepanga kuanza na hicho kipande cha kutoka Bunda kwenda Kisorya sababu ya mbili muhimu.

Kwanza ukichukua kipande cha kutoka Nansio mpaka pale kwenye feri kuna daraja ambalo usanifu wake haujakamilika na pia ukichukua kutoka Bunda mpaka Nyamuswa kuna maeneo ambayo watu wengi wameingia kwenye eneo la Hifadhi ya barabara. Kwa hiyo ni maeneo ambayo bado tuna-*sort out* ili kusudi tuweze kuona tunapotangaza kazi ya ujenzi kusiwe na vikwazo.

Mheshimiwa Spika, pili nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Spika kwamba Bajeti ambayo tutaanza kutekeleza hiyo sehemu ambayo tumeitangaza ipo na tutakapowasilisha hotuba ya Waziri wa Ujenzi itaonyesha fedha ni kiasi gani zimepangwa. *(Makofi)*

Na. 65

**Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati**

**MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MHE. ZABEIN M. MHITA)** aliuliza:-

Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati unatekelezwa kwa kasi ndogo sana:-

(a) Je, Serikali imeingia Mikataba na Makandarasi gani kwa barabara hiyo?

(b) Je, ujenzi wa barabara hiyo utakamilika lini kwa kiwango cha lami chini ya mikataba hiyo?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya makandarasi hao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati yenye urefu wa kilometa 247.8 unatekelezwa kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza inayohusu ujenzi wa sehemu ya Barabara ya Babati – Bonga yenye urefu wa kilometa 16 na Bicha – Kondoa yenye urefu wa kilimeta 3.2 ulianza Desemba, 2010. Mkandarasi anayejenga sehemu hii ni Kampuni ya *China Henan International Corporation Group Co. Ltd. (CHICO)* kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa gharama ya shilingi bilioni 19. 77. Awamu ya pili inayohusu ujenzi wa sehemu ya Barabara ya Dodoma – Mayamaya yenye urefu wa kilometa 43.65, ilianza tarehe 20 Juni, 2011. Mkandarasi anayejenga sehemu hii ya barabara ni kampuni ya *Sinohydro Corporation Ltd.* Kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa gharama ya shilingi bilioni 40.61. Awamu ya tatu inahusu ujenzi wa sehemu

za barabara za kutoka Mayamaya – Mela yenye urefu wa kilometa 99. 35 na sehemu ya Mela – Bonga yenye urefu wa kilometa 88.80. Tathmini ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa sehemu hizi za barabara *(Tender Evaluation)* imeshaanza.

(b) Mheshimiwa Spika, chini ya Mikataba iliyokwishasainiwa, utekelezaji wa ujenzi kwa kiwango cha lami ni kama ifuatavyo: Babati – Bonga na Bicha – Kondoa umekamilika kuanzia tarehe 31 Machi, 2013; Dodoma – Mayamaya ujenzi umepangwa kukamilika terehe 10 Septemba, 2013. Tarehe za kukamilika kwa ujenzi wa sehemu za Mayamaya – Mela na Mela – Bonga zitafahamika baada ya kutiwa saini kwa mikataba ya ujenzi wa sehemu hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi wa Ujenzi wa Barabara hii ya Dodoma – Babati kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ni shilingi bilioni 36.88.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika Bunge la Bajeti mwaka jana, Waziri wa Ujenzi aliahidi kwamba, Benki ya Maendeleo Afrika *(ADB)* tayari imekubaliana na Serikali ya Tanzania kutoa mkopo wa shilingi bilioni 240 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya kutoka Mayamaya – Mela – Bonga. Ningeomba nipate ufafanuzi ama nipate uhakika wa yafuatayo:-

(i) Je, *ADB* imeshatoa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii?

(ii) Fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 30 tu kwa mwaka huu wa fedha; ni kiasi kidogo sana cha fedha; Je, hii fedha ni kwa ajili ya kuwalipa fidia Wananchi walioko pembeni mwa barabara, ambao wanastahili kulipwa fidia ama ya kuendeleza ujenzi upi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Nkamia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimhakikishie kwamba fedha za kujenga barabara hii zimeshatolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Maeneo haya ambayo tumeyataja kwamba tutaanza ujenzi, siyo lazima fedha zote za kumaliza kilometa 180 zitolewe kwa mwaka mmoja. Mradi huu tunategemea tutaujenga kati ya miaka miwili au miaka miwili na nusu. Fedha tutakuwa tunazitoa kulingana na matumizi ambayo yanahitajika. Fedha hizi ambazo tumeziweka kwenye bajeti, zitaweza kutumika pia katika kuwalipa watu wanaostahili kulipa fidia kwa mujibu wa Sheria ya Barabara.

**SPIKA**: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, si muda mnauona; muda umekwisha, nina matangazo yafuatayo kwa ajili ya kazi:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.15 mchana, watakuwa na kikao chao Chumba Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Chumba Namba 219.

Katibu wa Wabunge kutoka Majimbo yanayolima pamba Tanzania, Dkt. Titus Kamani, anaomba niwatangazie Wabunge wote wanaotoka Majimbo yanayolima pamba kuwa, kutakuwa na Kikao Dodoma Hoteli, saa 7.30 mchana.

Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mwenyekiti wa *APNAC*, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati Tendaji, leo watakuwa na kikao saa 7.00 mchana kwenye Ukumbi Mkubwa wa Msekwa.

Wakati wa maswali ni *fixed time*, mwongozo haurusiwi kabisa, ukiingiza mwongozo unaenda nje ya ratiba. Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kifungu Namba 68(7) cha Kanuni za Bunge ambacho kinasema: "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba *"Mwongozo wa Spika"* kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika, yatatolewa hapo kwa hapo au baadaye, kadiri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ambazo zinalisimamia Bunge letu, jana wakati Bunge letu likiwa katika kipindi chake cha jioni, Waheshimiwa Wabunge watano wa Chama cha CHADEMA, walitolewa kwa maelekezo ya Mheshimiwa Naibu Spika. Wabunge waliotolewa ni pamoja na Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

Wabunge hawa walipotolewa, walipewa vilevile adhabu ya kutokuhudhuria vikao vitano vya Bunge, iliyotolewa papo kwa hapo na Mheshimiwa Naibu spika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni inayompa Naibu Spika au Spika, mamlaka ya kumtoa Mbunge kwa siku tano ni Kanuni ya 73(3), ambayo inahusu Mbunge ambaye atashindwa kutoa vielelezo vya aidha, kusema uongo, ambayo inasema hivi naomba niisome:-

"Endapo Mbunge yeyote atatakiwa kuthibitisha ukweli wa maneno aliyoyasema na hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa, amekataa au ameshindwa kutoa uthibitisho huo, Spika anaweza kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie Vikao vya Bunge visivyozidi vitano."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya yale yaliyotokea jana Bungeni, kulitokea sintofahamu kati ya Wabunge na Kiti cha Mheshimiwa Spika, ambapo katika mambo ya msingi

tulitegemea Kifungu Namba 74(1) cha Kanuni zetu za Bunge kingetumika, ambacho kinasema hivi:-

"Spika anaweza kutaja jina la Mbunge kwamba amedharau Mamlaka ya Spika na kisha kupeleka jina hilo kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikiwa:-

(a) Kwa maneno au vitendo, Mbunge huyo ameonesha dharau kwa mamlaka ya Spika; au

(b) Mbunge huyu atafanya kitendo chochote cha makusudi cha kudharau shughuli ya Bunge au Mbunge yeyote anayeongoza shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, Wabunge wale wametolewa kwa Kanuni gani na lini wataweza kurejeshewa haki yao ya kurudi ndani ya Bunge?

**SPIKA**: Ahsante. Maneno kama haya yangeanza wakati wa maswali, si unachukua muda wote! Kanuni hizo hizo zinasema; Spika, atatoa majibu wakati huo huo au wakati mwingine unaofaa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA**: Nilimwona kwanza Mheshimiwa Halima Mdee, aliwahi kuniambia nikamwachia. Hatuwezi kuendelea na mwongozo zaidi ya mmoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, msingi wangu wa kuomba mwongozo wako uko katika msingi ule ule wa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

**SPIKA**: Basi tena huwezi kurudia inatosha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Naomba nimalizie.

**SPIKA**: Inatosha. Kuunga mkono mwongozo nimesema nitatolea kauli baadaye, sasa kama nitatolea kauli

baadaye, wewe utauliza nyongeza kuhusu nini? Mimi nitatoa baadaye na wewe utaniuliza baadaye tena. Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nami naomba mwongozo wako kwa mambo ambayo yametokea katika Bunge la jana, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Jana kuna Mheshimiwa ambaye aliambiwa athibitishe kuhusiana na suala la udini kwa Mheshimiwa Rais. Vilevile Taarifa ya Kambi ya Upinzani, ilimhusisha Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba, anajihusisha na kitendo cha kijasusi.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni tuhuma nzito ambayo inahitaji nayo kuthibitishwa, kwa sababu tunajua Wizara hiyo inahusika na Ulinzi wa Nchi yetu. Sasa inaleta taswira mbaya kwa raia kuona Waziri husika anahusishwa na kitu ambacho hakiko wazi, ushahidi haujaletwa katika Bunge lako Tukufu. Naomba mwongozo wako katika hili, kwa Kanuni zilezile ambazo zilikuwa zinataka Mbunge yule alete uthibitisho, nadhani zilikuwa zinahitaji pia aliyesoma Taarifa hii kuleta uthibitisho wa Waziri huyo kujihusisha na vitendo hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA**: Kwanza kabisa, naomba wote mkae. Mheshimiwa Ester Bulaya, sehemu ya kwanza, Mheshimiwa aliyetoa kauli amepewa muda wa siku saba alete uthibitisho. Sehemu ya pili, wanaohusika hawajajibu hoja watajibu hoja.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, waandishi walioandika Kanuni ya 68(7), waliposema kwamba, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, hawakuwa na maana ya jambo lililotokea jana, walikuwa na maana ya jambo lililotokea katika Kikao hicho mapema. Unaweza kutikisa kichwa, unaweza kufanya chochote, lakini Kanuni hizi kwa tafsiri siyo jambo lililotokea jana, wangesema kwamba jambo lililotokea katika kikao kilichopita.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, unajua hakuna kitu kinachowa-*bore* Wananchi kama kushindana na Kanuni zetu, sasa andikeni maoni ya Kanuni na mlete kwenye Kamati ya Kanuni, mnawa-*bore* Wananchi. Jana siku nzima, hakuna kazi iliyofanyika. Naomba tufikirie hilo, kama *seriously* una swali, nimesema la Mheshimiwa Mbowe nitamjibu wakati mwafaka kwani Kanuni zinaruhusu. Sasa tukianza taarifa, taarifa, mimi siwezi kukubali.

Katibu, tunaendelea na hatua inayofuata.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serkali kwa Mwaka 2013/2014**
**Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma),**
**(Utawala Bora) na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu)**

*(Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA**: Jana wakati zahama zilipoanza kutokea, alikuwa anazungumza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, naomba uzungumze na sitegemei kuleta zahama tena. Sitegemei dhahama kweli, jadili yaliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nianze kwa kuongelea Mfuko wa *TASAF.* Niliwahi kuongea na Waziri husika na nikaweza kuongea na Ofisi ya *TASAF* Wilayani kwangu. Waliahidi watakamilisha Barabara ya Kengege kwenda Makunda, Barabara ya Ruzirukulu kwenda Ndago, Barabara ya Nsusu kwenda Mengela, ambapo Wananchi wangu wanapata shida sana. Vilevile walisema watashughulikia maji Kisharita pamoja na maeneo mengine ambayo yana shida kubwa sana.

Mheshimiwa Waziri unayehusika, naomba ulipe uzito unaostahili jambo hili, Wananchi wangu wale wanapata shida sana.

Mheshimiwa Spika, kikwetu, jirani yako akipata shida unaitoa na mifugo yake ukaichunge. Ukienda Jimbo jirani la

Igunga, kuna barabara katika Kijiji cha Mwabaraturu, jirani kabisa na Kata ya Itunduru katika Wilaya ya Igunga, Jimbo la Igunga, ilijengwa kwa Mfuko wa Fedha za *TASAF,* lakini Wananchi wanalalamika barabara ile iko chini ya kiwango na madaraja yale yalijengwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Waziri ukipata fursa zungukia ujionee mwenyewe na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Pia kuna maeneo ya pembezoni mwa Kata za Wilaya ya Igunga, kama Kata ya Isakamaliwa, iko pembeni sana, pamoja na kazi nzuri ya Serikali ya kukamilisha Daraja la Mbutu, bado mvua ikinyesha Wananchi wa Kata ile hawataweza kutumia Daraja lile. Naomba na kule Mfuko wako ambao unajali vipaumbele vya wanakijiji, uweze kulifanyia kazi eneo hilo.

Jambo lingine, niseme kwa maslahi ya Tanzania. Lilisemwa sana jana suala la Katiba na likaelezewa kwa kutumia mfano mmoja kwamba, *Ward C* zile ndizo zilizobana Wananchi kwa sababu ni za CCM. Ngojeni niwape mfano mmoja Watanzania muweze kuelewa; Halmashauri ya Karatu, kwa miaka mingi imekuwa chini ya CHADEMA na *Ward C* mpaka sasa ipo chini ya CHADEMA. Kuna Madiwani watatu tu wa CCM pale. Mwenyekiti ni wa CHADEMA, Mbunge ni CHADEMA, lakini Mabaraza ya Katiba, CCM wamepitishwa 63 na CHADEMA wamepatikana chini ya 20. Kwa hiyo, utaona kwamba, hiki kinachotaka kujengwa ni kwamba Mabaraza yamewabana baadhi ya wagombea kutoka chama fulani, ni hisia tu. *(Makofi)*

Mimi niwaambie Watanzania, kiutaalam kabisa, katika nchi yetu, fedha tulizozipitisha hapa Bungeni kupeleka kwenye mchakato wa Katiba, tungeweza kizipeleka kununua madawati, madawa, kulipa mishahara na kuboresha visima vya maji. Leo hii zoezi limefanyika kama tulivyopitisha hapa Bungeni, watu wanajitokeza wanasema watasusia huo mchakato. Hii ni kutokuwa na uchungu na fedha za umma.

Vilevile katika hali hiyo hiyo, mimi niwaombe Watanzania, kwa sababu Mabaraza ya Katiba hayatoi *veto* kwenye suala hilo la Katiba, litakuja hapahapa, tuje tubishane

kwa hoja hapa hapa na huo ndiyo ushauri mzuri ili tuweze kufikia hatua ya mwisho.

Watanzania wenzentu mnaweza msiwajue, mimi ninaowajua hii huwa hainipi shida; wakisema hapana huwa hawamaanishi hapana, wakisema hapana kwenye bajeti tukipitisha fedha, tunaenda kugombania fedha hizo hizo kwa ajili ya matumizi. Wakisema hapana kwenye fedha zinazopita hapa, hizo hizo zinaenda kuwa ruzuku mpaka kwenye Chama wanapokea na nyingine wanakopeshana. Kwa nini huwa hawasemi hizi fedha tulizikataa kule waache kuzichukua. Hata hili ni hivyo hivyo, tuendelee na Katiba mtaona itakavyopita kwa nguvu ya Watanzania, mtashangaa wataitumia ile ile na wataisifia. Tuendelee na zoezi hili hakuna kurudi nyuma.

Nchi gani inayoitwa Tanzania ambayo hutawakuta Wana-CCM, nionyesheni? Ni nchi gani inayoitwa Tanzania kwenye majukumu yote ya hapa nchini hutawakuta Wana-CCM wanashiriki? Hesabu walizotoa hata Kiongozi anasema zaidi ya asilima 90 Vijijini ni CCM halafu Mabaraza unategemea yatoke vijijini yasiwe na Wana-CCM! Uliona wapi ng'ombe akazaa punda? Kwa hiyo, kama ni Wana-CCM zaidi ya asilimia 90, tegemea hata *product* yake watakuwa Wana-CCM.

**KUHUSU UTARATIBU**

**SPIKA**: Mheshimiwa Mwigulu, naomba usikilize taarifa, sijui taarifa au kuhusu utaratibu. Kifungu gani?

**MHE. JONH J. MNYIKA**: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1); bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa majadiliano Bungeni, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni wala la kubahatisha tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anayechangia, amedai kwamba, utaratibu wa Mabaraza kwenda kwa Wananchi kuchujwa kwenye ngazi ya Kata, huo anaouzungumza, anadai kwamba, umepitishwa hapa Bungeni. Ukweli ni kwamba, hii ni mara nyingine tena Bunge hili linaambiwa maelezo yasiyokuwa ya kweli, mara ya kwanza ilielezwa na Waziri Mkuu na sasa inaelezwa na Mheshimiwa Mbunge anayechangia.

Sheria iliyopitishwa na Bunge hapa, kwenye Muundo wa Mabaraza imetamka kwamba, Mabaraza yataundwa kwenye maeneo ya kijiografia kwa kuzingatia uwakilishi wa makundi ya kijamii. Mfumo wa kwenda kuwachuja Wananchi waliochaguliwa kwenye vijiji kwenye ngazi ya Kata, haujapitishwa na Bunge hili, umepitishwa na mwongozo uliotengenezwa na Tume bila ridhaa ya Wananchi na bila ridhaa ya wadau.

Mheshimiwa Spika, naomba afute kauli hiyo, kwa sababu ameeleza maelezo ya uwongo.

**SPIKA:** Hawezi kufuta. Wewe uliuliza mwongozo wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anahusika na mimi najiandaa kukujibu hilo. Kwa hiyo, naomba uendee Mheshimiwa Nchemba.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, wanaume wanapoongea watoto wa kiume wanasikiliza.

Mheshimiwa Spika, ninachosema...

**SPIKA:** Mheshimiwa Nchemba, futa maneno yako ya mwishoni hapo.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nafuta.

Mheshimiwa Spika, ninachosema, Watanzania tuzihurumie fedha za walipa kodi ambazo zingeweza kwenda kupeleka madawa, tukazipeleka kwenye Katiba, tuache

zimalize zoezi hili la Katiba, tuendelee kutengeneza Katiba yetu.

Jambo linguine, hata hili ambalo limekuwa likiongelewa ongelewa, jana lilitawala sana, sijui Usalama wa Taifa umeng'oa kucha, sijui umeng'oa nywele, sijui umeng'oa nini.

Pana siri nzito sana kwenye jambo hili. Nawaomba Watanzania, inawezekana tunaongelea hili suala bila Watanzania kulijua, maadamu liko kwenye eneo ambalo litaturuhusu kuongea kinagaubaga, na mimi nilishasema nitasema; Watanzania niombeeni niwe hai tu, pana jambo limejificha hapo, hakuna cha Usalama wa Taifa umemng'oa mtu, hakuna cha Polisi, kuna watu wamefanya hilo jukumu, Watanzania hawajaona tu ule mkanda.

Mheshimiwa Spika, inawezekana hata Wabunge hawajui, labda utafute fursa uwaoneshe, kila kitu kiko wazi, twendeni kule, wasiwasi wenu nini mpaka mnaleta hapa. Twendeni tukutane pale, mnabaki kurundika manamba, ooh kawasiliana na huyu, kawasiliana na huyu, sasa kama tumewasiliana na siri tukaipata; tatizo liko wapi? Subirini mwende mkaone jambo lililofanyika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Nchemba, muda wako umepita, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mimi ndiye ninayesimamia hapa, ni ya pili. Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Mariam Kisangi ajiandae.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii adimu. Awali ya yote, naomba

nichukue nafasi hii, kwanza kabisa, kuungana na Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Vilevile kwa heshima na taadhima, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutuongoza vyema katika Ofisi hii ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa kufanya *comparison* kati ya Nchi yetu na Nchi zingine. Naanza na eneo la Utawala Bora, ambalo liko chini ya Rais**.** Utawala Bora niki-*compare* na Nchi zingine, Nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imekuwa ikiheshimika na kusifiwa sana mbele ya Umoja wa Mataifa na mbele ya Nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kutembelea Nchi mbalimbali na hususan Nchi ambayo nilipata mafunzo yangu ya Sheria; kwa kweli ukilinganisha na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Utawala Bora, sisi Nchi yetu inastahili kupata pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Nchi zinapewa *sanction* na *World Bank*, hakuna misaada, lakini sisi Tanzania, *World Bank* wametuamini kwa kiasi cha kutosha, *International Monetary Fund* wametuamini kwa kiasi cha kutosha, leo hii Miradi ya *TASAF* iko Tanzania kote, kila Wilaya, kila Mkoa kuna Miradi ya *TASAF*. Hii ni kutokana na imani waliyokuwa nayo vyombo vya nje. Vyombo vya nje kuna utaratibu wa kupata taarifa mbalimbali.

Tunapopata fedha kutoka kwa *Donor* na zile za ndani, tunaambiwa tupeleke takwimu na kadhalika. Sasa zipo Nchi zinawekewa *sanction*, hata misaada hawaipati, lakini sisi kutokana na uaminifu na *transparence* ambayo ipo, leo hii Miradi ya *TASAF* inajenga shule, Kamati yetu imeshuhudia shule zimejengwa kupitia Miradi ya *TASAF* maeneo mbalimbali, lakini pia tuna Mradi kama MKURABITA, hii yote inafadhiliwa na Umoja wa Mataifa.

Lazima tuwe watu wa shukrani, lakini sijawahi kuona Nchi ambayo haina *crime* asilimia 100, ndiyo maana nimesema leo nachangia kwa kufanya *comparison*, hata

Nchi kama Marekani, wanayo *crime*. Hakuna Nchi ambayo hakuna *crime*, yaani hiyo Nchi ni Paradiso, *Paradise*. *(Makofi)*

Tunavyo Vyombo kama Mahakama na *PCCB*, vinapaswa kuwa pale na Nchi ambayo haina vyombo hivyo hakuna Utawala Bora, *no Good Governance.* Hivi vyombo vipo kusaidia kuleta amani ambayo inastahili kuwepo. Vilevile kwa upande wa amani, kuna Nchi zingine tena nyingi zinazotuzunguka, tumekuwa tukisaidia kutafuta amani kwenye Nchi hiyo. Tanzania imekuwa ikisifiwa kwa kusaidia Nchi za jirani, kwanza, kupigania wakati wa Uhuru, lakini si hivyo tu, hata leo kuna Nchi zinazidiwa, Tanzania imekuwa ni msuluhishi katika hizo Nchi. (*Makofi*)

Tumeshuhudia Mataifa ya jirani kwenye chaguzi wanagombana, hakuna uwazi, Tanzania tumepeleka Majeshi kuwasaidia, imekuwa mfano bora. Kwa hiyo, ifike wakati tuwe watu wenye moyo wa shukrani. Changamoto siyo kwamba hazipo na hakuna Nchi ambayo haina changamoto, Marekani kwenyewe kuna changamoto. *The Big Eight;* Urusi, Ufaransa, zile Nchi ambazo ziko kwenye *Security Council,* nao wanazo changamoto. Kuna Mahakama, kuna *Murder*, hata kwetu kuna changamoto kama hizo ndiyo maana tuna Mahakama, tuna Poilsi, lakini hivi vyombo viko *accessible*. Juzi nilikuwa na *Chief Justice,* tumeona Nchi mbalimbali, lakini pia Tanzania Mahakama zetu ziko *accessible*, mtu akitaka kufungua kesi leo anaweza akaenda Mahakamani, haki ya Rufaa iko pale pale.

Sasa leo tukianza kusema kwamba, haya ni maeneo ambayo hayafanyi kazi vizuri, tutakuwa hatujitendei haki wenyewe, lakini pia hata Mataifa mengine yatatushangaa. (*Makofi*)

Idara ya Usalama, kwa heshima na taadhima, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Nchi hii isingekuwa na Usalama tusingempata, juzi amekuja Waziri Mkuu wa Denmark, ameondoka anaingia

Waziri wa China na wale ni watu wa *Intelligence* na *Security.* Sasa jamani usalama gani tunaoutaka?

Kazi tunayo; watu wanasema usalama haufanyi kazi! Jamani, matatizo ya kwenye familia, yanabaki ya kifamilia, lakini kama Nchi, tunatakiwa tu-*salute. (Makofi)*

Mataifa haya hawapeleki Viongozi wao ovyoovyo katika Nchi, wanatuma *advance cut delegation* inakwenda inaangalia ni namna gani hiyo Nchi ina ulinzi na usalama na kadhalika, ndiyo wanakwenda kupeleka Viongozi wao. *(Makofi)*

George Bush amekuja zaidi ya mara moja, Bill Clinton amekuja; sasa jamani Mungu atupe nini? Hata wakati wa kuchangia tuwe na hofu ya Mungu, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, ninayesimamia Ofisi ya Rais, Utumishi, Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kweli ninaipongeza Serikali ambayo iko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa rai, Nchi yetu mwaka 1992 tumeruhusu Vyama Vingi. Wananchi walipoulizwa walitaka Chama Kimoja asilimia 80, asilimia 20 walisema Vyama Vingi, lakini kwa heshima na hekima za Baba wa Taifa, Mwl. Nyerere, akasema hata wachache awape fursa. Na ile hata wachache tunaishuhudia leo, kwamba, wanaotaka Vyama Vingi bado ni wachache. *(Makofi)*

Ndiyo maana kwenye Mabaraza ya Kata na maeneo mengine, asilimia 80 ni Chama kinachotawala, humu Bungeni asilimia 80, tukienda kwa Wananchi asilimia 80, tumekwenda kuomba ridhaa kwa Wananchi wametupa fursa ya kukamata dola, sasa tusubiriane 2015 watupe ridhaa ndiyo utaratibu. Hatuna *Independent Candidates,* lakini tukitaka *Independent Candidates,* Katiba inakuja tuna haki ya kutoa maoni.

Mheshimiwa Spika, Vyama vingine; tunavyo Vyama 18 vilivyosajiliwa, nampongeza Msajili, anafanya kazi yake

vizuri, lakini pia Tume ya Uchaguzi ambayo inafanya kazi vizuri. *(Makofi*)

**SPIKA:** Wanakwambia 20.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, sawa, nashukuru viwili vimeongezeka, ahsante napokea taarifa.

Mheshimiwa Spika, neno kuitana Vyama vya Upinzani, *it carries a sprit* ya Upinzani; hebu tubadilishe lile jina *Opposition Party*, tutafute neno lingine, kwa sababu, mtoto ukimwita shida atapata shida, ukimwita tabu atapata tabu! *(Makofi)*

Mambo ya kuitana *Opposition*, Chama cha Upinzani, *automatically* ana-*carry the spirit* ya kupinga, *whether* mnafanya vizuri, hamfanyi vizuri. Ninaomba sana, kama Mwanasheria, nimefanya *research*, tutafute neno zuri zaidi, tusiitane vyama pinga wala *opposition*, kwa sababu *you will always oppose, that will be your motto, that will be your vision. (Makofi)*

Tuone ni namna gani Nchi yetu tunaiendeleza kwa pamoja, tumekubaliana vyama mbalimbali vya upinzani, sisi sote tunajenga nyumba moja kwa nini tugombee fito? (*Makofi*)

Kuna watu leo wanahubiri maandamano, tutamwaga damu, *how dear you are?* Yaani tumwogope Mungu, dhambi, tunahubiri watu kuuwana! Kuna Nchi wanatafuta amani, kuna Nchi wanahangaika wanatafuta msuluhishi wa Umoja wa Kimataifa, leo hii amani yetu watu wanaichezea, wanasema kitaeleweka, tutamwaga damu, yaani wewe kumwaga damu huogopi? (*Makofi*)

Unataka umwage damu ya nani? Tutaandamana, tutapinga, kweli ni maneno haya! Baba wa Taifa ametuachia urithi mzuri, Nchi amesema haina ukabila, haina udini, tupendane, masuala ya Ujamaa, leo hii Watanzania

tunavunja vunja bila hofu kabisa! Hivi kizazi kinachokuja tutawaambia nini? (*Makofi*)

Naipongeza tena Ofisi ya Rais, wanafanya kazi usiku na mchana hawalali, mipaka yetu inalindwa kwa ajili ya amani. Mikutano tumeshuhudia ya *SADC* inafanyika hapa, Mikutano ya *Commonwealth Parliamentary* inafanyika hapa, mbona hatuoni Nchi za jirani wanakwenda kufanya hiyo mikutano, kwa sababu wakifanya *advance cut* ikienda wanasema kule ni *risk*, lazima uende na *insurance; health insurance, life ansurance,* sisi Watanzania leo Mikutano ya Kimataifa inafanyika, Mawaziri na Marais wa Nchi mbalimbali wanapishana *airport*, leo tumempokea wa China, kesho wa Denmark, keshokutwa wa India.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilimwita Mariam Kisangi, atafuatiwa na Richard Ndassa; hawapo. Mheshimiwa Omar Nundu naye hayupo. Mheshimiwa Amina Makilagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo katika sekta hii muhimu sana ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niungane na Wabunge wenzangu na ninaomba niungane na Watanzania wote na hasa Wanawake, kuwalaani wale wote walioanza kuchochea masuala ya udini, ukabila, rangi na masuala mengine yoyote yale katika Nchi yetu.

Ninasema hivyo kwa sababu mahala popote panapotokea machafuko hasa ya kidini, ya kikabila au ya namna yoyote ile, wanaoumia ni Wanawake na Watoto. (*Makofi*)

Nchi yetu ya Tanzania imejengwa kwa misingi ya amani na utulivu. Kwa muda mrefu tumekuwa na amani na utulivu. Ninaomba niungane na Watanzania wote na ninaomba Wanawake wote mniunge mkono, tuwalaani wote wanaosema kwamba, eti, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye Mwasisi wa Udini. Ninaomba tuungane kulaani na tukatae kwa sababu Wanaume wote hata walioko humu ndani, pakitokea machafuko yoyote hapa katika Nchi yetu, wakatokea huu mlango wa Bunge, wakatokea Rwanda, wakatokea Msumbiji, wakifika kule wataoa tena watoto wadogo wa darasa la saba. (*Makofi*)

Wakifika kule hawatakumbuka kwamba waliacha watoto na wake na hata wake watakaowaoa huko, watawaambia hatujawahi kuoa maana tulikuwa bado shule, hata hawa wazee mnaowaona humu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu ninao ushahidi, wenzetu wa Nchi za Rwanda na Mataifa mengine, walifanya mzaha mzaha kama mnaouona. Nimekwenda Rwanda, nimeshuhudia makaburi ya Wazee, Wanawake na Watoto wasio na hatia, lakini wale walioanzisha chokochoko, wamekimbilia Nchi za mbali. Hapa Tanzania naomba nitoe wito, kuwaambia Wanawake wa Tanzania wote na Wananchi wote wapenda amani na hasa Vijana, tuepukane na uchochezi wa aina yoyote. Kuna baadhi ya watu wanasema damu itamwagika, kuna baadhi wanasema tufanye maandamano na tuko tayari mpaka kieleweke, lakini huyo anayesema tufanye maandano, wala hamtangulizi mke wake mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Naanza kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi na ninaomba nisirudie aliyoyazungumza Mheshimiwa Pindi Chana, maana nitaharibu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais na Serikali yetu Tukufu, wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana. Amani tunayoiona hapa, wasione watu vinaelea, ni Tanzania pekee

ambayo mtu anaweza akasimama akamtukana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na akaendelea kuishi nje na akiwa huru na salama. (*Makofi*)

Nchi zingine, hata kujaribu tu kusema, tayari umeshawekwa chini ya ulinzi na unafungiwa huko maisha. Kwa hiyo, naomba nipongeze sana Usalama wa Taifa, kwa jinsi wanavyotulinda, Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama na hata na Jeshi la Polisi, kwa kutoa uhuru ambao tunauona na baadhi ya wanasiasa sasa, wanaanza kuchezea shilingi katika tundu la choo. Naomba wote tuungane kuwalaani na tukatae, kwa sababu pakitokea machafuko ya aina yoyote...

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja asilimia 100 kwa 100. Hotuba hii imeeleza mambo mazuri ya msingi na kilichonifurahisha zaidi katika ukurasa wa 82 na 83, unazungumzia jinsi Serikali ilivyoleta mpango wa kuajiri Watumishi na Wataalam wa Nchi yetu.

Nimefurahishwa sana kwamba, katika mwaka huu wa fedha, Serikali itaajiri Wataalam ambao tumewasomesha kwa fedha nyingi, wasiopungua karibu 61,000. Naomba nipongeze utaratibu huu, sasa tunakwenda kupata Walimu wa kutosha, Madaktari wa kutosha, Wauguzi, Maafisa Ugani, Maafisa Mifugo na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, tujitahidi sasa kuhakikisha, hawa Watendaji ambao tumepanga kuwaajiri mwaka huu, waajiriwe kama ilivyokusudiwa, kwa sababu kero ya Wataalam ni kubwa na Watanzania walio wengi sasa wamesoma, tuna vijana wenye ujuzi, Wanawake ni asilimia 50 na ninaomba mtakapoajiri, msisahau akina mama, kwa sababu kwanza ni waaminifu na ni wachapa kazi kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na kitabu hiki, kimezungumzia suala la kuongeza mishahara ya Wafanyakazi. Naomba niipongeze sana Serikali yetu, kwa

kutambua umuhimu wa kuongeza mishahara ya Wafanyakazi wetu katika Nchi yetu, ambao wamekuwa wanafanya kazi kubwa sana katika mazingira magumu sana.

Nimefurahishwa sana na mpango huo, ombi langu; ninaomba Serikali, hizi fedha zote zilizopangwa, badala ya kupelekwa kwa hawa wakubwa, tukiwemo na sisi Wabunge, maana ukiona hata watu wanajisahau ni kulewa! Mmenipata, mtu anatoka *from nowhere*, alikuwa mtaani, anaingia hapa anajikuta ana milioni tano, analewa fedha mpaka anaanza kutukana kila mtu mpaka anamtukana Rais. Hizi fedha sasa zipelekwe kwa walala hoi. Wafanyakazi wa chini, wauguzi, manesi kule, walimu, wafanya kazi wa kawaida, madereva, askari wetu, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wanalinda amani mpaka wanawalinda na hao viongozi wanaotukana, lakini mishahara yao bado ni midogo sana. Tuelekeze fedha katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na suala la kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu katika mpango wetu huu na mmekuwa mkifanya hivyo; naomba utaratibu huu uendelee. Nimefurahishwa pia na mpango huu wa Serikali, sasa mnataka hata muwajengee na kituo, wakiwemo na Wajane.

Hivi Karibuni nilikuwa Musoma, nilikutana na Mama Maria Nyerere, unamwona ana afya nzuri, anazungumza vizuri, lengo letu waendelee kuwepo ili waendelee kutushauri na tuendelee kuchota busara zao. (*Makofi*)

Ombi langu sasa, tuendelee kuwaboreshea miundombinu. Kule kwa Mama Sokoine, tuangalie changamoto zinazomkabili, pale kwa Mama Maria Nyerere, tuangalie changamoto zinazomkabili; nilikuwa nazungumza naye, anafurahishwa sana na Serikali jinsi inavyomjali, lakini akanituma nizungumzie masuala ya maji Butiama. Nafikiri Waziri wa Maji nilishazungumza naye, naiomba Ofisi yetu iendelee kuboresha maisha ya kule ili mambo yaende sawasawa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la usalama kazini. Wafanyakazi wetu katika maeneo mengi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA**: Ahsante naona kengele ya pili.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, mtu anayesema hakuna kitu chochote ambacho Serikali imefanya anakuwa amekosea kidogo kwa sababu ni dhahiri kabisa kwamba, Serikali yetu inafanya mambo mengi katika Majimbo na katika Taifa letu. Kwa hiyo, kusema Serikali haijafanya chochote siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mbunge kusimama na kukosoa siyo kosa na siyo tatizo. Mimi nimekuwepo katika suala zima la kukosoa Bajeti za Serikali zinapoletwa na kinacholeta tatizo kubwa ni pale tunapofikia kwamba hata mambo ambayo tunakubaliana humu Bungeni, ambayo Serikali imekuwa ikiyaeleza hapa Bungeni, hayafuatwi na hayatekelezwi. Mimi leo ni Mbunge wa miaka minane, yapo mambo ambayo tangu miaka minane ya kuwepo kwangu hapa Bungeni yamekuwa yakielezwa na Serikali kwamba hili mwaka ujao wa fedha tutalifanya hivi na hili mwaka ujao wa fedha tutalifanya vile lakini mpaka leo hayajafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo mengi na kasoro nyingi katika utendaji ambazo leo ndiyo tumezizungumzia na upungufu wa utawala bora. Tuna tatizo la watumishi kuhusu suala zima la mishahara, tumezungumza hapa kuhusu mishahara ya Watumishi wa Umma, tumezungumza kuhusu

mishahara ya sekta binafsi. Mishahara ya watu hawa ni midogo mno na kwamba wanashindwa kulitumikia Taifa lao kikamilifu kwa sababu maslahi hayakidhi.

Mheshimiwa Waziri alitueleza hapa kwamba, upo mkakati ulioandaliwa na Serikali wa kuhakikisha kwamba, Watumishi wa Umma wanakadiriwa maslahi yao inavyopasa. Jitihada hizi hazitawezekana, hatutaweza kuwalipa wafanyakazi wetu stahili zinazotakiwa kama Serikali itaendelea kuendekeza matumizi ya kawaida, kama itaendelea na huu wigo mdogo wa ukusanyaji wa kodi na kama itaendelea kuwa na mfumo huu wa ukusanyaji wa kodi ambao ni dhaifu, kwa sababu mapato yetu kwa vyovyote vile hayataweza kupata fedha ya ziada ya kuwalipa wafanyakazi.

Tunazungumzia nafasi za kukaimiwa; nafasi nyingi zimekaimiwa katika Idara mbalimbali na Waziri wa TAMISEMI alilieleza Bunge siku ile kwamba, ninyi mkishaanzisha mchakato tu tayari sisi tunawaidhinishia Wakuu wa Idara na wanaendelea na kazi. Ukweli siyo hivyo, sisi katika Wilaya ya Meatu tumeshaleta maombi ya kuidhinishiwa Wakuu wa Idara zaidi ya watatu na leo ni zaidi ya miezi minane hawajaidhinishwa kazini, tunaendelea kuwa na Makaimu. Siyo Meatu tu, zipo Wilaya nyingi tu zina Makaimu. Suala hili limelalamikiwa na Bodi za Taasisi mbalimbali za Serikali hazina Wajumbe wa Bodi, Bodi haijateuliwa, Mwenyekiti hajateuliwa zina Makaimu. Mheshimiwa *CAG* amelilalamikia suala hili, ni udhaifu mkubwa katika uendeshaji wa Serikali. Sasa ukimwuliza mwidhinishaji wa mtu kumfanya kuwa Mkuu wa Idara ni wewe, mziba pengo ni wewe, ngonjera mwaka mzima halafu ukikosolewa unasema wakosoaji ni wabaya. Mambo kama haya yanaweza kurekebishwa tu kwa nini tunapigizana kelele kwa kitu kilekile?

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora tunalolihubiri, linatushinda kwa kiwango kikubwa na linapotushinda ndiyo sasa tunashindwa kuwahudumia Watanzania kwa kadiri ambayo wanahitaji kuhudumiwa.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya kwenda mwendo wa kinyonga wakati unaweza kupaa, nimesema Serikali yetu inafanya mambo mengi, ndiyo, lakini mwendo ni wa kinyonga; kwa nini twende mwendo wa kinyonga wakati tunaweza kupaa?

Mheshimiwa Spika, yapo mapato mengi ambayo yangeweza kukusanywa yakawasaidia Watanzania; ukienda Madini shilingi bilioni 525 zipo pale. Tume ya *TMAA* ilishagundua kwamba Makampuni ya Madini hayalipi kodi na wanatapeli kwa ajili ya kuweka matumizi yasiyoruhusiwa, wanapunja kodi ya Serikali, ukaguzi ulishafanyika na zikabainika shilingi bilioni 525 lakini mpaka leo *TRA* hawajaenda kukusanya. Huo ni utawala bora wa aina gani? Makampuni ya Simu tafiti zinasema kila mwaka wanapunja shilingi bilioni 600 katika ulipaji wa kodi. Wanakwepa kulipa kodi shilingi bilioni 600 kila mwaka. Huo ni utawala bora wa aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi, tulikubaliana kwenye mipango ya maendeleo kwamba, ifikapo mwaka 2015 lazima tuwe tumepunguza misamaha ya kodi kutoka tulipo hivi sasa mpaka asilimia moja ya *GDP*. Mpaka sasa kwa hesabu za *CAG* zilizotolewa za mwaka 2011/2012, misamaha ya kodi imepanda mpaka asilimia 4.3. Mawaziri wamehubiri hapa, chukua Hotuba za Mawaziri za kutoka mwaka 2005 mpaka leo, wametuhutubia hapa kwamba, Serikali inafanya jitihada ya kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja.

Mpango wa Maendeleo tumekubaliana, lakini badala ya kupunguza tunaongeza kila siku; kama siyo Serikali kulidharau Bunge hili ni nini? Kitu tulichokubaliana kwenye mpango halafu bado kinaongezwa kila mwaka, imebaki kuwa ni Wimbo wa Taifa kila mwaka. Sasa tukikosoa tunakuwa wabaya, Mpina ukikataa bajeti unakuwa mbaya! Tutaendelea kuzikataa Bajeti za Serikali kama hatuwezi kuzingatia makubaliano tunayokubaliana. Haya maneno siyo Mpina aliyekaa akayaandika, tumekubaliana kwenye mpango unasema na upo wazi, lakini leo ukikosoa ukisema

bajeti hii ni mbaya wewe ni mbaya, yale tunayokubaliana kwa nini Serikali haitaki kuyafuata?

Mheshimiwa Spika, utoroshaji wa fedha nje ya nchi ni tatizo kubwa katika Taifa. Tunazungumzia matrilioni ya fedha, lakini Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haikugusia kabisa, Hotuba ya Utawala Bora haijasema kabisa, mpaka siku ile nimekabidhi mabuku pale kwako, zaidi ya vitabu sita vya tafiti mbalimbali vya watafiti wa kimataifa wakionesha kila mwaka Tanzania inapoteza shilingi ngapi. Shilingi trilioni 13 ambazo zimepotea mpaka hivi sasa, nilikabidhi vitabu pale, lakini Hotuba ya Waziri Mkuu haijasema wala Waziri wa Utawala Bora naye hajasema. Pesa hizo ni nyingi sana kwa Watanzania lakini hajasema. Sasa kama hayo mafisadi ya nchi hii yana nguvu kuliko Serikali yenyewe inakuwaje?

Mimi najiuliza; kama Serikali yenyewe inashindwa hata kutamka, akina Mpina tunapata wapi ujasiri wa kutamka? Nadhani unatoka kwa Mungu na hii vita ipo siku tutaimaliza.

Mheshimiwa Spika, tumesema mambo makubwa na matumizi ya Serikali yanaendelea, mgawo wa raslimali za fedha tumeshuhudia hapa, Bajeti ya Waziri Mkuu inagawa shilingi bilioni 640 kwenda Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, shilingi bilioni 640 katika bajeti trilioni 16.7, tumepeleka fedha za maendeleo kwa Wananchi, shilingi bilioni 640 kwa sababu zile sasa ndiyo hasa zinazokwenda kujenga madarasa, shule, zahanati na kila kitu, *just* bilioni 640 katika bajeti hiyo kubwa. Kwa hiyo, unaweza ukaona udhaifu wetu mkubwa katika ku-*allocate resources* zetu. Wabunge hapa, kila mmoja anasimama anasema naunga mkono asilimia mia moja, lakini wana magofu ya kutoka mwaka 2010 wameyajenga na wametoa michango mikubwa, Serikali inakosa fedha ya kwenda kuyajenga majengo yale, kuna zahanati nyingi.

Mheshimiwa Spika, madhaifu kama hayo ya ugawaji wa rasilimali utaunga mkono lini Bajeti ya Serikali kwa sababu hata ushauri tunaoutoa hausikilizwi?

Mheshimiwa Spika, nilikueleza Bunge lililopita kuhusu udhaifu wa utoaji wa huduma kwa Wananchi, hospitali zetu zinalalamikiwa na Watanzania wote, Watanzania wanaamua kuacha kwenda kutibiwa Muhimbili wanakwenda kwenye *dispensary*. Hospitali zetu za mikoa zina madhaifu makubwa, hata vifaa tunavyojitahidi kununua kwa pesa kubwa, vinahujumiwa havifanyi kazi ya kuwasaidia Watanzania na gharama ya Watanzania kwenda kulipia vifaa hivyo au kwenda kupima vipimo hawana uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uliahidi kwamba, utaunda na Tume ichunguze suala hilo, japo mimi hata taarifa hizo mpaka hivi sasa sina, lakini Watanzania wengi wanakufa bila matibabu na wakati huo huo Serikali yao ikijitahidi kwa namna nyingine kununua vifaa na kuleta madawa ili Watanzania watibiwe. Tatizo lililopo katika mfumo wetu wa matibabu ni nini? Matatizo haya hayashughulikiwi, ninyi mnapanga bajeti, tunashindana mpaka unakuja na bajeti nyingine unasimuliwa *story* ileile.

Mheshimiwa Spika, tunafanya haya, tunafanya udhaifu huu wote wa kukusanya kodi zetu, tunafanya mzaha huu na misamaha ya kodi, nasema hata Waziri wa Uwekezaji namwambia siyo mibaya lakini inapotumika vibaya ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Munde Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Ally Omar.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda niishukuru sana ofisi yako, pamoja na wewe mwenyewe na pia nawashukuru Wabunge wenzangu wote pamoja na Serikali, kwa kunifariji wakati wa msiba wa mama yangu; nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kuanza kuwaambia Watanzania wenzangu kwamba, tupuuze kabisa *propaganda* na uzushi unaozuliwa humu ndani. Humu ndani sasa kumekuwa ni sehemu ya uzushi na *propaganda* na kumekuwa ni sehemu ya watu kujizolea sifa ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba Bunge lako Tukufu sasa tuangalie upya Kanuni zetu za Bunge. Iwapo Mheshimiwa Mbunge yeyote atakuja hapa na kutamka maneno ambayo hayana ushahidi wala uhakika kwamba Usalama wa Taifa amefanya moja, mbili, tatu, atoe uthibitisho na bila uthibitisho basi apelekwe Mahakamani. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chombo hiki ni kikubwa sana na Watanzania wengi wanakiangalia na kukiamini. Mheshimiwa Mbunge anapoinuka hapa na kusema kitu cha uongo, kwa uthibitisho kabisa, wanalivunjia heshima Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, tutake tusitake ni lazima tupitie tena upya Kanuni zetu, ziwe na meno zihakikishe kwamba, Mbunge akija kusema uongo hapa achukuliwe hatua zinazostahili na si kuwatoa nje, twende mbali zaidi na kuwafikisha Mahakamani wakatoe uthibitisho. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vitu vinavyosikitisha sana kuwaambia watu wa Usalama wa Taifa wanashiriki mtu mmoja mmoja kwenda kumfanyia vitu vichafu. Sitaki hata kuvitaja vitu hivyo, kwa sababu nadhani ni uzushi mtupu. Tulishinda uchaguzi mwaka 2010, wenzetu hawa walisema hawatambui matokeo na nchi haitatawalika. Waliingia kwenye majukwaa wakasema mambo ya ajabuajabu, hao Usalama wa Taifa kwa nini wasiwafanyie hayo wakati wanasema nchi haitatawalika? Kwa nini wasiwafanyie watu hawa hayo mambo wakati wanasema hawamtambui Rais wa nchi hii?

Nashangaa leo Usalama wa Taifa waje wamfanyie mtu mmoja kwa manufaa ya Taifa zima! Sitaki kuamini hilo na ninaomba Watanzania wenzangu tusiamini hilo.

Ninachoamini ni kwamba, Usalama wa Taifa wapo, wanafanya kazi yao vizuri na ndiyo maana mpaka leo nchi hii imekuwa ikitambulika dunia nzima kuwa ni nchi ya amani na utulivu.

Nawaomba Usalama wa Taifa wasivunjike moyo, waendelee kufanya kazi zao kama wanavyofanya kila siku, waendelee kutulinda na waendelee kuwa shupavu, wasikubali *propaganda* na uzushi usiokuwa na maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala zima la udini. Katika suala hili naomba kwanza nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kikwete, kwa kulisimamia vizuri. Anajitahidi sana pale anaposikia matatizo ya udini, amekuwa akituambia zaidi ya mara mbili au tatu kwamba, tuepuke kabisa masuala haya, lakini kwa sababu kuna watu wana mambo yao binafsi katika suala hili, ndiyo maana unawasikia kila siku kuna vita kubwa ya udini, damu itamwagika tusipoangalia na kadhalika. Mimi nashangaa, baba mzima mwenye nyumba unahutubia watoto hatari kila siku, huwahutubii mambo mema. Hii ni hatari kubwa, lakini mimi nasema hakuna udini wowote na wala Rais wetu hajawa kinara wa udini.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mdogo tu, Mheshimiwa Rais wakati anateua Ma-*DC* alichukua Wabunge watano wa Viti Maalum akawafanya kuwa Ma-*DC,* kati ya Wabunge hao watano ni mmoja tu ambaye ni Mwislamu lakini wanne wote ni Wakristo. Hasa huu udini unaoongelewa mbona mimi siuelewi? Mimi nadhani hapa kuna *propaganda* zinazoendelea na sidhani kama vitu vinavyoongelewa ni vya ukweli. Mimi nawaomba ndugu zangu, waache uzushi, wafanye kazi, waje hapa waongee vitu vya msingi kwa mustakabali wa Taifa letu la Tanzania na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, niwatahadharishe tu Watanzania kwamba, vita nyingi zinatokea kwa sababu ya sisi wanasiasa kwa uroho mkubwa wa madaraka na si vinginevyo. Mimi

niwaambie tu kwamba, twendeni majukwaani tukaongee sera zetu, tuombe kura, Watanzania watatupima, lakini tusichukue mambo haya ya udini, ya kumwaga damu, kwa sababu mambo haya yakija kutokea wanasiasa wote hapa mtakimbia hakuna atakayebaki kwani wote mna *passport* zenu mtaondoka, watakaoumia ni walalahoi na Watanzania wale wa chini kabisa. Naomba sana Watanzania mliangalie hili na mlifikirie kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kuhusu Idara Kuu ya Utumishi. Kwanza, niwapongeze kwa Hotuba yao nzuri waliyoitoa, kwa kujali kabisa watumishi wao kuwaongezea mishahara na vilevile niwapongeze kwa mikakati yao mikubwa ya kuajiri na kuziba mapengo yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi bado sijaridhika na utaratibu mzima wa ajira. Utaratibu uliopo sasa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza vizuri kwamba, zile kada tulizokuwa tunazipigia kelele hapa Bungeni za madereva, wahudumu na kadhalika, wameshusha Halmashauri, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunampongeza sana. Utaratibu wa kada hizi kubwa pia siridhiki nao, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na utaratibu wa Kikanda, kuna Sekretarieti ya Ajira ipo Dar es Salaam ambayo inatakiwa watu wote wenye kada kubwa waajiriwe Dar es Salaam.

Naiomba Serikali kwamba, hiyo Sekretarieti haiwezi kutembea ikaandika matangazo yake kwamba tarehe 10 tutakuwa na *interview* Dar es Salaam, tarehe 15 tutakuwa na *interview* Kanda ya Ziwa na tarehe 20 tutakuwa na *interview* Mtwara, lakini *interview* hiyo inahusu kama ni Madaktari ni ya Madaktari tu na kama ni mchanganyiko ni mchanganyiko tu; kwa nini jamani mtu wa Mtwara amemaliza Chuo Kikuu *Engineering* yupo kijijini kwao Mtwara unamwambia *interview* tarehe 10 Dar es Salaam hana hiyo nauli ya kumfikisha Dar es Salaam si umemnyima hiyo nafasi? Mheshimiwa Waziri, mtu yuko kwetu Tabora kijijini au Urambo kwa Baba yangu Mheshimiwa Samuel Sitta, unamwambia keshokutwa kuna *interview* Dar es Salaam, hana ndugu wala

jamaa na hapafahamu vizuri, amesomea zake Mwanza huko na ku-*graduate* Mwanza inakuwa ni vigumu sana.

Naiomba Serikali yangu iangalie hali ya Watanzania hawa, wengine ni watoto wa wakulima, ni vigumu sana kupata nauli umpe mwanao ya kwenda na kurudi, umpe pesa ya kulala na kula *then* akafanye *interview* kisha arudi. Mimi nadhani bado kuna ugumu mkubwa, wakati huo labda amekosa hiyo nafasi, naomba suala hili tuliangalie sana zigawiwe Kanda. Namwomba sana dada yangu Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, atugawie kanda za kufanyia *interview,* hiyo Sekretarieti yake ambayo yeye anaiamini na Utumishi iende kwenye hizo Kanda ikawafanyie watu *interview.* Kama ni vigumu kuweka kila Kanda watumishi basi walewale wasafiri waende kwenye Kanda husika. Kwa kweli hii itaturahisishia na itawapa fursa Watanzania wote kufanya hizi *interview* vizuri ili kila mtu apate kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichopo huko maofisini makaimu ni wengi sana, kipindi kilichopita nilikuwa Kamati ya Nishati na Madini, kila taasisi itakayokuja pale kuna makaimu zaidi ya kumi au zaidi ya watano, lakini safari hii niko Kamati ya *LAAC,* hata Halmashauri unakuta kuna ikama ya *Internal Auditors* wanatakiwa kuwa wanne lakini yupo mmoja au hakuna. Ukiwauliza wanakwambia tulishapeleka barua ya maombi Idara Kuu ya Utumishi bado hawajatuletea. Wakati huohuo huko mtaani kuna watu kibao wanatafuta hizo kazi lakini hawazipati. Kwa hiyo, nadhani mtiririko au mfumo bado haujawa mzuri, tunahitaji watumishi, wasomi wapo lakini jinsi ya kuwapata kwa muda mwafaka bado haujakaa vizuri. Mimi nadhani tukisogeza kwenye Kanda tutawapata wengi sana na tutawapata kwa muda mwafaka.

Makaimu wamekuwa wengi na hata mtu kumhoji unashindwa yeye ni kaimu tu, kwa hiyo na yeye anafanya kazi ile kwa woga, hajiamini vizuri kwamba sijui hapa nitakosea au nitapatia. Kwa hiyo, sidhani kama tuna haja ya kuwa na makaimu kwa sababu Serikali yetu imetufungulia vyuo vingi, tuna Vyuo Vikuu vingi, watoto wetu wengi wanamaliza shule na nafasi zipo wazi, kwa hiyo, naomba

Serikali basi iangalie vizuri suala hili ili kila sehemu ijazwe na mtu anayestahili kuwepo mahali hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Idara ya Afya; kwa mfano, pale kwetu Tabora, Kitete Hospitali, sisi watu wa Tabora hatuna Hospitali ya Wilaya Tabora Manispaa wala Uyui hawana Hospitali ya Wilaya, watu wote tunatumia Hospitali ya Mkoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu katika muda huu.

Mheshimiwa Spika, jana nilimsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, akiwasilisha hotuba yake hapa na alimalizia kwa kusema, naomba ninukuu alisema: "Ili tuwe na uchumi bora lazima tuwe na utawala bora ambapo Sera, Sheria na Kanuni na Taratibu zitatumika."

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nianze hapo alipomalizia yeye, maana alimaliza pazuri; ni kweli ikiwa tutapata uchumi bora basi utawala bora utaimarika.

Mheshimiwa Spika, lakini tutafikia namna gani huko ikiwa nidhamu ya kazi imeshuka? Wafanyakazi au Watumishi

wa Umma hawataki kufanya kazi, wanachelewa kwenda kazini na wakifika wanapiga soga tu hawafanyi kazi, hawawajibiki, hawatoi huduma inavyopasa kwa walengwa na Serikali kama haioni, inawafumbia macho au inawalea. Je, utawala bora utapatikana au uchumi bora utakua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima iyatazame haya na iwawajibishe wazembe wa namna hiyo ili uchumi uweze kukua na utawala bora uweze kuimarika. Kama tunavyoambiwa, utawala bora ni nguzo ya kila jambo.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba, Rais Mstaafu Mheshimiwa William Mkapa, aliingia katika kinyanganyiro cha kugombea *Mo Ibrahim Award,* ambayo inapima kigezo cha utawala bora katika nchi kwa Marais Wastaafu. Zawadi ile au nishani ile ilichukuliwa na Rais Mstaafu wa Msumbiji, Mheshimiwa Chissano. Kwa kweli nilihuzunika kidogo, nchi kama Msumbiji, ambayo sisi tumeilea wakati inapata uhuru mimi nilikuwa shule, lakini nchi hiyo wakati inapata uhuru mimi sijazaliwa, leo inatushinda sisi ambao ni wazazi au wazee au baba tuliyoilea Msumbiji inakuwa ni bora kwa utawala bora kuliko sisi wazazi, inatia huzuni.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni lazima tulizingatie ili tujipange upya safu yetu ya utawala bora tuweze kwenda mbele kwa ari zaidi kama tunavyosema katika Chama kinachotawala.

Mheshimiwa Spika, haki ni nguzo ya utawala bora na haki lazima ipatikane *regardless* nani mwenye haki ile, ikiwa haki ile ni ya Mheshimiwa Waziri Celina Kombani au ni yangu mimi Haroub, Mbunge anayetoka Chonga, Jimbo lililopo shambani huko Pemba, basi lazima yule mwenye haki yake apewe, ndiyo utawala bora utakapokuwa unaonekana. Maana yake lazima utawala bora uwe unaonekana siyo unaandika kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ni chombo kinachotegemewa au kinachotazamwa kutoa haki na kinaainisha haki ile ni ya nani?

Mheshimiwa Spika, Mahakama inabidi izingatie sana katika kutoa haki ili utawala bora katika nchi uwe imara. Sitaki kusema Mahakama haitoi haki, lakini nasisitiza tu kwamba izidi kukaza kamba haki za Wananchi zipatikane ili ionekane ile sura ya utawala bora. Kama haki za watu zinachelewa sana, mtu anapofika mahakamani kwa sababu ni mnyonge, basi haki yake inachelewa kupatikana au haipatikani kabisa, inakwenda kwa yule ambaye siyo haki yake, kwa sababu ya cheo chake au uwezo wake wa kiuchumi, basi hii itatushushia ile *chart* au *graph* ya utawala bora katika nchi.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu, analipenda sana jambo hili la kupewa haki mwenye haki yake na alimwamrisha Mtume wake Daudi ambaye amempa Kitabu cha Torati, akamwambia ewe Daudi, utakapohukumu baina ya watu basi hukumu kwa uadilifu. Hapa ni kwamba, Mwenyezi Mungu, alikuwa anamfundisha Daudi utawala bora. Alimwambia hukumu kwa uadilifu, uadilifu ndiyo sehemu kubwa ya utawala bora na alimwambia atakavyohukumu baina ya watu, maana wapo Wazungu, Waafrika, Wachina, Warusi, Wamarekani, wote hao wapo katika dunia. Kwa hiyo, mtu apewe haki yake bila kutazama ni nani, ana cheo gani na ana heshima gani.

Mheshimiwa Spika, tukiyafanya hayo kwa mazingatio, basi utawala bora utaimarika na tukiyabeza basi utawala bora pia utakuwa unaporomoka.

Mheshimia Spika, nataka niingie kidogo katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri imepangiwa katika bajeti hii zaidi ya shilingi bilioni 300, ambapo Watumishi wake hawazidi 100, lakini Bunge letu la Jamhuri ya Muungano, ambao ni Mhimili mkubwa katika nchi na ni Mhimili mmoja katika Mihimili mitatu inayoshikilia Dola, imepangiwa bajeti ya shilingi bilioni 114 fedha za

matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 80 ambazo ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kwamba, Wabunge wanafanya kazi katika mazingira magumu; hawana ofisi, hawana chochote na bado fedha iliyotengwa inakuwa ni ndogo kuwawezesha Wabunge kufanya kazi kama Mhimili; na ndiyo hapo ninapojenga hoja yangu kwamba, utawala bora utakuwa haupatikani. Kwa sababu Wabunge ndiyo wanaoisimamia Serikali, kuikosoa na kuielekeza, ikiwa Bunge linapewa bajeti ndogo kama hii, tumeambiwa hapa ni ofisi 45 tu za Wabunge ndiyo zimekamilika, Wabunge tupo 350, ni chini ya asilimia 20 ambao ofisi zao zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado hapa haijaonesha nia ya dhati ya kujenga utawala bora, kwa sababu kila mtu anatakiwa apewe haki yake kwa mujibu wa nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu *TASAF*. Mfuko huu wa *TASAF* tumeambiwa upo Zanzibar na Pemba na sehemu zote za nchi yetu. Lakini ni jambo la kusikitisha, hapa liliulizwa swali kwamba Wabunge hawashirikishwi kule Zanzibar katika Mfuko huu wa *TASAF* na ni kweli sisi hatuna habari hasa. Katika Jimbo langu la Chonga, juzi nimeona katika kipindi cha karibuni hivi kuna barabara ndogo tu labda ya kilomita moja ndiyo imechongwa hata sijui ingawa ni Mbunge. Nauliza kuna habari gani hapa naambiwa *TASAF. TASAF* wanafanya kazi na mimi Mbunge sijui, nawaona watu wanakwenda na kurudi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Namwita Profesa Mwandosya.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, kwa

kunipa fursa ya kuwa hai leo ili niwasilishe mchango wangu wa mawazo kutoka katika sakafu ya moyo wangu kulingana na uelewa wangu.

Mheshimiwa Spika, tunaposema Utawala Bora, basi uwe kwa vitendo na siyo kwa maneno. Hadi leo hakuna utaratibu wa kisheria wa makabidhiano kati ya ngazi mbalimbali za utawala; kwa mfano, baada ya uchaguzi na matokeo kutoka, hakuna hata Mbunge mmoja au Diwani anayeweza kukubali kumkabidhi aliyeshinda uchaguzi na kuonesha wapi ameishia na huyu aliyechukua nafasi wapi aanzie. Kutokuwa na utaratibu huu kisheria kwa muda mrefu, siyo tu kumesababisha mahusiano mabaya, bali pia hasara kwa Taifa hasa kwenye fedha za Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo, umekuwa ukipangwa na ngazi za juu za uongozi na utawala bila kuwahusisha Wananchi. Hii imeleta mivutano mikubwa sana ya kuainisha vipaumbele, nini kianze na nini kisianze na mfano mzuri ni kiwe cha mwisho. Jana (juzi) wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akitoa majumuisho yake kwa Taifa kupitia Bunge hili, mikutano hiyo ilionekana ni mpambano kati ya Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Pinda na siyo Serikali iliyopo madarakani na KAMBI Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa, kabla ya kuainisha vipaumbele vya miaka mitano au kumi kama vilivyopangwa (vya maendeleo) ni vizuri wataalam wa Wizara wakachukua ilani za vyama vyote na kuangalia jinsi gani ya kuweka kwa uwiano kwa asilimia ili kupunguza mivutano na kuweka mahusiano. Ikumbukwe kuwa, hata ambao hawakushinda wanatozwa kodi na zinatumika kuleta maendeleo ya nchi. Kwa mfano, uchangiaji wa hoja humu Bungeni umewekwa kwa asilimia (%) na sijasikia malalamiko na kwa kuwa ndiyo makubaliano, kila kitu kinafanyika kwa utulivu. Kwa mtindo uliopo sasa, unaonekana ni kama mtindo wa maendeleo ya chama kilichopo madarakani, kama kweli tunataka mahusiano na Utawala Bora basi haya yote ni vizuri yakaratibiwa vyema.

Mheshimiwa Spika, hayo ni mawazo ya mchango wangu, kama una manufaa kwa Taifa uchukuliwe na kama hauna manufaa basi ubakizeni kwenye karatasi hii kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, bado rushwa imekuwa ikichukuliwa tu kama kitendo cha kupeana fedha taslimu au vitu lakini tumeacha kuvichukulia vitisho kama rushwa; ni vizuri ikaeleweka kuwa kutoa vitisho kwa ajili ya kupata upendeleo wa huduma pia ni rushwa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa ikaeleweka ni kosa na katika utoaji wa elimu ni vizuri hilo likawekwa wazi.

Mheshimiwa Spika, Idara ya *TISS* hii ni muhimu sana na hata enzi za Mitume, Idara za Kipelelezi zilikuwepo. Kwa kuwa Idara hii ni nyeti kwa Taifa letu na Taifa liwe salama, yawezekana kabisa na hii ni wazi kuwa Idara ni safi na malengo yake ni safi ila ikawa baadhi ya watu waliomo siyo safi. Leo Idara hii imekuwa ikihusishwa na mambo yasiyo ya kimaadili na hii imetokana na Idara kuingiliwa na walevi, wazinzi na watu wasio na maadili, ambayo imepelekea kuleta wasiwasi kwa watawaliwa na baadhi ya sisi wanasiasa na vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, huko mwanzo Idara hii ilihusika kwa karibu sana na usaili wa Watumishi wa Umma hasa Askari.

Mheshimiwa Spika, leo Jeshi la Polisi limeonekana lina utovu mkubwa wa nidhamu na maadili kwa kuwa Idara ya Usalama imeacha kabisa usaili wa Jeshi hili na Majeshi mengine, kufanya waingie watu wasio na maadili na kuleta mitafaruku na sintofahamu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Idara ya Usalama ijihusishe kwa karibu sana katika usaili wa watumishi wake ikiwemo wanaojiunga na Majeshi yetu yote ili huko mbele tusiwe na Jeshi ambalo linatiliwa mashaka na raia wake.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kuona hili linafuatiliwa na linatendeka na hii ni kwa mustakabali wa usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kuwashukuru Wataalamu wote wa Wizara hizi kabla ya mwaka wa fedha kwisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa hii nami kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumisi wa Umma) ya mwaka 2013/2014. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa bajeti yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Dunia nzima inatambua umuhimu wa watumishi kwani nchi yoyote isipokuwa na watumishi wazuri, wenye kufanya kazi kwa juhudi na waaminifu, basi itachelewa sana kupata maendeleo yake. Hapa kwetu matatizo na malalamiko ya watumishi kila siku yanazidi, matatizo hayo yanapunguza ufanisi wao makazini, zaidi kutozifuata kabisa sheria na misingi ya kazi. Malalamiko mengi ya watumishi hawa ni maslahi yamekuwa madogo, hayawatoshelezi kujikimu na maisha magumu wanayoishi, kwani gharama za maisha zimekuwa zikipanda kila siku; mfano nauli za usafirishaji zimepanda, vyakula na kadhalika. Watumishi hawa imefikia kukata tamaa kabisa na kujiingiza katika vitendo viovu vya rushwa ilimradi wajipatie fedha za ziada waweze kukabiliana na hali ngumu ya kimaisha. Nashauri Serikali iweke mkakati wa kuwaajiri watumishi na kuwapa motisha kama wafanyavyo nchi nyingine ili na hawa watumishi wetu maisha yao yabadilike na mkakati huo uanzie kuboreshwa kwa mishahara yao na marupurupu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatiz0 lingine ambalo linawakumba sana Watumishi wa Umma, nalo ni la kufoji vyeti.

Inashangaza watumishi wawili au watu wote kutumia cheti kimoja. Hii ni aibu kwa Taifa changa kama letu, ambalo tunatafuta maendeleo kwa haraka. Napenda kuishauri Serikali kupitia vyombo vyake, ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwa watumishi wake na wakibainika wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, pia tatizo la watumishi hawa kutokuwa na kauli nzuri ni malalamiko ya Wananchi wengi; kwa mfano, maeneo yanayolalamikiwa zaidi ni kwenye Mahakama zetu, Polisi, Sekta ya Afya, Ardhi, *TRA,* Bandari na Halmashauri za Wilaya, kumekuwa na urasimu mkubwa ukifika huko kama unaulizia jalada (*file*) lako, basi utazungushwa mpaka utoe kitu kidogo, yaani fedha ili upate huduma. Ushauri kwa Serikali ni kujipanga kwa kuwagundua hao watumishi na kuwaadhibu kwa mamlaka ya sheria zilizopo. Pia naiomba Serikali kupitia Wataalam wa masuala ya Kompyuta, waweke zuio la matumizi ya mitandao ya kijamii kama *Facebook, Twitter, Twoo* na mingine katika Ofisi zote za Serikali kwani inachangia sana watumishi hawa kutofanya kazi na muda mwingi ku-*chart* kwenye mitandao hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lililopita nilizungumzia suala la wafanyakazi kukaa kituo kimoja cha kazi kwa miaka mingi bila kuhamishwa. Narudia tena; kufanya hivyo ni makosa kwani watumishi hao hujenga mazoea katika maeneo yao ya kazi na kuzidisha mianya ya rushwa. Inafikia mahali mtumishi akipata fununu za uhamisho nae anatishia kuacha kazi; najiuliza mtumishi huyu anatoa wapi ujasiri huo ilhali akijua uhamisho ni sehemu ya sheria za kazi?

Vilevile nilizungumzia suala la watumishi hawa kupewa nafasi za kujiendeleza kielimu; hapa pia kuna matatizo makubwa katika hizi nafasi, watumishi wachache wanajikuta wakipewa kipaumbele kila wakati huku wengine wakikosa. Naomba liangaliwe kwa mapana na kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la baadhi ya watumishi kujiingiza katika mambo ya kisiasa na hili tatizo limefika mpaka kwa Wakurugenzi lakini hakuna hatua stahiki zilizochukuliwa.

Hilo linafanyika kwa kuwa mtoa maamuzi nae ni mwanasiasa, inamuwia vigumu kufanya maamuzi au wanasikiliza maoni ya wanasiasa ambao wako kwenye vyama vyao ama kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, tatizo la watumishi kugomea kwenda kufanya kazi vijijini ama kwenda kukaa kwa muda mfupi na kuondoka, limekuwa kubwa sana. Naishauri Serikali iweke mazingira mazuri kwa watumishi wa vijijini ili kuwapa moyo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini linakabiliwa na changamoto nyingi katika Sekta za Elimu, Afya, Ulinzi na Usalama, Kilimo na Mifugo. Watumishi hawa mishahara yao hufika kwa kuchelewa sana na ikizingatiwa Halmashauri iko mbali, vitendea kazi duni. Nashauri Serikali iboreshe upungufu huo ili kuleta tija kwa watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA**: Mheshimiwa Spika, niwanapongeza Mawaziri husika kwa uandaaji mzuri na uwasilishaji mzuri. Vilevile ninazipongeza Idara zote kwa uendeshaji na ufanisi katika Idara husika.

Mheshimiwa Spika, maandilizi ya Katiba yanakwenda vizuri. Ushauri ni kwamba, tusonge mbele kwa umakini uleule ambao tumesimama nao tangu zoezi lianze.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara kwa Watumishi; maisha yanaendelea kuwa magumu na gharama kupanda. Hivi sasa hata gharama ya usafiri hasa daladala, ni vizuri kiwango cha chini cha mshahara kikaangaliwa haraka.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umekuwa wa manufaa. Ninashauri mafunzo kwa wajasiriamali yaongezwe na hasa mahesabu madogo na njia ya kupanga bei bila ya kuleta hasara. Pia uelewe kuwa mikopo ni ya biashara na siyo kwa matumizi mengine na kuwa utamaduni wa kulipa ni muhimu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu hususan Tume ya Mipango – Fungu 66 ni chombo muhimu katika kuinua uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya Wananchi. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2012/2013, kumekuwepo udhaifu na upungufu mbalimbali ambao unapaswa kuondolewa au kurekebishwa katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Marekebisho ya Sheria Na. 11 ya mwaka 1989 iliyounda Tume ya Mipango, yalipaswa kukamilika katika mwaka 2012/2013, kwa sababu mchakato ulianza toka mwaka 2011/2012. Kipindi cha miaka miwili na nusu kimepita cha uhai wa Bunge, ambayo ni nusu ya muhula. Kama hatua hii haitaharakishwa, miaka miwili na nusu iliyobaki bila utekekelezaji wa mpango wa maendeleo kukamilika kutokana na udhaifu katika mfumo wa upangaji na utekelezaji; hivyo, kabla ya kuweka mkazo kwenye kuanzisha chombo kipya kiitwacho *President's Delivery Bureau*, nguvu zielekezwe kwenye kuiwezesha Tume ya Mipango. Kama ni lazima kuwa na *PDB* na kwa kuwa Tume ya Mipango nayo iko chini ya Rais kama Mwenyekiti; itungwe Sheria moja ya Mipango, Usimamizi na Ufuatiliaji, itakayounganisha mifumo yote, kupunguza gharama na kuongeza ufanisi bila mgongano na mwingiliano (*Dublication and Overlaps*).

Katika kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013, Tume ya Mipango imeeleza kwamba imefanya uchambuzi wa mipango kazi ya kisekta na ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo. Naomba kupatiwa nakala ya ripoti ya tathmini na uchambuzi huo katika Sekta ya Maji na Ujenzi hususan juu ya Miradi ya Maji na Barabara za Kupunguza Msongomano katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, katika majumuisho, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, anipatie majibu mahususi kutokana na mapendekezo niliyoyatoa wakati Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unapitishwa Bungeni Juni, 2011 na pia michango niliyotoa kuhusu Tume ya Mipango wakati wa mijadala ya Bajeti ya Ofisi ya Rais mwaka 2011 na 2012.

Juu ya kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014, nilipata fursa ya kutoa mapendekezo mwezi Januari, 2013 kupitia Kamati ya Fedha na Uchumi. Hata hivyo, Mpango ulipotoka mwezi Machi na Aprili, 2013, mapendekezo hayakuzingatiwa pamoja na kuwa niliyatoa nikitaka vipaumbele na viwango vya mgawanyo wa rasilimali kuzingatiwa kwa kadiri ya Mpango wa Miaka Mitano. Hivyo, katika majumuisho, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aeleze ni kwa nini mapendekezo hayo hayakuzingatiwa na ni lini yatazingatiwa ikiwemo kutenga bilioni 100 za ujenzi wa barabara za pembezoni za kupunguza foleni na bilioni 200 za kuweka mtandao wa mabomba ya maji katika maeneo yaliyowekwa. Pia, kuzingatia mapendekezo juu ya kuwezesha Wananchi kukabiliana na ongezeko la gharama za maisha na kudhibiti mfumko wa bei.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa sijapokea majibu ya michango yangu Bungeni kuhusu Fungu 20 na Fungu 30 kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na 2012/2013 pamoja na ahadi iliyotolewa ya kupatiwa majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu, ikiwa ni shehemu ya majukumu yake ya kuongeza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali, naomba itoe majibu kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, iwapo mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliyotajwa kwenye aya ya 13 ilishughulikia pia waraka kuhusu ya tathmini au uperembaji wa viwanda vilivyobinafsishwa. Katika miaka ya 2011/2012 na 2012/2013, Serikali iliahidi kufanya hivyo. Katika kutoa taarifa hiyo, Ofisi ya Rais, ieleze hatua zilizochukuliwa kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa na kudidimia katika eneo la viwanda la Ubungo. Itakumbukwa kwamba, Serikali iliahidi kulifanyia kazi pendekezo nililotoa na kuchukua kutoka eneo hilo la viwanda, kiwanja kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo ili kukuza ajira kwa vijana. Aidha, Ofisi ya Rais ieleze hatua iliyofikia katika kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Rais alizotoa katika Jimbo la Ubungo; mfano, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kutoka Kimara – Mavurunza – Bonyokwa, ujenzi

wa Machinga Complex na jengo la viwanda vidogo vidogo katika kiwanja kilichokuwa kinamilikiwa na *Simu 2000* Sinza.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ieleze hatua iliyofikiwa kuhusu uchunguzi wa madai ya ufisadi katika Miradi ya Maji kata ya Goba na Kata ya Ubungo (Msewe Golani), kwa kurejea barua nilizowasilisha mwaka 2011 na 2012. Aidha, TAKUKURU imechukua hatua gani mpaka sasa juu ya ripoti ya uchunguzi wa uvamizi wa maeneo ya wazi katika Jiji la Dar es Salaam ya mwaka 2010 ambapo TAKUKURU ilishiriki kuchunguza? Pia, TAKUKURU ieleze kuhusu uchunguzi juu ya malipo kwa Kampuni ya Twiga Cheimicals ikiwemo juu ya eneo la Kimara Baruti kama ambavyo *CAG* alibainisha na maswali ya nyongeza nikayahoji Bungeni mwaka 2011 na 2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Serikali ieleze sababu za hati miliki za eneo la Kimara Baruti kuchelewa toka 2011 na lini hasa hati hizo zitatolewa. Nachukua fursa hii kuwaalika Watendaji wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea *(PTF)*, kuendesha mafunzo kwa wateja wa mikopo ya nyumba na wajasiriamali katika Jimbo la Ubungo ikiwemo kuhusu taratibu mpya zilizoandaliwa. Aidha, Ofisi ya Rais imkumbushe Mheshimiwa Rais kuhusu ahadi yake aliyoitoa Jimboni Ubungo tarehe 20 Machi, 2013 ya kukutana nasi Ikulu tarehe 25 Machi, 2013 kuhusu hatua za kuboresha upatikanaji wa maji Jijini Dar es Salaam kwa kuwa tarehe hiyo ilipita bila mkutano kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake (Fungu 9, 32, 33, 67, 94), juu ya Bodi ya Mishahara, Serikali iwasilishe Bungeni ripoti ya maoni ya wadau mbalimbali kuhusu uwiano baina ya tija, mishahara na maslahi pamoja na kuchukua hatua kuongeza kima cha chini cha mishahara kufikia Sh. 315,000 kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi *(TUCTA)* katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Serikali iongeze fedha katika vifungu na kasma zinazohusu uchunguzi ili kuwezesha chombo hiki muhimu kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya nchi na Sheria. Aidha, badala ya kutenga fedha kwa ajili ya Sekretarieti kulipa pango la Makao Makuu yake, mgogoro wa kiwanja cha Makao Makuu ya Sekretarieti upatiwe ufumbuzi katika mwaka wa fedha 2013/2014. Serikali ieleze sababu za mgogoro huo kutopatiwa ufumbuzi katika mwaka 2011/2012 na 2012/2013 kama nilivyopendekeza katika michango yangu ya miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, ni muhimu Sekretarieti ikatoa maelezo ya ziada juu ya sababu za kutomaliza madai ya malimbikizo ya mishahara na posho kwa Watumishi wa Umma ikiwemo waajiriwa wapya. Aidha, Wizara itoe kauli kuhusu sababu za wahitimu wa Vyuo mbalimbali vya Kilimo kutokuajiriwa mpaka sasa pamoja na ahadi ya Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, juu ya Tume ya Utumishi wa Umma; Idara ya Utumishi wa Walimu itoe majibu Bungeni kuhusu hatua/uamuzi uliofanywa na Mahakama kufuatia mgogoro kati ya Walimu na Serikali. Malalamiko ya Walimu ni kwamba mpaka sasa msuluhishi hajapatikana na usuluhishi haujafanyika. Hali hii ina athari kubwa sana katika Sekta nzima ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma *(TPSC)* kishirikiane na Ofisi ya Bunge kuendesha mafunzo maalum ya Makatibu na Wasaidizi wa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) uratibu mfumo wa mitandao ya Serikali ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Umma yanayofanyika hivi sasa. Serikali kupitia Wizara ya Habari na Idara ya Habari Maelezo, ilianzisha tovuti ya wananchi miaka michache iliyopita kwa gharama kubwa. Serikali itoe maelezo ya sababu za kuingia gharama nyingine kutengeneza tovuti nyingine ya wananchi. Hali hii iko pia kwa tovuti kuu ya Serikali

na Serikali ieleze mchanganuo wa kiwango cha fedha kilichotengwa kwa mwaka kwenye miradi ya maendeleo ya Serikali Mtandao (eGA).

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ni Taasisi nyeti na muhimu kwa Taifa hili. Uchumi na ukuaji wake unategemea sana Utawala bora zaidi katika kuepukana na rushwa. Taasisi hii kazi zake ni ngumu na zenye changamoto kubwa. Hii haitafanikiwa endapo tu mfumo uliopo utaendelea. Wanafanya kazi katika mazingira magumu ya vitisho na kadhalika. Kubwa la msingi, Taasisi hii ipewe meno ya kuchunguza na kushtaki ili kuweza kuonyesha *deliverables*. Tukumbuke kizazi cha sasa siyo sawa na kizazi cha jana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengi yanayofanywa na Taasisi hii katika mapambano dhidi ya rushwa, *(i.e* Uhamasishaji elimu ya Umma kwa wananchi hadi mashuleni, TAKUKURU utaratibu) Muswada uletwe Bungeni ili wapewe meno zaidi ya kuchunguza na kushtaki pasipo kusubiri Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchaguzi unapokaribia, pia elimu ya Uraia juu ya kuepukana na mambo hayo inatakiwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi haijaelezea vipaumbele/mkakati wa Serikali kwa mwaka 2013/2014. Nini matarajio ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKURABITA; pamoja na Hatimiliki bado mabenki yanaweka ngumu kukopesha. Wananchi wa kawaida wanashindwa kutumia hati hizi kulipa kwa sababu bado hazitambuliwi na mabenki, wakati Serikali inaelewa fika kuwa wananchi wa vijijini hawana *Collateral* kama nyumba zenye hati na kadhalika. Serikali itoe ufafanuzi kwenye eneo hili, ifungue milango ili wananchi wa kawaida waweze kukopa kwa ajili ya maendeleo yao yatakayowaondolea umaskini. Aidha, usimamizi wa miradi yake ya vijijini uimarishwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *TASAF. TASAF* inafanya kazi nzuri lakini bado usimamizi wa miradi yake kule vijijini (Wilayani) unapwaya. *TASAF I* ilifanya vizuri kwa sababu usimamizi wake ulifanywa vizuri na Mhasibu wake Wilayani, lakini *TASAF II* wakakasimu usimamizi kwa Halmashauri, ufanisi ukaporomoka.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TASAF III* isimamiwe na mtumishi wake kama ilivyofanya kutekeleza *TASAF I*. Dhana ya *D by D* kwa *TASAF* kwamba wenyewe huko huko wasimamie, itapelekea miradi ya *TASAF* kukwama. Aidha, napendekeza kuwa Kamati ya Kudumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) isimamie *(oversight function)* kukagua miradi ya *TASAF* badala ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala ili miradi hiyo iweze kukaguliwa kwa karibu zaidi na kwa ufanisi na pia kwa sababu miradi hii iko kwa wananchi chini ya Serikali zao za Mitaa.

(3) Mheshimiwa Spika, Kima cha chini kuongezeka kutoka Sh. 150,000 hadi Sh. 170,000 yaani ongezeko la Sh. 20,000, siyo sawa kwa wakati huu. Miaka ya nyuma, wakati uchumi ulipokuwa nafuu, ingekuwa sawa. Lakini nyakati hizi ambapo mfumuko wa bei ni mkubwa, Sh. 20,000 haitoshi na wala haieleweki. Nashauri kima cha chini kiongezeke kwa Sh.100,000 (angalau) na kuwa Sh. 250,000. Naiomba Serikali iliangalie hili isijekuwa *gesture* hii ya Serikali ya kuongeza Sh. 20,000 ikasababisha manung'uniko makubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekretarieti ya Ajira, chombo hiki kikasimu zaidi madaraka yake kwa Mikoa na Wilaya kwa watumishi wa ngazi za chini. Sheria ya kufanya hivyo bado haijatekelezwa na hivyo kusababisha manung'uniko mengi kwa Mikoa na Wilaya zake kuhusu upungufu wa watumishi. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kurekebisha hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Siberia, naishauri Serikali ione uwezekano wa kuwa na Siberia ya wale wote wanaoeneza siasa za chuki, udini, ukabila, wezi na wabadhirifu wa mali za Umma ili kuliondolea Taifa janga. Wafungwe huko kwa Sheria maalumu ili warekebishwe.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja katika sehemu kuu tatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kuhusu uratibu au mgawanyo wa fedha za mradi wa awamu ya tatu ya *TASAF,* ambapo kwenye hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu alizungumizia fedha za matumizi ya takribani Shilingi bilioni 440, ambapo zimeainishwa kuwa ni kwa ajili ya kunusuru kaya zilizo maskini katika maeneo makuu manne, kwamba ni chakula, lishe bora, afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni vigezo gani vinatumika kutambua hizo kaya ni za umaskini? Ningependa kujua kama hivyo vigezo vimetumika kutambua hizo kaya 3,056 katika Halmashauri ya Bagamoyo. Lakini pia ningependa kujua ni kiasi gani cha fedha kinatarajiwa kugawiwa kwa kila kaya masikini na zaidi ni kiasi gani kwa chakula kwa mwaka na/au mwezi, kiasi gani cha fedha kwa ajili ya chakula/lishe bora, kiasi gani cha fedha kwa ajili ya Afya na Elimu pia?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliambie Bunge lako Tukufu ni kiasi gani cha fedha kwa mwezi, na hii/au huu utaratibu utakuwa endelevu au utakoma, baada ya Awamu ya Tatu ya *TASAF* kwisha?

Mheshimiwa Spika, ilevile ningependa kujua kama itakuwa inatolewa fedha taslimu kwa kaya au kuna muundo mwingine ambao utatumika katika kuhakikisha huduma lengwa zinamfikia mlengwa katika kila kaya.

Mheshimiwa Spika, mbali na kutoa fedha taslimu, pia kuna njia nyingine kama utoaji wa vocha au kadi ambapo kaya hizi hupewa kulingana na mahitaji husika kama ni elimu, afya na lishe, kwani ni dhahiri kuwa siyo kila kaya itakuwa na uhitaji unaowiana. Mahitaji yatatofautiana kulingana na idadi ya watu katika kaya, umri wa wanakaya na kadhalika. Hivyo utoaji wa vocha utadhibiti mianya ya watendaji wabadhirifu ambapo fedha lengwa hazifiki kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ambayo inaweza kuwa mbadala hasa kwa upande wa huduma ya afya na elimu, hizi zinaweza kutolewa kwa njia ya *Post paid*, yaani mlengwa anapatiwa huduma halafu Ofisi inaratibu zoezi la mgao wa hizo huduma. Hii itaondoa mianya ya ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ni juu ya ubambikwaji wa kesi. Tumeshuhudia ubambikaji wa kesi na hasa hili limekomaa kwenye Wilaya ya Tarime na Rorya, yaani Mkoa wa Kipolisi wa Tarime/Rorya. Yaani wananchi hawa wanabambikwa kesi, kunusurika kwao ni kutoa hongo/rushwa ili waachiwe. *In fact* hawakutenda hayo makosa. Vilevile tumeshuhudia Polisi wakiua raia tena pasipo na ukiukwaji wa Sheria au mashambulizi na wengi wao wanateswa na hata kupoteza maisha wakiwa mikononi mwa Polisi. Hili halikubaliki. Naiomba Serikali iingilie kati ili kurejesha amani na mahusiano bora na Jeshi la Polisi, kwa maana ya mahusiano mema kati ya Raia na Walinzi wa Raia ambao ni Polisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya mwenendo wa kesi kuchukua muda mrefu na ambazo zimejaa nyayo za rushwa na wenye haki ni wenye fedha na wanyonge daima hawana haki.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba haki itendeke kwenye suala lote la kuhusu utekaji na hata uuaji wa

Waandishi wa Habari. Maana imekuwa ni kwa muda mrefu sasa matukio haya yakiendelea hapa nchini na hamna hatua yoyote iliyochukuliwa. Tumeshuhudia vilevile viongozi wa kidini wakiua (Padri Zanzibar), na wengine kumwagiwa tindikali (Sheikh Zanzibar), hii inahatarisha sana amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tumeshuhudia mauaji ya wanawake kule Wilaya ya Butiama, Manispaa ya Musoma. Wanawake hawa wamekuwa wakiuliwa, lakini Serikali haijaonyesha jitihada zozote zile za kukomesha uharibifu huo ambao unasadikika ni wa kiimani, ya kuwa hawa wanawake wamekuwa waking'olewa sehemu mbalimbali za mwili wao kama vile viungo vya uzazi, matiti na hata damu zao. Hii inazorotesha juhudi za uzalishaji mali/kukuza uchumi. Hivyo kubaki majumbani kwa uwoga wa kuuawa. Haya mauaji hufanyika nyakati za asubuhi na mchana.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaomba chombo cha kupambana na rushwa nchini, lakini Taasisi hii haijaweza kufanya kazi kwa ufanisi kutokana na changamoto nyingi, kama vile watuhumiwa kutokuchuliwa hatua, vitisho na rushwa ndani ya TAKUKURU wenyewe.

**MHE. ANGELLAH JASMINE KAIRUKI**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kombani – Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Steven Wassira, Mheshimiwa Prof. Mwandosya na Mheshimiwa George Mkuchika, Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu wote na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Taasisi zilizopo chini ya Rais, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nami napenda pia kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia malalamiko mbalimbali dhidi ya Watumishi wa Serikali na Taasisi zake, nashauri kuanzishwe Taasisi ya "OMBUDSMAN" itakayoshughulikia malalamiko dhidi ya Watumishi zitolewazo na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira ina kazi sana. Aidha, muhimu sana wakahakikisha kwamba wanaajiri watu wenye sifa za hali ya juu. Hususan, ninashauri ikiwezekana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapopewa kibali cha kuajiri basi aruhusiwe kuajiri watu anaoona wanafaa na pia, anaweza hata kuwa anachukua moja kwa moja kutoka Taasisi ya Uanasheria kwa vitendo ili kuwa na uhakika na ubora wa watu anaowachukua. Aidha, akishawa-*spot* basi ndiyo anaweza kuwafanyia usaili na kukamilisha taratibu zingine za uajiri. Hii itasaidia kupata watu wenye weledi na sifa tarajiwa. Nasema hivi kwa sababu unakuta wenye sifa wanakuwa wameshachukuliwa na Taasisi zingine.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiona Wizara mbalimbali ambazo watumishi wake wamekuwa wakiacha kazi, kufariki na kustaafu, lakini utaratibu wa kuziba nafasi hizo kwa kupata vibali vya kuajiri tena vimekuwa vikichelewa. Ningependa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Utumishi), atakapofanya majumuisho, atoe ufafanuzi wa utaratibu huu ili kupunguza tatizo la ukosefu wa watumishi hususan kwa nafasi ambazo mishahara ipo tayari na kada hiyo ilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Ofisi ya Rais (Utumishi) inabidi waliangalie ni mtumishi wa kada nyingine anapojiendeleza na anabadilishwa kada *(recategorization)*, wengi wao wamekuwa wakipata mshahara wa chini sana, kiwango cha kutisha ukilinganisha na mshahara wa mwisho aliokuwa akiupata mtumishi husika. Nimefanya ziara katika Mahakama mbalimbali, wako Watumishi wa Mahakama ambao wamejiendeleza kutoka kwenye kada kama ukarani, ulinzi, upiga chapa na nyinginezo. Aidha, mtumishi huyo alishafikia kupata mshahara wa shilingi milioni moja na laki mbili, lakini cha kushangaza, baada ya kubadilishiwa kada na kuwa Hakimu, anahesabiwa kama ndiyo anaanza kazi katika kada ya Uhakimu na anakuwa sawa kimshahara na Mahakimu wengine ambao ndiyo kwanza wameajiriwa (*entry point*). Hali inayopelekea mtu kupata mshahara wa shilingi laki saba, ni punguzo kubwa sana. Watumishi wengi wamekuwa wakielezea kwamba, haina maana kujiendeleza

kwa kuwa utaishia kupata mshahara ambao ni pungufu na wa awali. Ningependa Mheshimiwa Waziri, ulifuatilie suala hili kwani linajitokeza kwa Watumishi wa Afya na Wizara kwa kada nyingine zinazojiendeleza.

Mheshimiwa Spika, Wakala nyingi zimeanzishwa kwa lengo la kuboresha utendaji na baadaye waweze kujitegemea na pia kuchangia katika Pato la Taifa. Ni muhimu Ofisi ya Rais (Utumishi), ikafuatilia kwa karibu utendaji wa Wakala zilizoanzishwa chini ya *Executive Act* kwani zingine hazitekelezi wajibu wake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulijadili ni ulipaji wa madai ya malimbikizo ya mishahara. Mfumo wa *Lawson* ambao unatumika kuingiza taarifa za watumishi, maafisa utawala wengine wamekuwa wakihujumu ufanisi wake. Wengine wamekuwa hawaingizi kwa wakati taarifa za kiutumishi za watumishi waliopo katika Wizara zao. Naomba ufuatiliaji wa karibu na wa mara moja ufanyike ili kuhakikisha kumbukumbu zinaingizwa kwa wakati. Ninao uthibitisho, mtu ameajiriwa miezi saba ndipo baadaye afisa anajaza taarifa zake kwenye *Lawson* tena baada ya kukumbushwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Nchi mbalimbali wana Kituo Maalum cha Kitaifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu za Taifa (*National Data Center*) na kimsingi kwa Tanzania kituo hiki kingekuwa mwafaka endapo kingekuwa chini ya Ofisi ya Rais (Utumishi) – Wakala wa Serikali Mtandao. Wizara na Taasisi zingine wanaweza kuwa na *Servers* zao kwa ajili ya taarifa zao, lakini mwisho wa siku ni lazima *E-Government* wawe na *Server* yao kubwa ambayo ndiyo ita-*host National Data Center*. Kumbukumbu ambazo zinaweza kuwemo katika *National Data Center* ni kama vile kumbukumbu zote za kiutumishi, Hazina, Usajili wa Vizazi na Vifo, Uraia, Vitambulisho vya Taifa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuipongeza Ofisi ya Rais (Utumishi) kupitia Mradi wake wa *Regional Communication Infrastructure Programme,* ambao hadi sasa

umefanya kazi nzuri. Aidha, niombe tu Mradi uangalie uwezekano wa kututengenezea mfumo wa *Birth and Death Registration System* pamoja na kuweka mfumo wa kielektroniki kwa Mahakama hususan, kutuunganisha (*Network)* ili kurahisisha kazi na kuleta ufanisi pindi Mradi wa Mahakama wa *TELEJUSTICE* utakapoanza ukute mtandao uko tayari.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni muhimu sana katika kutoa huduma za kifedha na mafunzo kwa wajasiriamali wadogo. Kazi ya Mfuko huu ni ndogo sana, kunahitajika maboresho ya hali ya juu kitaasisi na kuiwezesha kifedha. Ukiangalia katika ukurasa wa 34 wa Hotuba ya Ofisi ya Rais (Utumishi), Mfuko umetoa mafunzo kwa wateja wake wa Kibaha, Morogoro na Turiani. Mahitaji ya wajasiriamali ni makubwa na kazi ya Mfuko ni ndogo. Ni vyema kazi iongezwe ili Wananchi wengi zaidi waweze kupata mikopo na mafunzo kuhusiana uendeshaji wa biashara, utunzaji wa fedha, masoko na kadhalika. Aidha, riba zinazotozwa hivi sasa na Mfuko huu ni kubwa. Ni muhimu wakafanya mashauriano na Taasisi mbalimbali za fedha kama vile *UTT* ili waweze kukopeshwa fedha kwa riba nafuu ili nao *PTF* wakopeshe wateja wake kwa riba ambayo itamnufaisha mjasiriamali na Mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, bado bajeti yao ni ndogo; hivyo, ni vyema hoja zaidi zijengwe ili kuiwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi. Ni muhimu pia, wigo wa Viongozi wanaowajibika kujaza fomu za mali na madeni uongezwe. Na kwa kuanza maafisa wote wa Shirika la TRA, Wakurugenzi Watendaji wote wa Halmashauri, Manispaa na Wilaya na wengine nao wakaguliwe mali zao. Aidha, Sekretarieti ya Maadili inaweza pia kutumia taarifa za hali ya Rushwa nchini na Ripoti zingine za Kimataifa ambazo zimefanya utafiti kuangalia Sekta ambazo zinatajwa kuongoza kwa rushwa, basi ni muhimu Viongozi na Maafisa wao wakaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA**: Mheshimiwa Spika, mchango wangu ninaishauri Serikali kuangalia Watumishi wa Serikali ambao siyo waaminifu hasa Makatibu Wakuu wa Wizara wamekuwa siyo waadilifu kwenye Utumishi wao. Makatibu hawa wanaoharibu kwenye Wizara na kujilimbikizia mali, wafukuzwe kazi mara moja na kuajiriwa Makatibu wengine na siyo kuhamishwa Wizara hii na kupelekwa Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa Kiongozi kujaza fomu za Serikali na kuorodhesha mali zao na hii ni kwa mujibu wa Sheria. Viongozi ambao wanakiuka Sheria hii na kuiibia Serikali na kujilimbikizia mali ambazo hawakuzipata kwa njia ya halali; je, Serikali imewachukulia hatua gani watu kama hawa?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Viongozi ambao wanamiliki mashamba ambayo yamegeuka na kuwa mashamba mwitu (pori). Hii inapelekea kusababisha migogoro na Wananchi na Wananchi kuichukia Serikali yao. Ni kwa nini Serikali inapobaini kama kuna Viongozi ambao siyo waadilifu haiwachukulii hatua na hizo mali kuzigawa kwa Wananchi ambao ni maskini?

Mheshimiwa Spika, suala la Watumishi wa Serikali kuhamishwa mkoa huu na kupelekwa mkoa mwingine imekuwa ni kero, unakuta Mtumishi wa Serikali anatolewa Ruvuma anapelekwa Dar es Salaam na aliyetolewa Ruvuma mazingira ya Dar es Salaam hayajui. Kwa nini Serikali haiwaajiri Watumishi wa Serikali ambao wametoka mkoa ule ule na wanazijua kero za mkoa huo?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro, ubadilifu na tabia ya kutoheshimu Utawala Bora. Kwenye Halmashauri kumekuwa na kusambaa mpaka kwenye ngazi za Kata na Vijiji kwani sasa Watendaji wa Vijiji na Kata wamejigeuza na kuwa wao ni Polisi, Mahakama na Magereza na kusababisha migogoro baina ya Serikali na Wananchi. Kwa nini Serikali inapogundua matatizo kama haya isiwachukulie hatua na kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima?

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU inapowakamata baadhi ya Viongozi ambao wanahusika na rushwa na kupata taarifa kwa Wananchi mfano, kuna baadhi ya Viongozi wanahusika na rushwa; kuna baadhi ya Viongozi ambao siyo waadilifu katika kazi zao za kupambana na rushwa, wanapopata taarifa kutoka kwa Wananchi wamekuwa wakienda kuwaambia wahusika na wale wahusika ambao wana uwezo mkubwa, wamekuwa hawafikishwi mahakamani, wanaofikishwa kwenye vyombo vya sheria (mahakama) ni wale watuhumiwa wanaohusika na rushwa ndogo ndogo, wanaohusika na rushwa kubwa kubwa hawafikishwi Mahakamani na hatujui kesi zao zinaishia wapi. Kwa nini Serikali haiangalii upya Sheria za TAKUKURU na kuipa TAKUKURU mamlaka ya kufanya kazi kwa uadilifu bila ya kuingiliwa na Serikali na Wananchi wawe na imani na hiki chombo cha kupambana na rushwa na kionekane kinafanya kazi kwa mujibu wa sheria bila upendeleo wowote.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE**: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Celina Kombani (Mb) - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi), kwa uongozi wake mahiri. Vilevile nampongeza Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwa utendaji wao mzuri. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kushughulikia ushauri na maoni niliyotoa wakati wa mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) mwaka 2012/2013 bila kuchelewa. Hongera sana kwa usikivu wenu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira ya watumishi wapya na ujazaji wa nafasi zinazoachwa na watumishi wanaofariki au kuacha kazi; utendaji wa Serikali na Taasisi zake umekuwa ukilegalega kwa sababu ya kutokuwepo Watumishi wa kutosha kutekeleza mipango iliyoidhinishwa kwa sekta mbalimbali. Sababu kubwa inayosababisha upungufu huo ni urasimu katika uidhinishaji wa ajira pamoja na mchakato wa ajira kuchukua muda mrefu sana. Nashauri kuwa:-

(a) Ili kuharakisha ajira mpya, isiwepo haja ya mwajiri kuomba kibali cha kuajiri, badala yake kibali cha

ikama kilichotolewa na Utumishi kiwe kibali cha mwisho ilimradi mwajri apate fedha kwa nafasi inayohusika. Mara baada ya kupata fedha, mwajiri huyo apeleke mapendekezo yake Sekretarieti ya Ajira kwa ajili ya kushughulikiwa. Sekretarieti ya Ajira ipewe muda wa juu (*deadline*) usiozidi miezi mitatu kukamilisha taratibu za ajira na kuwasilisha mapendekezo kwa mwajiri. Ikiwa Sekretarieti itashindwa kukamilisha mchakato katika muda huo, mwajiri awe huru kutangaza nafasi na kuajiri waombaji watakaofaulu kwenye mchakato atakaoendesha yeye;

(b) Kujaza nafasi zinazoachwa wazi na watumishi wanaofariki au kuacha kazi; kwa vile mtumishi anapofariki au kuacha au kuachishwa kazi anaacha nafasi wazi yenye fedha, mwajiri atakiwe kutoa taarifa Utumishi na kuendelea kujaza nafasi hiyo bila kusubiri kibali cha Utumishi.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia kwa karibu utekelezaji wa Miradi inayopata fedha toka *TASAF* katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha Mkoani Arusha. Tunashukuru kwa uwezeshaji kidogo tuliopokea kwani imesaidia kupunguza kero pale ilipofikia. Hata hivyo, yako maombi mengi ya Wananchi walioibua Miradi mbalimbali ambayo hadi sasa hayajapatiwa majibu. Kwa ufupi ni kwamba, kiasi cha Miradi iliyotekelezwa kwenye Wilaya hiyo kupitia Mfuko huu ni kidogo sana. Naomba Miradi iliyowasilishwa ya Maji, Barabara, Elimu, Afya na maeneo mengineyo, ipatiwe fedha ili kupunguza kero zinazowakabili Wananchi wa Wilaya hiyo ambayo ndiyo Jimbo ninalowakilisha.

Mheshimiwa Spika, ingawa Miradi ya *TASAF* huibuliwa na Wananchi na hivyo uwezekano wa kupata fedha za kutekeleza Miradi mbalimbali hutegemea uhodari wa Wananchi kuibua Miradi, uko ukweli pia kuwa uwezo wa Wananchi kuibua Miradi hutegemea uwezo na utayari wa Afisa wa *TASAF* Wilayani kuwahamasisha na kuwasaidia kuandaa miradi hiyo. Ikiwa Afisa hana ari ya kusaidia Wananchi wahusika, watabaki na kero zao bila suluhisho. Hivyo, nashauri kuwa kila Wilaya itengewe kiasi fulani cha

fedha *(minimum allocation*), ambayo itatolewa kutekeleza walau Mradi mmoja ulioibuliwa na Halmashauri ya Wilaya.

Tunaishukuru Serikali kwa kuweka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Hata hivyo, inaelekea kuwa Wananchi wanaoelewa uwepo wa Mfuko huu ni wachache sana, kwa sababu hakuna habari wala elimu kwa umma inayotolewa. Ni vizuri taarifa juu ya Mfuko huu ikapelekwa wilayani na vijijini ili Wananchi wanufaike nao. Aidha, yako malalamiko kwa Wananchi wachache waliowahi kukopa kutoka Mfuko huu kuwa riba inayotozwa ni kubwa sana kuliko ya Benki za Biashara. Nashauri kuwa, riba ipunguzwe ili Wananchi wa kipato cha chini wamudu gharama zake na waweze kujipatia mtaji wa kujiwezesha kibiashara.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE**: Mheshimiwa Spika, kwa njia ya maandishi nichangie Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Awali ya yote, nibainishe kuwa majukumu ya Ofisi hii ni muhimu kwa ustawi na mustakabali mzima wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maelekezo yangu ni kwa Sekretarieti ya Ajira. Mfumo wa kuajiri au kutoa vibali vya ajira kutoka Makao Makuu umekuwa na upungufu. Umekuwepo urasimu hasi na ucheleweshaji wa kuajiri watumishi. Madhaifu ni pale ambapo Sekerarieti au Ofisi inaposhindwa kutoa ajira kwa sekta ambazo uwepo wa Watumishi hao mafanikio yanaonekana mara moja. Kushindwa kutoa vibali vya ajira kwa Sekta ya Nishati na Madini ambako rasilimali zenye thamani kubwa zinaachwa bila watendaji kisa vibali vya ajira. Pamoja na Bajeti na uwezo mdogo wa Serikali kumudu mahitaji yote kwa wakati mmoja, sekta hizi ambazo zinaleta tija na uwezo wa kujiendesha mara moja zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nichangie utendaji wa TAKUKURU. Kitengo au Taasisi hii ni muhimu na ni chombo kinachoendeshwa kwa gharama kubwa. Hata hivyo, utendaji wake hauna tija inayotegemewa katika utendaji wake kazi na weledi wa kuzuia na kupambana na rushwa na hasa zile

zilizoko karibu na Wananchi walio wengi ni mdogo mno. Rushwa zilizoko karibu na Wananchi ndizo hasa zinazochafua taswira ya TAKUKURU. Kumekuwepo kudai, kutoa na kupokea kwa rushwa katika sehemu za huduma, hali inayowaaminisha Wananchi waamini kuwa hizi ni tozo halali. Nashauri Taasisi hii ielekeze nguvu kwa Wakuu wa Taasisi au Wizara kinara wa rushwa kero, kwa kuwaelimisha na zaidi kubuni mbinu na mikakati ya kuzuia vishawishi vya rushwa kwa kushirikiana na wakuu wa sehemu za kazi wala rushwa sugu wadhibitiwe hata kwa ushahidi wa mazingira.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kutoa maoni kuhusu mada tajwa hapo juu hususan mchango wangu katika Wizara zilizo chini ya Ofisi ya Rais zifuatazo: Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mahusiano na Uratibu; na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU imesaidia kwa namna moja au nyingine, kupambana na tatizo la rushwa hapa nchini ingawa inakabiliwa na changamoto zifuatazo: Kutotambulika kikatiba; ufinyu wa bajeti; kutokuwa na uwezo wa kushtaki na kuhukumu; baadhi ya maofisa wake kula rushwa; na baadhi ya watu hasa sehemu za vijijini hujifanya Maofisa wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na matatizo au changamoto tajwa hapo juu, napendekeza kuwa chombo hiki kiwezeshwe kwa kutengewa fedha za kutosha. Kipewe meno ya kukamata, kushtaki na hata kuhukumu pale kinapokuwa kimemkamata mtuhumiwa. Pia ufanyike uchunguzi wa kina ili kuwaajiri watu waadilifu katika chombo hiki nyeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TASAF* katika maeneo mbalimbali hapa nchini, bado inaonekana dhahiri kuwa kuna upungufu ufuatao:-

(a) Kutoa Miradi kwa upendeleo kwa baadhi ya Wilaya.

(b) Wananchi wengi hususan wa Vijijini hawaelewi maana ya *TASAF* na Miradi iliyo chini yake.

(c) Miradi ya *TASAF* huendeshwa kwa gharama kubwa katika Halmashauri zetu unapolinganisha na Miradi mingine.

(d) Elimu ndogo kwa Wananchi hasa wanaopewa pesa za *TASAF III.*

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na matatizo yote yaliyotajwa hapo juu, napendekeza kuwa, Waziri mwenye dhamana ya kusimamia *TASAF* ahakikishe kuwa, Miradi inayosimamiwa na *TASAF* inapelekwa kwa kila Wilaya bila upendeleo. Pili, Elimu kuhusu Miradi ya *TASAF* itolewe kila sehemu ya nchi. Tatu, Miradi ya *TASAF* ikaguliwe mara kwa mara ili kuona thamani halisi ya fedha iliyotumika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuizungumzia Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na baadhi ya Mawaziri ingawa si wote, ni wachache sana, napenda kushauri kuwa, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na hata Wabunge, wapewe *Performance Service Contract* ili kuongeza ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika napendakeza kuwa utendaji kazi wa Baraza la Mawaziri uwe shirikishi kwa misingi ya baadhi ya Wizara huingiliana katika Idara mbalimbali. Hivyo basi, badala ya kazi nyingi kuachwa TAMISEMI hasa katika Halmashauri zetu, naishauri Serikali ibuni mbinu mpya ya ushirikishi ili kurahisisha maendeleo ya nchi yetu. Kwa mfano, Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uvuvi na Mifugo na kadharika. Utendaji wa Wizara hizo hauonekani katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa misingi ya haki na Utwala Bora. Hata hivyo, inaonekana dhahiri kuwa katika kipindi hiki Serikali imeruhusu sana mambo ya Utawala Bora kuingiliwa na Wanasiasa uchwara wanaothubutu kuvuruga amani katika nchi yetu. Naomba maswali yafuatayo yajibiwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora):-

(a) Je, Utawala Bora bila kufuata na kutii Sheria za nchi, nchi inaelekea wapi?

(b) Je, Nyaraka nyeti za Serikali kwa nini zinazagaa mitaani?

(c) Je, tetesi kuwa baadhi ya Watumishi wa Usalama wa Taifa siyo waaminifu na watii ina ukweli ndani yake; na kama ndiyo ni hatua zipi zimechukuliwa?

(c) Nini hasa majukumu makuu ya Usalama wa Taifa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mawasiliano na Uratibu; kwa heshima na taadhima napenda kumwuliza Waziri wa Wizara husika maswali yafuatayo:-

(a) Serikali imelishughulikia vipi suala la udini linalojitokeza kwa kasi hapa nchini mwetu?

(b) Serikali inasita nini kuwachukulia hatua watu wote wanaoleta chokochoko za udini hapa nchini?

(c) Wajibu wa Waziri wa Wizara hii ili kuleta mahusano mema katika jamii ni mkubwa sana na hauwezi kupuuzwa hata kidogo. Je, Waziri ameitumia vipi nafasi hii ili kuleta mahusiano mema baina ya Vyama vya Siasa hapa nchini na Serikali yao?

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ni jicho la maendeleo katika nchi yetu. Mpango huu ukisimamiwa

vizuri na utekelezaji wake ukafanyika vizuri, nchi yetu itapiga mbele kimaendeleo.

(a) Mpango wa Maendeleo una vipaumbele vipi katika mwaka huu wa bajeti?

(b) Je, Mpango wa Maendeleo unasimamiaje rasilimali zetu za gesi, bahari, madini, misitu, wanyama na hata milima na mabonde ili kuweza kutekeleza vipaumble hivyo vya Mpango?

(c) Je, fedha za bajeti za mpango wa maendeleo zinatoka wapi?

(d) Je, kupitia Tume ya Mipango, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuhakikisha kuwa rasilimali za Taifa letu zinawanufaisha Watanzania wote?

(e) Ni lini Tume ya Mipango itawajumuisha *The Great Thinkers* wa nchi juu ya kutafakari ni namna gani ya kutumia rasilimali ya nchi yetu kwa manufaa ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO**: Mheshimiwa Spika, katika Kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Celina Kombani (Mb), ukurasa wa 106, Kiambatanisho Na. 2 kuhusu Miradi iliyoidhinishwa kwa makundi ya walengwa na fedha zilizotumwa na *TASAF* kwa kipindi cha Julai 1, 2012 hadi Machi, 2013 kwa Miradi ya Kaya zenye uhaba wa chakula katika Halmashauri ya Meru Mkoani Arusha. Je, ni Kaya ipi hiyo katika Halmashauri ya Meru ambayo ilipatiwa Mradi kutokana na uhaba wa chakula?

Mheshimiwa Spika, na je ni watu wangapi walipata huduma hiyo katika Halmashauri ya Meru kwa kiasi hicho cha fedha kilichooneshwa katika Jedwali Na. 2, ukurasa wa 106 cha Tshs. 65,091,863.89?

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, inaelezea kuhusu mkakati wa kupambana na kuenea kwa Virusi vya UKIMWI na UKIMWI mahali pa kazi. Utekelezaji wa mkakati huu ukoje na nini mafanikio yake katika kuzuia unyanyapaa kwa waathirika wa Virusi vya UKIMWI mahala pa kazi?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Waajiri wa Makampuni binafsi ambao wakishajua mfanyakazi fulani anaishi na Virusi vya UKIMWI huamua kumwachisha kazi kwa hofu kwamba uzalishaji wa mfanyakazi huyo utakuwa hafifu. Je, Serikali inalindaje ajira au nafasi za ajira za wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ili wasipoteze ajira zao kwa kunyanyapaliwa na waajiri wa Makampuni binafsi?

Mheshimiwa Spika, ili nchi iwe na uchumi imara na endelevu, tunahitaji Utawala Bora ambapo Sera, Sheria, Taratibu na kanuni bora zinatumika katika kusimamia uchumi na uendeshaji wa shughuli za Umma. Serikali ihakikishe kwamba, inasimamia vizuri Sera, Sheria na Taratibu zilizopo kwa maslahi ya Watanzania wote ili kuondoa uhasama uliopo katika jamii yetu. Tumeshuhudia Watanzania wasio na hatia wakiuawa, hali ambayo ni hatari na amani iliyokuwepo kwa muda mrefu inatoweka. Wananchi wa Tanzania wanaiangalia Serikali wakiamini kupata ulinzi kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma ni nzuri na kama zingekuwa zinafuatwa, kungekuwa na ufanisi katika Utumishi wa Umma. Ili Watumishi wa Umma wawe wenye ufanisi, Serikali inapaswa kuhakikisha wanafuata Kanuni zinazosisitiza haya yafuatayo:-

(a) Kufanya kazi kwa uadilifu, bidii za kazi, kuitii Serikali iliyopo madarakani. Japokuwa wewe ni Mpinzani

kutoa huduma bila kupendela, kuheshimu Sheria na mengineyo.

(b) Kuporomoka kwa maadili kunatokana na Serikali kutosimamia Maadili na Kanuni hizo. Kuna tatizo pia la watumishi kutojali muda wa kazi.

(c) Wapo wale ambao hawana uchungu wa nchi hii, wanatumia madaraka yao vibaya kuwatesa Wananchi ili kuipaka matope Serikali ambayo iko madarakani.

(d) Kuna tatizo sugu la rushwa ambalo linadhoofisha maendeleo ya nchi yetu, wachache wananufaika na wengi wanateseka. Ni vyema sasa hivi Serikali ikaja na mikakati ya kupambana na watumishi hawa kwa kuwapa adhabu watumishi hao ili iwe fundisho kwa wengine.

Suala la mtumishi kuhamishwa kwenye eneo lake baada kufanya kosa siyo suluhisho kupelekwa eneo lingine. Imefika wakati Serikali iwaadhibu watumishi bila kujali ni nani.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, nachangia kwenye Mradi wa *TASAF*. Ni kweli chombo hiki kinafanya kazi vizuri katika Miradi yake iliyopita; *TASAF I* na *II* na sasa tumeingia *TASAF III.*

Nashauri Serikali iongeze fedha kwani inaonekana Wananchi wamefahamu Mradi huu faida zake na kiasi kilichopagiwa ni kidogo.

Serikali iandae au iweke utaratibu mzuri kupitia Sekta zake ambazo ni Wizara ili Mradi ukianza kusitokee upungufu wa rasilimali watu na fedha zinazochangiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa MKURABITA umechukua muda mrefu wa kufanya *Dioginosis Studies, Researches* na kadhalika kuliko muda wa utekelezaji. Pia fedha nyingi zimetumika katika *Researches* hizo kuliko eneo la utekelezaji

na utaona kuwa fedha hizo nyingi zimechangiwa au kutolewa na wafadhili.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Mradi huu upo Dar es Salaam na utendaji unafanyika vijijini kama Katavi na Micheweni. Je, ni lini Serikali itaanzisha Programu hii huko Wilayani na Mkoani?

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHAMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii ya Ofisi ya Rais, Menenimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, naanza na nidhamu kazini. Ukienda katika Ofisi zetu za Serikali utakuta watendaji wanazungumza hata hawashughuliki na mgeni aliyefika pale. Wakati mwingine utamkuta Afisa wa Serikali anaongea na simu kwa muda mrefu hata hajali kuwa yuko kazini anapoteza muda mwingi kuongea na simu. Wafanyakazi wanatoka kazini kiholela, ikifika saa tano kwenye maofisi hakuna watu, wengi wanakwenda kwenye shughuli zao wanabakia wachache tu.

Mheshimiwa Spika, Magari ya Serikali yanatumiwa kwa shughuli za kibinafsi zaidi kuliko za Kiserikali. Utakuta magari yanafanya kazi baada ya saa za kazi, utayakuta katika mabaa, masoko na sehemu nyingi za starehe. Hali hii inadhihirisha wazi kuwa, hakuna nidhamu kazini. Naomba Serikali iliangalie kwa makini suala hili. Nidhamu inapokuwepo katika Maofisi ya Serikali, basi ufanisi unakuwa mkubwa sana, bila ya kuwapo kwa nidhamu kazini hakuna ufanisi utakaopatikana na nchi itazidi kudidimia kiutendaji.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika**,** hali ya kisiasa nhini tunaelekea kubaya. Kuna baadhi ya Vyama vya Siasa hasa CHADEMA wanaitizama nchi hii kwa mtazamo finyu, wao wanajifanya ni wamiliki wa nchi hii, wana mwelekeo wa kuona au kudhani kuwa kila wakionacho na

kukisema wao ni sahihi. Wana dhana ya kuona Serikali iliyopo madarakani haipo kwa maslahi ya umma. Mwendo wao wote umo katika harakati za ukombozi na kuweka taswira ya CHADEMA ni chama cha ukombozi. Baya zaidi ni propaganda wanayoiendesha na kusaidiwa na vyombo vya habari na mataifa au vikundi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo na sasa ingawa wanajitahidi kuelekeza nguvu zao kuchochea wanafunzi, madaktari na wafanyakazi, kwa kiasi fulani kama siyo jitihada zilizochukuliwa na vyombo vya usalama na Serikali yake, tusingekuwepo hapa leo, machafuko yangeanza zamani. Mtakumbuka wao ndiyo walioanza kudai Katiba mpya kwa ujasiri mkubwa, Serikali ikakubali, lakini wao ndiyo wanaokataa sasa. Tulipoingia madarakani mwaka 2010, wao walisusia Serikali na walitoka Bungeni wakati Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge na kupinga uhalali wa uchaguzi huo na ilhali wao kuingia Bungeni ni kutokana na uchaguzi huo au uhalali wa uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu; utakumbuka wakati wa matayarisho ya Muswada wa Sheria ya Katiba mpya, waliwakusanya Wanafunzi wa *UDOM* hapa Dodoma na kufanya fujo maeneo ya Bunge. Ukabila ndiyo dhana yao na sasa wanapendekeza suala la dini ambao halina mipaka.

Mheshimiwa Spika, bado tutegemee makubwa zaidi katika kipindi kijacho, kwani kutofanikiwa kwa yote hayo waliyoyafanya sasa, kama wanavyodai kutokubali mchakato wa Katiba, Udini, Ukabila Ukanda, Muungano na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, waliyofanya yanatosha, watu wamechoka na tafsiri iliyopo ni kuwa Serikali inawaogopa na haina uwezo. Ushauri wangu, Serikali ijipange upya yenyewe pamoja na vyombo vyake, Mahakama iharakishe kusikiliza na kutolea *judgement* haraka iwezekanavyo hasa kwa kesi ya uharamia. Vyombo vya usalama viangaliwe upya lakini na Polisi imo na utaratibu mzima wa upelelezi na kesi kwenda Mahakamani nao ufanye kazi ya ziada. Magazeti nayo pale walipotoa taarifa tata lazima

washitakiwe na kama sheria hazikidhi haja, basi zirekebishwe haraka kama inavyowezekana. Wabunge nao watoe ushahidi wa wayasemayo hasa kwa wanaotoa taarifa za kichochezi na wakishindwa wadhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, haya ni mapambano na ni uvunjifu wa amani katika nchi hii. Endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa, damu itakayomwagika itakuwa kubwa na nchi hii itakatika vipande vipande. Lawama zitakuwa kwetu CCM, tuangalie Somalia; nchi moja, dini moja, lugha moja na hata jirani zetu Burundi na Rwanda, mauaji yaliyotokea ni kwa sababu ya ulegevu na utashi binafsi wa wanasiasa.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, kwa nini kumekuwa na historia ya migomo katika Sekta ya Utumishi wa Umma katika nchi yetu? Mfano, Sekta ya Elimu na Afya; katika Afya imetokea migomo mara kadhaa tangu tupate Uhuru kama kwa mfano, 1974, 1990, 1995, 2002, 2005 na 2011/12 (Desemba, 2011 – Januari/Februari, 2012). Hali hii inatisha; je, Serikali imeweza kufahamu kwa utafiti wa kina kwa nini hali hii ya migomo katika Afya inajitokeza?

Kwa nini Wizara ya Afya hadi sasa ni mwaka moja na miezi minne hakuna uongozi rasmi (*substantive),* viongozi karibu wote ukiacha Mawaziri wanakaimu kama Katibu Mkuu, Mganga Kiongozi na wengine wengi wanakaimu? Hii ni kinyume na Sheria ya Utumishi mtu kukaimu zaidi ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, kwa nini mwaka jana (2011/12) kulikuwa na kibali cha ajira kwa Watumishi wa Afya zaidi ya 6,700 nafasi 2,000 zilibaki wazi? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, Sekretariet ya Ajira ivunjwe ili Sheria ya Ajira ya Halmashauri na Mikoa iwe na meno na ifanye kazi yake. Hii itasaidia kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na itaondoa mlundikano wa watafuta kujaa Dar es Salaam wakiulizia matangazo ya ajira.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa kesi na watumishi ni hafifu uimarishwe na pia utaratibu wa uwajibikaji kwa

watumishi uboreshwe kwa vile usimamiaji wa ujazaji *(OPRAS)* imeshindwa, ni vizuri utaratibu ubadilishwe kuwe na *Performance Contract,* ambapo mtumishi kiongozi atasaini kwa bendera ya nchi yetu na kuapa.

Mheshimiwa Spika, mishahara inakatwa kodi kubwa mno, huku ni kuwaonea watumishi wakati wapo wafanyabiashara wengine wanakwepa kodi ama kwa kushirikiana na *TRA* au wanatoa taarifa za uongo. Kodi kwa watumishi iangaliwe upya.

**MHE. ANNA MARYSTELLA MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nianze na suala la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Mheshimiwa Spika, kama mikakati ya Taasisi hii ilivyoelezwa, ikiwa ni pamoja na kuuelimisha Umma juu ya athari za rushwa kwa kulenga makundi maalumu ya Viongozi wa Dini, Viongozi wa Klabu za Wapinga Rushwa, Wasanii na Nyimbo, Ngonjera, Muziki na Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii imekuwa haifanyi kazi yake ipasavyo kutokana na upungufu uliopo; mfano, usafiri (magari) ya kufanyia kazi kwa ajili ya kuwazungukia Wananchi mara tu wanapohitajika kwa Wananchi. Mfano ni Wilayani Mpanda, yamewahi kutokea matatizo ya rushwa katika chaguzi za Serikali za Mitaa Vijijini, Wananchi wanatoa taarifa TAKUKURU, wanajibu kuwa hawana usafiri na wakati mwingine wanazima simu hawataki kupokea kabisa.

Mheshimiwa Spika, je, kwa hali hii tunaweza kutokomeza rushwa au tunailinda? Naiomba Serikali iboreshe Taasisi hii muhimu ambayo inatetea haki za Wananchi ipewe vyombo vya kutosha kufanyia kazi kama magari na mishahara mizuri kuepuka tamaa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni mzuri na wenye nia ya kuwasaidia Wananchi. Ninachopenda kusema ni kwamba, MKURABITA ni chombo ambacho kimepita

mkono wa kushoto kwa Wananchi, sababu Wananchi wengi hasa vijijini hawafahamu maana ya MKURABITA na faida zake. Naomba kuishauri Serikali iwaelimishe Wananchi kuhusu MKURABITA, kazi zake na faida zake.

Mheshimiwa Spika, niendelee na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF).* Mfuko huu ni mzuri, wenye lengo la kusimamia Miradi ya Maendeleo kama majengo ya madarasa pamoja na visima. Miradi mingi iliyoanzishwa na *TASAF* imesimama na kubakia vipolo; hivyo, naiomba Serikali isimamie Miradi yote ihakikishe imekamilishwa na hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia Bajeti ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa mwaka 2013/14, fedha maendeleo na matumizi ya kawaida ni Sh. 302,568,805,000 wakati Mfuko wa Bunge una jumla ya Sh. 123,401,059,000. Kwa ufahamu wangu, Baraza la Mawaziri ni dogo ukilinganisha na Bunge na pia shughuli za Bunge ni nyingi mno zinazowahusisha watu wengi. Sasa ilikuwaje Bajeti ya Sekretarieti ya Baraza ikawa kubwa karibu mara tatu ya Bajeti ya Mfuko wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, *TASAF* inaingia katika Awamu ya Tatu ya kuwa pamoja na Miradi mingine. Pia upo Mradi wa Uhawilishaji wa Fedha kwa haya mashauri; je, wahusika wamefanya tathmini ya mafanikio na changamoto ya Awamu ya Pili ya *TASAF?*

Mheshimiwa Spika, *TASAF* kwa maeneo ninayotoka haikufanya vizuri kwenye barabara, kinawekwa kifusi kwenye barabara bila ya kushindiliwa, matokeo yake inapokuja mvua ya masika kifusi chote kinachukuliwa na mvua.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kuku inayofanywa na *TASAF* imedhihirika kuwa kuku wanaonunuliwa kwa ajili ya vikundi huwa hawana ubora, matokeo yake Miradi yote ya Ufugaji wa Kuku imekuwa haina tija.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *TASAF* kwa upande wa Zanzibar, baadhi ya Wabunge hatuielewi vipi inavyofanyika. Nadhani watu sahihi pia nao kuelewa Miradi hiyo ni Wabunge ili waelewe inavyofanyika, mafanikio yake na changamoto zake. Itawawezesha Wabunge kuja kuchangia hapa Bungeni ili kutoa dosari ya Miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Wabunge kutoka Zanzibar tupatiwe orodha ya Miradi iliyofanyika na thamani yake katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta bajeti nzuri ya Wizara zote ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais, yaani Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Waziri wa Siasa, Mahusiano pamoja na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuiomba sana Serikali kuacha mtindo wa kukaimisha Idara kwa watendaji wenye Idara zao tayari. Vilevile kama mwenye Idara amestaafu au kufariki na kadhalika, ni vyema Serikali kujaza nafasi kwa kuteua wengine mapema.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la watumishi wapya kuchelewa kuajiriwa; mfano, wauguzi na walimu. Mara baada ya kuhitimu, ninaishauri Serikali iweke utaratibu wa kuajiri kila baada ya wahitimu kumaliza mafunzo vyuoni ili tusizalishe wezi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa, watendaji wetu ngazi mbalimbali katika Taasisi ya Usalama wa Taifa na TAKUKURU wanafanya kazi nzuri sana. Hivyo, ni vyema kila Mtanzania tukiwemo Wabunge, tunatakiwa kuwapongeza, kuwatia moyo na kuwaunga mkono ili kudumisha amani na usalama wa nchi yetu, yaani raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi nchini wanalia na Serikali kuhusu mishahara wanayopata kutokukidhi haja. Kwa maelezo yao wanasema kodi ya mapato kwa mishahara midogo kukatwa asilimia 14 ni kubwa sana. Tunashauri Serikali itazame uwezekano wa kupunguza na asilimia inayopunguzwa ipelekwe kwenye maliasili ya nchi yetu, ambayo Mungu aliijalia nchi yetu, ni nyingi sana mfano madini, gesi, utalii na kadhalika. Pamoja na kuwapunguzia watumishi riba kwenye mikopo mbalimbali kupitia mabenki.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro na Watumishi wa Serikali ni vyema walipwe madeni yao na tuache kuwakopa tunapowapa kazi au madai yoyote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumaliza mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii, Mungu awatangulie katika utekelezaji.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya. Naomba kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Katika ongezeko la mishahara, naishauri Serikali iweke mkazo katika kuwaongeza mishahara, iwe kipaumbele kwa kada za chini.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Utumishi ndiyo tatizo kubwa, wengi hawatimizi wajibu wao. Hawa ndiyo wanaoleta migogoro katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na Wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuliongoza Taifa letu kwa uadilifu na uzalendo uliotukuka. Aidha, niwapongeze sana Mawaziri wake wa Ofisi ya Rais, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa uhodari na uadilifu. Juhudi zao zimeonekana katika Hotuba

ya Bajeti ya 2013/2014, ambayo imetayarishwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Watendaji wa Ofisi ya Rais, wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi, kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na Hotuba ya Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Mfuko wa *TASAF* usaidie Halmashauri kugharamia ujenzi wa madaraja hususan katika maeneo ambayo Wananchi wamepoteza na wanaendelea kupoteza maisha kutokana na kukosekana kwa madaraja. Aidha, nyakati nyingine wanajeruhiwa au kuliwa na mamba. Mfano ni eneo la Gizgiz katika Mto Mbezi katika Kata ya Kivule. Eneo lingine ni eneo la Kisanga Stendi kuvuka kwende Kijiji cha Mbarangwe, Wananchi wanavuka kwa kutumia mtumbwi wa kienyeji, eneo hili mamba ni wengi na wanahatarisha maisha Wananchi kila siku.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Morogoro haina kabisa uwezo wa kifedha wa kujenga madaraja haya muhimu. Naomba msaada, Wananchi wanaangamia na maendeleo hayapo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kama inawezekana Ofisi za TAKUKURU zisiishie Wilayani bali ziteremke mpaka ngazi ya Kata ili iwe karibu na Wananchi hususan vijijini. Tafadhali, tutafute namna ya kuwahamasisha watoto waweze kujenga msingi wa Utawala Bora hususan waweze kuchukia rushwa. Nakipongeza sana Kitengo cha TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa ni Idara inayojitahidi sana kufanya kazi ya kuilinda nchi hii, ndiyo sababu tunatembea barabarani na tunalala usingizi. Utendaji wao mzuri unakuwa *reflected* kwenye hali ya amani ambayo imedumu siku zote hata kufikia Tanzania kuitwa Kisiwa cha Amani. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri na waendelee

kulitumikia Taifa hili kwa uzalendo. Napenda niwajulishe kwamba, kuna vijana wetu wengine wanatoroshwa na watu ambao hawatutakii mema na kuwapeleka kwenda kujiunga na Al-Shabaab. Mfano upo katika Tarafa ya Mkuyuni Morogoro, wameondoka kwenda kujiunga na kundi la Al-Shabaab, naomba Usalama wa Taifa watusaidie katika kukomesha tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba walimu waliopandishwa vyeo katika Wilaya ya Morogoro walipwe marupurupu yao, kwani wengine karibu wanastaafu kama Mwalimu Mbega wa Shule ya Msingi Kivuma katika Halmashauri ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja, naomba Daraja la Kisanga Stendi na la Gizgiz yagharamiwe na *TASAF.* Msaada huu utawapa matumaini Wananchi wa Morogoro pamoja na kuchochea maendeleo.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA**: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuchangia Hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, rushwa ni jambo ambalo limetia aibu na kuzorotesha maendeleo hasa ya watu wa kipato cha chini. Zipo Taasisi kama za Mahakama, Polisi, zimekuwepo kwa muda mrefu lakini ni Taasisi zinazoshughulika na ulinzi wa Wananchi na kutoa haki kwa Wananchi. Polisi wamelalamikiwa sana, lakini Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wamekuwa wakikaa maofisini wakisubiri matukio ya kuletewa na walalamikaji badala ya kwenda kutafuta ukweli wa malalamiko katika ofisi au maeneo ya kazi ya hao wanaolalamikiwa. Pia wafanyakazi wasio waaminifu katika Taasisi ya Takukuru hutumia vyeo vyao kuwatishia Wananchi na hatimaye kupokea rushwa. Wafanyakazi hawa ni vyema wakadhibitiwa ili kurudisha uaminifu wa chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, katika suala la Utumishi wa Umma, Serikali ina kazi kubwa ya kufanya ili kuleta ufanisi katika Sekta ya Utumishi wa Umma. Kumekuwepo na malalamiko kwa Watumishi kutoweza kutoa huduma nzuri katika maeneo yao

ya kazi. Watumishi kutokuwa na uwezo hata wa kutoa baadhi ya taarifa za msingi kwa Wananchi na hatimaye kuonekana kama wanapuuza Wananchi. Nashauri Serikali iwapatie elimu ya kutosha wafanyakazi wake na kuwataka kuwajibika ipasavyo wawapo katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitajika sana kufuatilia au kuweka utaratibu mzuri wa kuwafuatilia Watendaji wake katika Mitaa na Kata. Watendaji wanashindwa kuwajibika kwa visingizio kuwa wamekwenda Wilayani wakati wakiwa katika shughuli zao binafsi. Naishauri Serikali kuwa, kwa kuwa watendaji hawa ni muhimu sana kwa maendeleo ya Wananchi, wawajibike ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR**: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kuangalia upya mishahara ya watumishi na pia kuboresha namna ya malipo yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mpango wa Kupambana na Umaskini. Nashauri Mipango hii iingizwe Wilaya mpya na Jimbo la Nyang'hwale ili kuwanyanyua Wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TASAF* ijikite kutusaidia Wilaya mpya katika mipango yake ya 2013/2014 ili kuleta maendeleo haraka katika Wilaya mpya ya Nyang'hwale hasa elimu, afya, maji, miundombinu na kadhalika.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na Watendaji wake wote, kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 150,000 hadi 170,000, wakati huo huo imeridhia gharama za usafiri kuongezeka, gharama

za vyakula ziko juu, maisha ya Watanzania wa kawaida kwa ujumla ni magumu.

Mheshimiwa Spika, ni vigezo gani Serikali imetumia kuongeza kiasi hicho cha mshahara? Je, kwa kiwango hicho kidogo sana kilichoongezwa Serikali haioni kuwa hali ya maisha bado itaendelea kuwa ngumu?

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko ya upendeleo wa kupandishwa vyeo kwa watumishi katika sekta mbalimbali. Wapo wanaopandishwa cheo kila leo, akiongeza elimu kidogo akirudi tayari kapandishwa cheo. Wengine wamekaa miaka zaidi ya kumi, ni watendaji wazuri sana lakini hata nafasi ya kujiendeleza kwa masomo hawapewi ruhusa. Haya yanatokana na kujuana au kuwa karibu na mabosi wenye dhamana. Hali hii inakatisha tamaa sana na kuondoa moyo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa utaratibu mtumishi anatakiwa kuthibitishwa kazini muda gani tangu apate barua ya ajira? Kumekuwepo sintofahamu; wapo watumishi wamefanya kazi miaka miwili, wanapoomba nafasi ya kwenda kusoma wanaambiwa hawajathibitishwa kazini hivyo hawawezi kupewa ruhusa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maadili ya Utumishi ya Umma haiwajibiki kikamilifu kuhakiki mali za Watumishi kama sheria inavyotaka. Nina uhakika zaidi ya asilimai 80 ya mali za Watumishi hazijahakikiwa. Hili linasababisha Watumishi kujilimbikizia mali nyingi, hazijulikani zimepatikana vipi na Watanzania walio wengi ni maskini kabisa huku wachache wakichuma.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia Rushwa uwezo wake ni mdogo wa kiutendaji kwa sababu ya uwezo wa fedha na hata muundo wake.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kupambana na Rushwa iwekwe kwenye Katiba iwe ni Taasisi inayojitegemea (*autonomy),* iwe na uwezo wa kukamata, kushtaki na

kupeleka Mahakamani. Chombo hiki kipatiwe uwezo wa fedha na vitendea kazi waweze kufika kila eneo la nchi hii. Rushwa imeota mizizi huko chini kwenye ngazi na Halmashauri ya Wilaya, kwa kukosa Watumishi wa kutosha kwenye Taasisi hii, watu wanatoa na kuchukua rushwa peupe na mbaya zaidi katika maeneo ya kutoa huduma; kwa mfano, Hospitalini, Polisi, Mahakamani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa *PCCB* wachunguzwe kwani wapo wanaokula rushwa na hivyo kuondoa maana wa umakini wa chombo hiki muhimu sana. Rushwa inarudisha nyuma sana maendeleo ya nchi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako, mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi), kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2013/14 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti sana katika ustawi wa nchi yetu, kwa maana ni Idara ambazo zina mamlaka na wajibu wa kusimamia nidhamu, uadilifu na uwajibikaji kwa Umma. Kumezuka tabia ya ajabu sana kwa baadhi ya watu, vyombo vya habari na hata wanasiasa, kuzua taarifa za uongo kuhusisha Idara ya Usalama wa Taifa na TAKUKURU. Wanatumia muda mwingi sana katika kuchambua uwepo wa Idara hizi nyeti kwa Taifa letu. Huu ni ukiukwaji mkubwa sana wa maadili na Utawala Bora nchini. Kwa sasa, hili jambo litafutiwe suluhisho la kudumu, kwa kuangalia vyema huu uhuru uliovuka mipaka utatufikisha wapi. Haiwezekani kila mtu akaamua kufanya analotaka kwa wakati wowote. Hakuna nchi hata moja Duniani ambayo inaweza kuwa mfano unaowiana na hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kupambana na Rushwa ipewe uwezo wa kiutendaji, nyenzo na uwezo kisheria ili kuipa ufanisi zaidi. Sheria iliyopo sasa ni ya muda mrefu na haiendani na wakati. Huu ni wakati mwafaka kabisa kuanzisha mahakama ambayo itashughulika na masuala ya

rushwa kama ilivyo Sekta nyingine kama Ardhi, Viwanda na Biashara ili kurahisisha ufanisi na utendaji wa taasisi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maadili ya Viongozi itoe mafunzo ya kutosha kwa Watumishi na Maafisa wake ili isiwe kero kwa Watumishi wengine wa Umma. Mfano mzuri ni zoezi la uhakiki mali ambalo linafanyika bila ya kuzingatia muda wa wahusika ama ratiba zao wakati wa zoezi. Wahakikishe kuwa kila mmoja anapata haki anayostahili bila ya uonevu wala bughudha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alizungumzia sana namna hali ya uchumi ilivyo nchini pamoja na mtawanyiko wa watu. Hakika sina shaka na takwimu zilizotolewa ila nataka kuzungumzia namna ambavyo mgawanyo wa rasilimali na Pato la Taifa linavyochangia umaskini katika Mikoa yetu ya Kusini hususan Lindi, Mtwara na Ruvuma. Lini Serikali itasikia kilio chetu na kuweka jitihada za makusudi kuondoa hali mbaya ya kijamii na kiuchumi kwa Wananchi wa Mikoa hii ambayo kwa muda mrefu wamekuwa wasikivu na watiifu?

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15 kumekuwa na uendelezaji wa gesi ambayo imegundulika Mikoa ya Kusini. Naishauri Serikali iweke jitihada za makusudi kuainisha fursa za kiuchumi zilizopo katika Sekta hii, ikiwa ni pamoja na ajira, kilimo, ufugaji na uvuvi. Siyo jambo rahisi watu kutegemea kulipwa mishahara bila ya kufanya kazi. Wananchi wapewe elimu ya kutosha namna ambavyo wanaweza kushiriki kwa manufaa.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Tatu ya *TASAF* inalenga kuwawezesha Wananchi kiuchumi. Naishauri Serikali kuwa, *TASAF* isijitoe katika Miradi ambayo ilikwishaianza kuifadhili hadi pale itakapokamilika. Hii itasaidia sana kuokoa pesa za Umma na kuleta manufaa yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya kidini isiyo na tija wala taswira nzuri kwa nchi yetu sasa inaelekea kuota mizizi; hili ni jambo hatari sana kwa ustawi na usalama wa nchi yetu.

Serikali ilitazame hili kwa mtazamo mpana zaidi na kulipatia ufumbuzi suala la uchinjaji, naamini suluhisho pekee ni kuwa wote waruhusiwe kuchinja. Ila kwa Waislam ambao wana sharti katika uchinjaji, tuanzishe utaratibu kuwa kila sehemu itamke nyama halali au vinginevyo. Huu ni utaratibu mzuri kwa nchi nyingi Duniani, naamini itaondoa kabisa migongano isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ameonesha dhahiri kuwa Serikali ipo makini kuhakikisha matatizo ya ajira yanatatuliwa kwa haraka na kupatiwa ufumbuzi unaostahili. Ninaishauri Serikali iangalie kwa makini mfumo wa ajira uliopo kama kweli unaendana na wakati na unakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, madai ya malimbikizo ya mishahara, posho za uhamisho na stahiki nyinginezo kwa Watumishi wa Umma wa kada zote, imekuwa ni kero zisizo na majibu. Ukiangalia kwa makini mengine yanasababishwa na mfumo wa utunzaji kumbukumbu malipo na mara nyingine ni chuki baina ya Viongozi na Watumishi wengine mahali pa kazi. Lazima suala la mahusiano mema kazini lipewe nafasi kubwa kiutendaji ili kuleta tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mishahara iangaliwe jinsi gani ambavyo Watumishi walio katika maeneo ya vijijini na kufanya kazi katika mazingira magumu sana wanapewa posho maalum, kwa maana siyo sahihi kulipwa sawa na wale wa mijini. Watumishi wa vijijini wanafanya kazi kubwa mno kulingana na mazingira wanayofanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la ajira mpya, naishauri Serikali ili kukabiliana na tatizo hili sugu, iweke utaratibu wa kuwaajiri vijana katika maeneo ya kazi kwa kuwalipa posho ili kuwajengea uzoefu wa kazi lakini pia kuondoa hali ya kukaa vijiweni hadi pale ambapo watafanikiwa kupata ajira zao za kudumu. Mfumo huu unatumika sehemu nyingi Duniani hivyo siyo dhambi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mishahara hewa bado linaendelea kuwepo licha ya jitihada zinazofanyika. Naishauri Serikali kutumia mfumo wa ki-eletroniki na *bio-technology* ili kudhibiti na kuhifadhi taarifa mbalimbali za watumishi. Hii itasaidia sana kuondoa udanganyifu uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, muda wa kufanya kazi lazima uzingatiwe kwa sababu Watumishi wanatumia muda mwingi kufanya shughuli ambazo haziwiani wala kuendana na majukumu wanayopewa kila siku.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, kwa namna ambavyo imekuwa ikifanya kazi, inaonesha dhahiri utendaji wake hauna tija, mara nyingi imekuwa ikitoa matangazo ya kazi kwenye vyombo vya habari hususan magazeti lakini hakuna mrejesho kwa wale ambao aidha hawajaingia kwenye usaili au wameingia kwenye usaili lakini hawapati mrejesho wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao watakuwa wamepata nafasi pia ni tatizo kwani wanapopelekwa kwenye maeneo ambayo hawana mazoea nayo, huenda tu kuripoti na kurejea maeneo wanakotokea . Hiyo ni dalili ya ufujaji wa pesa na pia rasilimali watu, kwani wengi wao wanakuwa hawarudi kwenye fani hizo huamua kufanya shughuli nyinginezo waweze kujipatia mlo wao wa kila siku.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Sekretarieti hii ikavunjwa ili nafasi za ajira zirudishwe kwenye Wizara husika kwa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingi za *TASAF* zinafanyika bila ushiriki wa Wananchi na pia zimekuwa zikigawanywa kutokana na maeneo; kwa mfano, miradi ya

kaya zenye uhaba wa chakula; kwa nini ni baadhi ya Mikoa na Wilaya na si nchi nzima? Serikali inasema nini kuhusu hili?

Mheshimiwa Spika, madai ya walimu ni vyema Serikali ikachukua hatua za dharura ili kunusuru hali hii kwani imekuwa ni kero ya muda mrefu. Kwa nini mpaka sasa walimu wapatao 11,626 hawajalipwa? Serikali inasemaje kuhusu hili?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, naomba kujua jinsi ambavyo mimi Mbunge naweza ku-*access* (kushirikiana) au kupata njia ambayo Wananchi wangu wa Jimbo la Bahi wataweza kupata fursa ya kupata huduma ya mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kupata mafunzo ya kibiashara na ushauri wa kuboresha biashara zao kutoka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, nitafurahi sana kama nitapata maelekezo yatakayoniwezesha kushirikiana na Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, nakutakia kazi njema. Ahsante.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, natambua Ofisi ya Rais, Utawala Bora, inafanya kazi kubwa ya kusimamia nchi yetu iwe na Utawala Bora na wenye amani.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika kufanya utaratibu wa kuwachunguza wale wote wanaochangia mifarakano ya kidini wachukuliwe hatua kali sana, vinginevyo, wataliweka Taifa letu pabaya.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Utumishi wa Umma iangalie utaratibu wa ajira na kurudisha katika Halmashauri husika. Kwa mfano, Afisa Mtendaji wa Mtaa wa Dar es Salaam anachaguliwa na Tume ya Ajira toka Kagera. Afisa huyo anatumia gharama kubwa sana wakati wa likizo na mabadiliko ya mazingira toka mkoa hadi mkoa mara nyingi waajiriwa wa aina hiyo hushindwa kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, mshahara na marupurupu ya Wafanyakazi wa Serikali na hasa kada za chini iangaliwe kulingana na gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ipewe meno na itengewe Bajeti ya kutosha waweze kufanya kazi yao vizuri kwani wanaonekana wapo wapo tu hawana nyenzo yoyote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Celina Kombani, yeye binafsi, Waziri wa Nchi Mheshimiwa Wasira, Katibu Mkuu Yambesi, Naibu Katibu Mkuu Mkwizu, Wakurugenzi wote na Wataalam alionao, kwa kazi kubwa wanayofanya katika mazingira magumu ya kifedha na changamoto nyingi zinazofuatana nazo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawapongeza kwa Hotuba nzuri lakini nina yafuatayo ya kusema:-

(i) Je, ili kuweza ku-*support* ya mikopo kwa Wajasiriamali wadogo na mafunzo stahiki, tufanyeje? Utaratibu wa *PTF* ukoje?

(ii) Kumekuwa na malalamiko mengi ya TAKUKURU, lakini tujiulize TAKUKURU wamewezeshwa kuwa na meno ya kuchunguza na kushtaki. Kama kweli tunayo dhamira ya haki kupambana na tatizo hili na pengine kulifuta kabisa kama ilivyo katika nchi nyingine kwa mfano Rwanda, hebu tudhamirie kwa nguvu tuwape mamlaka hayo.

Mheshimiwa Spika, wazo la kuhudumia Viongozi Wastaafu ni jambo la busara sana, ila naona sasa ni vyema tukaliangalia upya. Awali Viongozi Wastaafu wenye stahili hiyo walikuwa wachache, lakini hivi sasa ni wengi mno na kuwahudumia kifedha, kwa kuzingatia rasilimali fedha chache tulizonazo, ni vyema tukaliangalia upya. Kwa mfano, ushauri mmoja unaweza kuwa kama ifuatavyo:-

Anapostaafu Kiongozi mwenye stahili hiyo, apewe huduma hiyo kwa miaka miwili kwa sababu za kiusalama, baada ya hapo apewe *lumpsome* kama Shilingi bilioni moja, ajihudumie usafiri, walinzi na kadhalika. Pia wanapozidi kuzeeka gharama ya matibabu inakuwa kubwa zaidi, huku wanaongoza na misafara mikubwa ambayo ukiangalia ni bajeti kubwa mno. Hili naomba lirekebishwe. Hizo fedha chache zitoe huduma kwa Wananchi katika masuala muhimu ya elimu, afya na kadhalika. Tufanye maamuzi magumu kutekeleza hili.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Sekretarieti ya Ajira kwa kazi nzuri wanayofanya, pamoja na kwamba ni vigumu sana kufanya kazi ambayo mara nyingine haina matokeo ya mwisho. Kwa mfano, Sekretarieti ilifanya usaili wa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi, lakini hakuna fedha ya kuwaajiri ilihali mahitaji ya wataalamu hao ni makubwa mno na athari kwa Wananchi ni kubwa; hivyo, kuongeza kero nyingi mno. Naomba basi kwa vile kazi zinachujwa huku, watu wenye sifa wako mtaani tuwawezeshe kufanya kazi yenye tija au la Bwana Daudi atakuwa anafanya *business as usual, no value for money*.

Mheshimiwa Spika, ajira ni jambo la kusikitisha na lisiloelezeka, kwani kabla ya Uchaguzi 2010 tulianzisha Vijiji na Kata, lakini hadi leo tunapoelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani, Watendaji wa Vijiji kwenye Wilaya nyingi hawapo. Tunashindwa hata kukusanya mapato kwa ukamilifu kwani Serikali huko chini hakuna. Tusingoje uchaguzi ndiyo tuanze kutafuta Watendaji. Kwa mfano, Kilindi tuna Vijiji 102, Watendaji 52 na maeneo mengi hali ni tete kabisa. Naomba hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Usalama hasa Mawilayani waliokaa muda mrefu na kufanya mazoea, wafanyiwe tathmini za mara kwa mara kuhakikisha maadili yanaendelea kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri, namwomba anisaidie nipate Afisa

Utumishi (Mkuu wa Idara), mwenye sifa na uwezo kwani pamoja naambiwa TAMISEMI ndiyo wanaopanga, anisaidie kwani nimechoka kufanya kazi za Utumishi. Kwa mfano, Afisa Utumishi aliyetoka Morogoro aliyeletwa kwangu amechoka sana. Nakushukuru.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia tatizo la Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Nimekuwa napokea malalamiko ya Wananchi maeneo ya Mvomero, Turiani na Kange kuhusu kutopatiwa mikopo huku dhamana zao zikiwa tayari mikononi mwa Watendaji wa Mfuko huu. Wananchi waliokwishatoa dhamana zao wamekuwa wakifuatilia mikopo au fedha za dhamana zao pasipo mafanikio. Naomba kauli ya Serikali juu ya tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu kupitia Mfuko wa Jimbo tumeanza kujenga masoko katika Vijiji vya Luale, Mlali, Kibati, Dakawa na Mvomero, kwa lengo la kuchochea kukua kwa uchumi. Naomba Serikali kupitia *TASAF* isaidie fedha za kukamilisha masoko haya. Maeneo ninayoombea fedha ni baadhi yaliyo pembezoni na mengine yamekuwa na idadi kubwa ya watu na kuna hitaji la kujengwa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mvomero kuna uhaba mkubwa wa Watumishi wa Idara ya Afya na kupelekea baadhi ya Zahanati kushindwa kufunguliwa na baadhi ya Zahanati kutoa huduma hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali itupatie Watumishi wa kutosha katika Idara ya Afya. Zahanati zifuatazo zimeshindwa kufunguliwa Vijiji vya Maguruwe, Lusungi, Diburuma Vikenge na sehemu zingine watumishi hawatoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la Watendaji wa Vijiji na Kata kukaimu kwa muda mrefu bila kuajiriwa. Wapo Watendaji wa Vijiji na Kata wanafanya kazi kwa kujitolea kwa muda mrefu, naomba Watendaji hao waajiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni watumishi kutopandishwa madaraja ikiwemo Walimu. Kuna malalamiko ya Watumishi kukaa kwa muda mrefu bila kupandishwa madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Spika, tumesema kwa maelekezo yako na taratibu zetu tusitoe shukrani, lakini kwa mtu ambaye ulikuwa unachungulia kaburi, huwezi hata kwa taratibu zote ukashindwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

**SPIKA:** Nakuruhusu wewe tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Namshukuru Mwenyezi Mungu, kwamba, naweza kusimama mbele yenu Waheshimiwa Wabunge, nikaweza kuzungumza machache. Nawashukuru nanyi kwa dua na maombi ambayo kwa hakika Mwenyezi Mungu ameyasikia, naweza leo nikasimama mbele yenu. Jimboni wamenivumilia sana, sikuwepo kwa miaka miwili, lakini mambo yameendelea hata ambapo sikuwepo, lakini nawashukuru kwa uvumilivu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, utajibu kwa dakika kumi na tano, zingine unachukua za Waziri wa Nchi anayefuata, yeye atakuwa na dakika 55.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Sasa sina mengi kwa sababu katika kipindi cha miaka miwili, nilishindwa kufuatilia yaliyokuwa yakiendelea pamoja kwamba, nilikuwa naweza mara moja au mara mbili, kufuatilia yale ambayo yalikuwa yakizungumzwa Bungeni; lakini kwa hizi siku mbili ambazo nimekuwepo, naomba nizungumze yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hasa hili la udini, kwa masikitiko makubwa tunalizungumza, kwa kweli ni kitu ambacho sisi Watanzania ni kigeni. Mara chache sana unakutana na mtu

unamwuliza kitu cha kwanza wewe dini gani; hatujawahi hata kutokana na jina tu, marafiki zetu, ndugu zetu, majirani zetu wote ni Watanzania tu, ni rafiki na ndugu. Nadhani hili litaendelea tu, hili linalopita ni shetani anataka kuivuruga nchi, lakini nchi itakuwa imara.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa upande wa Mheshimiwa Rais, jana limezungumzwa mimi nimeshangaa sana. Kwa mara ya kwanza, leo asubuhi nikasema ngoja na mimi baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Mbunge wa Tabora, mimi ni mgeni sana pale Ikulu, wamenipokea bila kujua ni nani ana dini gani, wote walinipokea vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, sasa na mimi kwa mara ya kwanza ndiyo naanza kuangalia huyu wanayemsema Mheshimiwa Rais ni mdini; nikasema hebu ngoja Mawaziri wote wa nchi wa Ikulu tunaomsaidia pale wote wanne ni Wakristo hakuna Mwislamu hata mmoja. Makatibu Wakuu wa Ikulu kuanzia Katibu Mkuu Kiongozi wote ni Wakristo. Sasa sijui huo udini umetoka wapi? Katibu wa Rais, ambaye ni mtu wa karibu sana ni Mkristo. Wakurugenzi pale Ikulu, Wakurugenzi wa Huduma, Mkurugenzi wa Mawasiliano wote ni Wakristo. Huyu mtu ambaye nimefanya naye kazi kwa miaka 26 mpaka sasa, kuanzia mwaka 1987, siyo huyo wanayemzungumzia nafikiri ni mtu mwingine. Kwa hiyo, nadhani hili tuliachie hapo.

La pili, ni kuhusu Usalama wa Taifa; imenishangaza sana kwamba, wenzetu ni wataalam sana wa masuala ya Usalama wa Taifa ama wamo katika hiyo Idara, maana wanazungumza kama vile siku zote wanaifanya hiyo kazi. Ajabu sana, maana mambo haya ni ya siri. Mambo ya Usalama wa Taifa ni ya siri, lakini wanayazungumza kama vile ni marafiki, ni ndugu au wanapata taarifa kila siku za Usalama wa Taifa; hiyo si kweli. Usalama wa Taifa haufanyi kazi namna hiyo; haiwezekani sisi tukawa wataalam wa masuala ya Usalama wa Taifa. Sasa Duniani taasisi hizi zipo na ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia usalama wa nchi, hivi tulivyo sasa umoja wetu hapa tulipofika na heshima

tuliyopata, inatokana kwa kiwango kikubwa na kazi kubwa iliyofanywa na vyombo vyetu vya usalama na ulinzi na lazima tuviheshimu. Hawa ni mashujaa ambao hatuwafahamu lakini wapo, hatuwapi hata sifa wanafanya mambo makubwa sana. Yaani ni hawa tunaowaita *unsigned heroes*, leo tunakuja kuwazungumzia hapa kwamba, wanatoa vidole vya watu, huo siyo Usalama wa Taifa hata kidogo. Mimi naweza kusema labda ni porojo tu. Hayo mambo kama yanafanyika basi ni uhalifu, uhalifu siyo usalama. Kila mtu sasa anakuwa mtaalam wa masuala haya.

Mheshimiwa Spika, duniani pote masuala ya ulinzi na usalama hayazungumzwi hadharani kama tunavyotaka kuanza utamaduni huo. Kama ni kweli yapo, basi Bunge lina Kamati yake ambayo inaweza ikalizungumza kwa undani, inaweza kuwaita watu hawa wakawaeleza, lakini kuja kuyazungumzia hapa hadharani!

Mheshimiwa Spika, siku moja nilimsikiliza Mheshimiwa Anne Malecela, nakumbuka alisema, hata maskini na nyumba yake ya tembe huwa wakati mwingine mlango anaufunga, ndiyo masuala ya ulinzi hayo, siyo kwamba utakuja kuyazungumzia hadharani, Dunia nzima ijue kwamba Tanzania tupo namna hiyo, haiwezekani hata siku moja. Kwa hiyo, naomba sana tuzingatie hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Marekani tunajua ustaarabu wao, kuna masuala ya *CIA, FBI,* kuna Kamati za Ulinzi na Usalama katika *Senate*, kuna Kamati za Ulinzi na Usalama katika Baraza la Wawakilishi, huko ndiko yanakwenda kuzungumziwa na mambo ambayo ni ya siri hayatatoka hata siku moja. Sasa leo tunataka tuliibue suala la ulinzi na usalama tulizungumze hapa, haiwezekani. Utamaduni wetu umekuwa hivyo, masuala ya Jeshi, tutayazungumzia masuala ya nyumba, masuala ya mishahara na masuala ya nini, hatuwezi kuzungumza mambo ya ndani ya ulinzi ya Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo hatuwezi kuzungumzia masuala ya ulinzi na usalama, kwa maana ya Idara yetu ya

Usalama wa Taifa. Naomba kama taratibu haziruhusu au taratibu zetu tuziangalie upya ili tusijielekeze huko, tusirudie haya yaliyotokea jana kwa ndugu zetu hapa. Nendeni popote pale mtaangalia Marekani, Uingereza kuna MI6, MI5, Bunge litazungumza masuala yake kwenye Kamat tena kwa siri. Nendeni Israel, mtakuta Shing Belt, mtakuta Mosad, Bunge litazungumza masuala haya kwa siri katika Kamati zake siyo hadharani. Kwa hiyo, tuangalie Kanuni zetu, ndiyo ombi langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, nimesikitika sana kwamba, suala kubwa la mipango halijazungumzwa, ndiyo maendeleo ya nchi hayo. Labda Mheshimiwa Waziri Wasira atalizungumzia zaidi, lakini kwa maana ya undani, hotuba hazijalizungumzia, kama wapo ni wachache labda wameandika, lakini tuliokaa hapa ilikuwa ni vurugu tu. Sasa mambo ya maendeleo, mambo ya msingi, hayazungumzwi na Bunge hili na Hotuba ya Waziri anayeshughulikia Mipango haijazungumza kabisa. Mambo ya ajabu kabisa haya!

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Rais wa Kenya, ametoa mambo tisa ambayo yataivusha Kenya kutoka hapo ilipo kuruka kimaendeleo. Nilidhani wenzangu vilevile wangesema aaha jamani kuna mambo haya na sisi tuyaige, lakini hakuna mtu yeyote aliyezungumzia. Nashauri kwa sababu ni majirani zetu, twende tukaisome hiyo Hotuba ya Rais Kenyetta, alipokuwa anafungua Bunge siku mbili zilizopita, ni muhimu sana.

Juzi niliombwa kuzindua Kitabu, siyo cha kwangu ni cha Wataalam wa Afrika ya Kusini. Sasa nilipokuwa nafanya *research* katika kuandika ile hotuba yangu nikasema aah nilizungumza mambo mengi ambayo yalikuwa yanasikitisha kwa maana ya maendeleo ya Afrika. Nikawaambia pamoja na yote haya, wenzetu sasa lazima tutembee kifua mbele kwa sababu wanatuona vinginevyo. Wanasema katika Mataifa 20 Duniani, kwa vigezo vya Benki ya Dunia, Mataifa 20 Duniani ndiyo ambayo yatapiga hatua kubwa kimaendeleo Duniani, Mataifa 11 yapo katika Afrika ya Kusini mwa Sahara na Tanzania ni mojawapo. Kama hiyo haitoshi,

*IMF* kwa vigezo vyake inasema katika Mataifa kumi ambayo yatapiga hatua kati ya mwaka 2011- 2015, saba yapo Afrika, Tanzania ni mojawapo. Ukiangalia mazungumzo yote tuliyokuwa tunazungumza hapa, utafikiri sisi ndiyo basi, ndiyo watu wa ajabu wa mwisho kabisa, kumbe sivyo. Tutembee kifua mbele, tusipotembea sisi kifua mbele na kujivuna, hakuna mtu atakayetembea kifua mbele kwa niaba yetu.

Kwa kumalizia sasa kuhusu hili la maendeleo, mchango wangu ni kidogo tu. Ni kwamba, moja ya kigezo cha maendeleo ni jinsi nchi inavyokuwa na waandishi wa vitabu wengi, pale ambapo kuna waandishi wa vitabu wengi ndipo maendeleo yalipo, ni moja ya kigezo. Mimi wakiniuliza sasa mchango wako ni upi, nitasema basi niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba, juzi Mheshimiwa Makamu wa Rais, alizindua kitabu ambacho nimeandika pamoja na kuwa na udhaifu wa afya na ugonjwa, lakini nimekitoa kinaitwa Udhibiti wa Huduma za Kiuchumi Tanzania; hiki hapa. Ndiyo mchango wangu na mimi. Kitasambazwa na mchapishaji hivi karibuni. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hili.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine la mwisho katika suala hili la maendeleo, suala la maji lizungumziwa sana. Mchango wangu ni mdogo tu, nakumbuka Mzee Sabodo, alitoa visima kama 200 kwa Chama ambacho jina lake nalihifadhi, kile Chama kikapeleka visima vyote hivyo kwa maeneo ambayo ni ya Chama hicho hicho. Sikusikia wakigawa kwa nchi nzima na walisema hivyo visima vinagawiwa kwa Chama hicho. Sasa nasema, nina visima 100 nimepewa na Mzee Sabodo na mimi nitavitoa kwa nchi nzima, pamoja na maeneo ya sehemu za Upinzani; na nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Katibu Mkuu wake, waratibu maana mimi siko huko siku hizi na sina uwezo wa kuratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mtoa hoja wa kwanza, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, dakika 55.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa muda huu. Naomba tu nianze na machache ya utangulizi.

Mheshimiwa Spika, una kipindi chako kizuri sana cha *Briefing* hapa Bungeni. Kipindi cha *Briefing* kilichofanyika safari hii Wabunge tuliwekana vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, tulielezana kabisa kwa waliokuwepo, maana yake wengine wamekuja juzi. Lakini waliokuwepo kwenye *Briefing* watu tulisema kwamba tutaheshimu Kiti, tukamwambia Spika kwamba wewe ni mama na maneno mengi tu.

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka Mheshimiwa Leticia Nyerere aliongea kwa uchungu sana kumtetea Spika na wengine wengi kwamba sasa hivi tunakwenda kwenye Bunge la kiustaraabu.

Mheshimiwa Spika, lakini yale yote ya *Briefing* naona yameishia kule kule *under camera,* hapa tumerudia yale yale. Kwa kweli mimi nasikitika sana, tena sana kwamba yale ambayo tumekubaliana yakija hapa hatufanyi yale. Naomba nitoe ushauri kwamba kipindi cha *Briefing* Wabunge wetu wote tuwepo kwa sababu ukiangalia wale wanaotoa matusi na nini ni wale ambao hawakuhudhuria kile kipindi cha *Briefing* kama kweli mna-*note.*

Mheshimiwa Spika, la masikitiko lingine, jamani sisi wenzenu upande wa pili, sisi Mawaziri ni binadamu kama nyinyi. Mnapotutukana kwamba Serikali hii ni *impotent* ina maana kwamba hatufanyi kazi. Lakini mwenye macho haambiwi tazama. Hivi barabara zinaweza zikajengwa na mtu *impotent?* Hivi visima vinaweza vikajengwa na mtu ambaye ni *impotent?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hili neno lenyewe wala usilitumie, linatia aibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI:** Ndiyo Mheshimiwa Spika! Kwa kweli wametutukana na sisi tuna nyongo. Tukiamua kurudisha kwa kweli haitakuwa ustarabu. Kwa hiyo, tunaomba sana tuwe tunaheshimiana katika Bunge hili badala ya kutukanana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya watumishi. Maslahi ya watumishi kwa kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi sana kuongeza maslahi ya watumishi. Tusiangalie tu kwamba maslahi ya watumishi ni mshahara tu. Maslahi ya watumishi ni pamoja na mazingira mazuri pamoja na kulegeza masharti mbalimbali, pamoja na mshahara, pamoja na motisha za aina mbalimbali.

Kwa hiyo, Serikali ndiyo maana imeanzisha ile Bodi ya Mishahara na Motisha ili kuhakikisha kwamba tunaboresha mishahara ya watumishi na ndiyo maana kila mwaka tunaongeza mishahara ya watumishi. Mshahara wa mtumishi huwezi kuutangaza hadharani, ni kinyume na sheria na ni siri ya mtumishi. Ndiyo maana hata sisi Wabunge, Wahariri wakiandika kwenye magazeti kwamba mshahara wetu ni kiasi fulani, tunakasirika. Kwa hiyo, mshahara wa mtu ni siri.

Kwa hiyo, kima cha chini cha mshahara msinilazimishe kutangaza hapa. Ila tunachosema ni kwamba kila mwaka tutahakikisha kwamba tunaongeza au tunaboresha mishahara ya watumishi.

Maslahi mengine kwa watumishi, Serikali inajenga nyumba za watumishi katika sehemu mbalimbali. Tusiwe na ubaguzi kusema kwamba ni Walimu tu wanatakiwa kujengewa nyumba. Kule kwenye Kata wapo Maafisa Ugani, Manesi, Madaktari, Walimu, kwa hiyo, tusibague kundi fulani. Tuangalie makundi yote kwa ujumla, wote. Wafanyakazi wote wana faida yake. Kila mfanyakazi ana kazi yake, kila mfanyakazi ana faida yake, kila mfanyakazi ana *profession* yake na ana mahitaji sawa na mtumishi mwingine yeyote. Hata mhudumu hapa asipofanya kazi kwenye vyoo vyetu pale tunapiga kelele. Kwa hiyo, na yeye mhudumu ni muhimu.

Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaangalia mishahara ya watumishi wote kwa ujumla kwanza, badala ya kunyofoa kada moja moja. Hicho ndicho tunachofanya cha kwanza kuhakikisha kwamba tunainua kwanza mshahara wa watumishi wote baadaye tutaangalia hizo kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imetoa motisha kwa wafanyakazi. Sasa hivi tumeruhusu wafanyakazi kukopa katika Mabenki mbalimbali. Ni mwajiri anamwekea sahihi tu asubuhi, jioni anapata mkopo. Hiyo ni motisha tosha. Tumejenga nyumba, tumepeleka miradi mbalimbali vijijini kuboresha mazingira ya huko vijijini.

Kwa hiyo, suala la motisha kwa wafanyakazi kwa kweli kwa upande wa Serikali tunalifanyia kazi kubwa sana. Naomba Waheshimiwa Wabunge tusiwaone watumishi wa Serikali kwamba tunawaonea, tunawasikiliza matatizo yao, tunayasikiliza maombi yenu na ushauri wenu tunaufanyia kazi na tunaufanyia kazi kwa awamu, siyo tunaufanyia kazi mara moja. Lakini tunafanya kwa awamu na baadaye kuhakikisha kwamba mishahara inakuwa mizuri na maslahi ya wafanyakazi yanaboreshwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hilo linaendana na wajibu. Alisema Mheshimiwa Haroub Shamsi, Mbunge wa *CUF*. Alisema uwajibikaji nao ni mbovu Serikalini. Rasilimaliwatu zinatumika vibaya, rasilimali fedha zinatumika vibaya, rasilimali vitu zinatumika vibaya. Kwa mfano, magari ya Serikali kubeba mikaa ni nje ya utaratibu. Unamhudumia mteja wewe mfanyakazi unasikiliza simu mteja yuko pale, humsikilizi, nayo ni kinyume cha sheria.

Kwa hiyo, tunapodai mishahara na maslahi, tuhakikishe kwamba na sisi wafanyakazi tunatimiza wajibu wetu, tunawahudumia wananchi ipasavyo. Siyo mgonjwa anakwenda hospitali, Nesi anasikiliza simu, huo siyo uwajibikaji. Dereva anachukua gari la Serikali anabebea mkaa, huo siyo uwajibikaji. Tutumie rasilimali vitu na rasilimali watu kwa manufaa ya Watanzania na siyo kwa manufaa ya watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye upande wa majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Mnyika yeye alisema kuhusu malimbikizo ya mishahara. Kwenye taarifa yangu nimetoa taarifa kwamba hadi tarehe 31 Machi, 2013 jumla ya wafanyakazi 11,820 walikwishalipwa kiasi cha Shilingi bilioni 12.6 na kati ya hao 7,400 walikuwa Walimu, kada ya Afya walikuwa 1,117 na watumishi wengine 3,293. Nikasema kwamba madai mengine yameshahakikiwa na *breakdown* nitampatia Mheshimiwa Mnyika na Waheshimiwa ambao wanahitaji na zile ambazo hazijahakikiwa ziko kwenye laini ya kuhakikiwa.

Kwa hiyo, yale madai yanayohusu malimbikizo mnayoyaona sasa hivi kama nilivyojibu asubuhi, ni yale ya nyuma ambayo yalikuwa hayajaingizwa kwenye mfumo, yale ambayo tulikuwa tunafanya *manual* kabla ya mfumo huu wa *LAWSON 9,* yaani *Human Capital Management Information System,* Wajumbe wa Katiba na Sheria walifika pale Utumishi waliona ule mfumo unavyofanya kazi.

Kwa hiyo, hayo malimbikizo tunayoyasema sasa hivi ni yale ya nyuma ambayo hatujaingiza kwenye mfumo. Mimi nasema kwamba baada ya muda, malimbikizo ya mishahara yatakuwa historia kwa sababu yatakuwa yanaingizwa kwenye mfumo moja kwa moja. Naomba tuvute subira kidogo tu ili mfumo huu uweze kukamilika kutoka Utumishi; Utumishi, Hazina; Hazina wao wanalipa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tumelifanyia kazi kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, mfumo huo unafanyaje kazi? Ni kwamba waajiri kule waliko nilisema kwenye hotuba yangu, tumewafundisha Maafisa Utumishi karibuni 1,047 wana-*feed* hizi taarifa za wafanyakazi wanaporipoti tu kwenye mfumo na sisi tunazipata kule Utumishi. Tukishazipata *payroll* tunai-*process* kwa siku tisa tarehe 1 mpaka tarehe 9 baada ya hapo tunapeleka Hazina wenzetu wana-*process* mshahara unatoka. Kwa hiyo, hiyo *process* kwa kweli imeleta mafanikio makubwa sana.

Kwa hiyo, huo mfumo unafanya nini? Unatoa taarifa ya Utumishi ya ajira mpya kuingizwa kwenye mfumo pale pale na mwajiri. Akifika, akiripoti, mwajiri anachukua taarifa zake anaziingiza kwenye mfumo, sisi kule Utumishi tunazikuta.

Pili, ule uhamisho ambao hauna msingi, sisi tumeshazuia na tumeanzisha *leave roster* ili kupunguza hayo madeni ya likizo. Pia kuna mpango maalum wa bayana wa mafunzo ili kuepuka madeni yatokanayo na mafunzo. Kuna *training programme* ambazo zinatengenezwa ili watu waende wakati kuna fedha, tusiende kiholelaholela. Changamoto iliyopo ni ufinyu wa bajeti inayotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo malipo ya likizo, matibabu, mafunzo na kadhalika. Lakini hayo sisi kama Serikali sasa hivi tunayafanyia kazi ili tuone namna bora ya kuhakikisha kwamba tunawalipa watumishi kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, upande wa Kambi ya Upinzani walimtaja mtumishi mmoja anaitwa Emmanuel Gwalanji Afisa Mifugo, wamesema kwamba yeye amefukuzwa kwa sababu za kisiasa. Mimi nasema kwamba Watumishi wa Umma badala ya kwenda kulalamika kwenye vyombo vya siasa, pale Utumishi ndipo tunaposhughulikia malalamiko ya watumishi kupitia Tume ya Utumishi wa Umma. Kama una rufaa yako peleka pale itasikilizwa itafanyiwa kazi. Ukija humu ukisema kwamba uingize kwenye siasa, unaonekana kweli wewe ulikuwa unafanya mambo ya kisiasa.

Kwa hiyo, namwomba huyo mtumishi Emmanuel Gwalanji, akate rufaa kwenye Tume ya Utumishi wa Umma kama anaona kwamba ameonewa, asiendelee kufanya siasa. Niwaase Watumishi wa Umma, kama wanataka siasa asilimia mia moja, waje upande huu kama sisi tuliotoka makazini, tumekuja kugombea Udiwani, Ubunge badala ya kukaa kule, kuwahudumia wananchi, wewe unapiga siasa kwa saa za kazi. Hairuhusiwi, siasa zipigwe baada ya saa za kazi na siku ambazo siyo za kazi. Hatuwakatazi, sheria haiwakatazi. Lakini kama wewe kila siku kazi yako ni kupiga siasa ofisini, kwa kweli tutakuchukulia hatua za kinidhamu na nasema kwamba waajiri wote waangalie wale wanaopiga

propaganda za kisiasa wakati wa kazi na saa za kazi wawachukulie hatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa mwenzangu Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, namheshimu ni Waziri mwenzangu kivuli, lakini Watanzania wamemwona ndugu yangu hapa akibabaika hata kusoma ile hotuba yenyewe. Ina maana kwamba ile hotuba Profesa kama kweli ameiandika mwenyewe, asingeshindwa kusoma hapa. Mimi nasema kwamba kwa kweli inaaibisha kwa Maprofessa wengine wote, yaani ni mfano mbaya kwa Profesa kuja hapa na kushindwa kusoma hotuba yake ya Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, naomba nijibu masuala yake kama ifuatavyo kwa sababu nimeisoma ile hotuba yake.

Mafanikio ya upimaji wa utendaji kazi. Ule mfumo wa *OPRAS* unafanya kazi, watendaji wanapimwa kwa uwazi, una upungufu, lakini sisi kama Serikali kwa mwaka huu tunaangalia ule upungufu yaani tunaufanyia *review* ili kuuboresha zaidi. Mafanikio yapo baadhi ya sehemu za kazi wanafanya vizuri, lakini baadhi ya Taasisi hawafanyi vizuri. Tumetoa agizo kwamba mtumishi yeyote ambaye hakujaza zile fomu za *OPRAS* sisi tutahakikisha kwamba kwenye mtandao haingii. Kwa hiyo, hata upande wa Walimu tumewatengenezea fomu ya peke yao kama walivyoomba. Kwa hiyo, naomba Walimu nao wajaze fomu za *OPRAS* ili kuimarisha utendaji kazini.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kwamba mara zote Walimu kupitia Chama chao wanalalamikia maslahi yao na mara nyingi Serikali inakimbia Mahakamani kwenda kuwashtaki wanapoona kuna mgomo. Ninachosema ni kwamba Serikali inashtakiwa na ina uwezo wa kushtaki. Kwa hiyo, kama wanaona mambo hayaendi vizuri, msuluhishi ni Mahakama na siyo chombo kingine chochote kile, ndiyo chombo kinachotoa haki. Kwa hiyo, Serikali ilivyokwenda Mahakamani haikutenda dhambi yoyote na wala haikukiuka taratibu zozote kwa sababu inaweza kushtaki na inaweza kushtakiwa.

Kwa hiyo, tulikwenda Mahakamani, kesi ile ilisikilizwa na *ruling* yake naomba kunukuu: "*All parties have expressed the need to return to negotiation, then parties should make deliberates effort to reach un-amicable settlement by even inviting persons who are good in labour law and relation to assist them.*" Nimenakili tu hicho kipengele. Kwa hiyo, majadiliano kati ya Chama cha Walimu na Serikali yanaendelea ingawa wenzetu kwa upande mwingine walikata rufaa, lakini kulikuwa na kikao Desemba, 2012 na Machi, 2013. Kwa hiyo, jamani tunaendelea, tunajadiliana na tutafikia muafaka tu, Serikali haina mgogoro wowote na Walimu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Kamati ya Bunge ya Kudumu. Serikali ichukue hatua za haraka kuwabaini watumishi hewa na kufuatilia watumishi wale wote ambao hawakuwajibika. Kama nilivyosema ni kwamba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma sasa hivi ndiyo inayosimama ile *payroll system.* Kwa hiyo, suala la watumishi hewa kwa sasa hivi halipo. Kwa wale ambao walikutwa na matatizo ya watumishi hewa huko nyuma, baada ya kufanya *data cleaning,* yaani kuingiza taarifa za wafanyakazi wote nchi nzima katika mfumo, wanachukuliwa hatua za kisheria. Masuala mengine yako *PCCB* na wengine wamefikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa sana ni la watumishi kukaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu, hilo lilijibiwa na TAMISEMI, kwamba mtumishi kwa mujibu wa sheria anatakiwa akae kwenye kituo siyo zaidi ya miaka mitano. Kwa hiyo, wale watumishi ambao wamekaa kwa muda mrefu sisi tunachukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba wanahamishwa pale inapoonekana kwamba inabidi ahamishwe, lakini tatizo kubwa ni lile la ufinyu wa bajeti. Hatutaki kumhamisha mtu wakati hatuna fedha za kumlipa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ukweli usiopingika kwamba wakati mwingine mtumishi akikaa sehemu moja kwa muda mrefu anafanya kazi kwa mazoea na ukimbadilisha

kwenda sehemu nyingine anafanya kazi vizuri zaidi. Kwa hiyo hilo tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na Mheshimiwa Sylvester Mabumba walisema utaratibu wa Ajira za Mkataba kwa watumishi waliostaafu.

Waheshimiwa Wabunge nimejibu mara nyingi tu kwamba watumishi tunaowachukua mara nyingi ni wale ambao hawako kwenye soko la ajira kama vile Watumishi wa Afya, Walimu, Marubani na kada nyingine ambazo kwa kweli zina upungufu wa kutosha. Lakini kuna watumishi ambao Serikali inaona kwamba kuna umuhimu kumpa Mkataba kulingana na mazingira ya kazi. Kwa mfano, kuna baadhi ya miradi, ili amalize mradi ule inabidi Serikali impe mkataba ili ule mradi aumalize vizuri kwa kuwa ameanza yeye. Kwa kweli Serikali inapoona kuna hitaji hilo, sisi tutawaajiri watumishi hao kwa mkataba.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi zile ambazo ni *Presidential Appointment* kwa mujibu wa Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais anayo mamlaka ya kuteua mtu yeyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika wadhifa wowote kama atakavyoona inafaa. Kwa hiyo, zile nafasi za uteuzi wa Rais msimwulize Mama Kombani wala nani; ni Katiba yetu inaruhusu na kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba tunaajiri watumishi, tunawapa mikataba baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu kama tulivyosema, ni kwamba tunaajiri watumishi 61,000. Hao ni watumishi wapya tu. Haijawahi kutokea hata mwaka mmoja kuajiri watumishi wengi wa namna hiyo. Achilia mbali watumishi wale watakaostaafu, tutakuwa na watumishi wastaafu karibu 7,000; achia mbali ya wale watumishi ambao watakaoacha kazi.

Kwa hiyo, tutaajiri watumishi siyo chini ya 70,000. Kwa kulingana kanzi *data* yetu ambayo inachukuliwa na

Sekretarieti ya Ajira mpaka sasa kuna wahitimu wa Vyuo mbalimbali ukitoa walimu, ukitoa na Watumishi wa Afya kuna kanzi *data* ya wahitimu 28,000. Nimesema kwamba kwa mwaka huu tunaajiri watumishi wa kada mbalimbali nje ya Walimu, Madaktari, wa Kilimo na Mifugo 12,000. Sasa 28,000 tukitoa 12,000 watakaoajiriwa watakuwa wengi, ongeza nafasi mbadala 7,000 ina maana tutaajiri watumishi wengi sana na wengine watakaoajiriwa na sekta binafsi ni wengi. Kwa hiyo, tatizo la ajira litapungua kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kidunia tatizo la ajira ni kubwa. Kwa Tanzania tatizo la ajira ni asilimia 11.5, wenzetu Kenya tatizo la ajira ni asilimia 40, ukienda Uganda tatizo la ajira ni asilimia 3.5, ukienda nchi za Ulaya tatizo la ajira liko kati ya asilimia 11 - 12, ukienda Marekani tatizo la ajira liko asilimia 7.7.

Kwa hiyo, jamani tatizo la ajira liko dunia nzima, siyo Tanzania peke yake na sisi Tanzania tunajitahidi kwa kiasi kikubwa. Angalia an *employment rate* ya Kenya ni asilimia 40, ni kubwa sana, ndiyo maana wengine wanakimbilia Tanzania kupata ajira katika sehemu mbalimbali hata kazi za mahotelini wao wako tayari kufanya. Kwa hiyo, tatizo la ajira tusiliangalie tu kwa Tanzania, tuliangalie kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu Serikali kupitia wataalam wa kompyuta kuweka zuio la matumizi ya mtandao wa kijamii, yaani *facebook*. Ni kweli watumishi wa Serikali wakati mwingine wanatumia hivyo vyombo vya Serikali vibaya. Kama nilivyosema kwamba wanatumia rasilimali vitu vibaya. Kwa hiyo, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imetoa maelekezo kwa Taasisi zote za Umma kwa Waraka wa Na. 5 wa mwaka 2009 kuhusu matumizi bora na salama ya vifaa na mifumo ya *TEHAMA* Serikalini.

Katika waraka huu Serikali imekataza vifaa na mifumo ya *TEHAMA* Serikali kutumika tofauti na makusudio ya Serikali. Taasisi zote za umma kupitia Waraka huu kwa kuhakikisha

Mfumo wa TEHAMA haitumiki kwa mitandao ya kijamii na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaokiuka maelekezo hayo. Ndiyo kama nilivyosema kwamba rasilimali vitu vya Serikali visitumike vibaya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni tatizo la watumishi kutokuwa na kauli nzuri kwa wananchi. Ni kweli kuna baadhi ya watumishi katika Taasisi za Umma ambao wanatumia kauli mbaya kwa wananchi ambao wanawahudumia. Hilo siwezi kubishana na ninyi, lakini hilo ni kinyume kabisa na utaratibu wa Sheria. Ukienda Hospitalini, ni kweli baadhi ya Manesi wana lugha mbaya, wanawaita wazazi wifi. Kwa hiyo, lugha kama hizi hazitakiwi mahali pa kazi.

Mimi niwaase tu, watumishi wa umma kutotumia lugha chafu au lugha mbaya na lugha za kejeli katika utendaji wao wa kazi. Kwa hiyo, wale Wabunge ambao wanaona kuna watumishi ambao kauli zao ni chafu na pengine tunamhamisha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine anaendelea na tabia hiyo, naomba mtupe taarifa ili tuweze kumshughulikia mtu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine kuhusu vyeti vya ku-*forge*. Limezungumziwa kwamba baadhi ya watumishi wa umma wana vyeti vya ku-*forge* na siwezi nikawakatalia. Sekretarieti ya Ajira imeliona tatizo hilo, kuna watu ambao wana-*forge* vyeti. Tatizo la ku-*forge* vyeti jamani tusiliangalie tu kwa watumishi wa umma, tujiangalie na sisi wenyewe humu na sisi tusiwe tuna-*forge* vyeti. Kama mtu umemaliza Darasa la Saba, sema kwamba mimi nimemaliza Darasa la Saba, umemaliza Kidato cha Nne, andika umemaliza Kidato cha Nne, umeandika Chuo Kikuu andika hivyo. Kwa hiyo, tatizo hili tusiliangalie kwa Watumishi wa Umma tu, lakini na sisi Bungeni tuliangalie pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Sekretarieti ya ajira sasa hivi inachofanya, inafanya mchujo mkali sana. Inawasiliana na *NECTA, RITA, VETA JKT* na *TRA* kuhakikisha kwamba wanashirikiana kuwabaini wale watumishi ambao wana-*forge* vyeti. Mimi nilikuwa Afisa Utumishi Chuo Kikuu. Kwa kweli

nilikuwa nawabaini tu, nikiangalia Cheti cha *NECTA, D* ya *NECTA* ya mwaka 1966 na *D* ya sasa hivi zinafanana. Ukiangalia utofauti upo kabisa vyeti vya ku-*forge* na vitu vingine. Kwa hiyo, Serikali tumelibaini na tutahakikisha kwamba wale watumishi wanaoajiriwa hawaajiriwi kwa vyeti vya ku-*forge*.

Mheshimiwa Spika, nimeshaiagiza Ofisi yangu, tunalifanyia kazi hilo tatizo. Wapo Watumishi wa Umma ambao wako kazini lakini wanatumia aidha vyeti vya kugushi au vyeti vya watu waliokufa au vyeti vya ku-*forge*. Tutalifanya zoezi hili kwa umakini sana na tutachukua muda mrefu kidogo. Kwa hiyo, watumishi mtatusamehe kwamba sisi sasa hivi tunataka watu wenye *qualification* na sio wale ambao wame-*forge* vyeti. Sasa hivi kuna tatizo la ajira wasomi ni wengi, kwa hiyo, wale ambao wame-*forge* vyeti wajiandae kabisa kwamba kuna zoezi hilo la kufanya kutathmini vyeti kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu kuwaendeleza baadhi ya watumishi na watumishi wengine kutowaendeleza. Ni kweli nikubaliane na baadhi ya Wabunge kwamba kuna Ofisi ambazo zina upendeleo. Utakuta huyo huyo anakwenda *training*, huyo huyo anakwenda kwenye mafunzo, semina na kozi mbalimbali. Hili tumeshalitolea Mwongozo wa kuhakikisha kwamba kila Taasisi ya Umma inatengeneza *Training Program* ili wafanyakazi ambao wanakwenda *training* kwa mwaka fulani waweze kujibaini kwamba mimi zamu yangu ni mwaka unaofuata au mwaka huu ili tuweze kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limeongelewa sana ni kuhusu utaratibu wa kujaza nafasi unachelewa sana hasa zile nafasi mbadala. Tunachosema ni nini? Ni kwamba mtumishi anapofariki, au anapoacha kazi au kuachishwa tunaomba taarifa zitufikie mapema Utumishi ili tuhakikishe kwamba hizi nafasi mbadala tunazijaza mara moja kwa sababu zenyewe hazihitaji vibali au nini, maadam kwenye mfumo wetu tumeshaona kwamba mtumishi fulani

amefariki au ameacha kazi, *replacement* tunaifanya mara moja.

Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, ni kwamba Sekretarieti ya Ajira inapofanya *interview* kuna watu wengi huwa wanafaulu. Kwa hiyo, tunaiweka kwenye *database* kwamba watumishi hao wamefaulu. Inapotokea nafasi tuna-*off load* ile *database* au tunawapangia sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, tatizo hili kwa ujumla limeanza kupungua lakini tutaendelea kuliimarisha ili kuhakikisha kwamba hizo nafasi mbadala hazikai kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Angellah Kairuki alisema kuhusu Mfumo huu wa *Human Capital Management Information System* wakati mwingine unachelewa. Kwa sasa hivi kwa kweli hakuna uchelewaji. Ile Idara ya *Human Capital Management Information System* au watumishi wale wanaoshughulikia suala la kuingiza mifumo na ku-*process payroll,* tumewawekea fedha nyingi.

Hata ukiangalia kwenye kitabu chetu tumewawekea fedha nyingi ili wafanye kazi mchana na usiku ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi usiku. Mfumo huu unafanya kazi vizuri zaidi usiku wakati mifumo mingine yote imetulia. Kwa hiyo, suala la mfumo huu sasa hivi, unafanya kazi kwa ufanisi na watumishi wale tunawapa motisha kuhakikisha kwamba wanafanya kazi masaa 24 hasa wakati wa *peak period* ambazo wanatengeneza *payroll* ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, suala linguine, Mheshimiwa Angellah pia alisema kwamba ule mradi wa *Regional Communication Infrastructure Programme* uangalie uwezekano wa kutengeneza mfumo wa *Birth And Death Registration System*. Sisi tunasema kwamba mradi huo unafadhili miradi mbalimbali mojawapo ni huo mfumo na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kupitia Wakala wa Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba imeweza kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huu wa *Tele Justice* ili kujua mahitaji halisi ikiwemo namna bora ya kuziunganisha Mahakama zote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira, Mheshimiwa Mariam Kisangi amesema Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iangalie utaratibu wa ajira na kurudisha zile ajira za nafasi za chini, chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mimi nimesema Waraka huu tumeshauleta hapa Bungeni na wakati wa *briefing* kama mlimsikiliza Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu walisema kwamba wataangalia nafasi kuhakikisha kwamba Waraka huu wa ku-*delegate* baadhi ya nafasi katika Utumishi wa Umma ili zifanyike kule kule kwenye Halmashauri au kwenye Taasisi husika unafanyika. Kwa hiyo, Waraka huu uko mikononi mwetu na tukipata muda tutaujadili na sisi kwa kweli tulitaka kuanzia tarehe 1 Julai nafasi hizi za chini ziajiriwena Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo aliongelea kuhusu huduma kwa viongozi wastaafu ziboreshwe. Kwa kweli huduma za viongozi wastaafu sasa hivi tumeziboresha, hata msemaji mmoja amesema kabisa kwamba amekwenda kule Butiama ameona kuna kazi nzuri iliyofanyika na nyumba za wastaafu tunaziboresha. Tunazidi kuwalea na kuhakikisha kwamba wanapata matibabu, wanapata hifadhi, wanapata ulinzi, wanapata magari mazuri ili tuwaenzi hao wastaafu wetu.

Ni kweli wakati wanapofanya kazi viongozi hawa kwa kweli hawafaidiki au hawakufanya kazi kwa raha. Kwa hiyo, wanapostaafu ni lazima tuwaenzi. Kwa hiyo, Ofisi yangu inafanya kila njia kuhakikisha kwamba wanapata matibabu na mambo mbalimbali ili kuwaenzi na waishi maisha mazuri. Tunajitahidi na waishi maisha yao kwa umakini. Kuna tatizo la maji Butiama, kuna tatizo la maji pia kule kwa wajane wa Mheshimiwa Hayati Sokoine, hayo tunayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rage yeye ametuomba tu kwamba Chuo cha Utumishi hakina mabweni. Kwa kweli hilo tunajitahidi. Tunasema kwamba tutajenga mabweni katika Vyuo vyetu kikiwemo cha Tabora. Suala la Zahanati, kwa kuwa Watumishi wa Afya wanaajiriwa mwezi

wa Tano tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunaleta Watumishi wa Afya katika Zahanati ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tabora.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kima cha chini cha mshahara. Nilishasema kwamba mshahara wa mtu ni siri yake, ila nilitaja *figure* kwamba mwaka huu tumetoka kwenye Shilingi trilioni 3.7 tumekwenda kwenye Shilingi trilioni 4.7 Kiasi hicho ni ongezeko kubwa. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba watumishi wanapata promosheni zao, watumishi wanapata *increment* zao lakini pia tutaongeza kiasi fulani cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni re-*categorization*, kwamba kuna baadhi ya watumishi anakwenda kujiendeleza halafu anashushwa tena chini. Kwa upande wa Walimu tumeshahuisha Muundo wao wa Utumishi. Kwa hiyo, akienda kujiendeleza na kupata *Diploma* anakuwa Afisa Elimu Msaidizi, akipata *Degree* anakuwa Afisa Elimu.

Kwa hiyo, miundo yote tutaihusisha ili kuhakikisha kwamba hatumshushi mtumishi yoyote chini ili wale wanaofanya mafunzo katika kada husika waweze kupata promosheni zao au waweze kuwekwa kwenye stahili zao. Lakini yule mtumishi ambaye kwa mfano Mwalimu amekwenda kusomea Uafisa Utumishi, lazima atarudi kwenye kada ya mwanzo ya Uafisa Utumishi, kwa kuwa amekwenda kujiendeleza kwenye kada ambayo sio yake. Kwa hiyo, ataanzia mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msabaha anasema kwamba kuna baadhi ya Makatibu Wakuu wanajilimbikizia mali. Mimi nasema kujilimbikizia mali ni uvunjifu wa Sheria. Tuna Sekretarieti ya Maadili ndiyo inayoangalia suala hili. Kama kuna mtu amejilimbikizia mali, wanamwita kumhoji kuhusu uhalali wa mali zake. Kwa hiyo, hilo tuwaachie wenzetu wa Tume ya Maadili ili waweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba watumishi wawe wanapangwa kwenye Mikoa yao wanayotoka.

Jamani tuzingatie Utaifa. Sasa hivi tunasema kwamba mtumishi akiajiriwa apelekwe popote bila kuangalia kwamba ametoka mahali gani au tumpeleke mahali gani. Tukisema hivi, baadhi ya sehemu watakosa watumishi. Niwaambie habari njema kwa wenzetu wale wa Zanzibar, naomba kwenye kikao cha Muungano, kero za Muungano, suala la watumishi pia liliongelewa. Kwa hiyo, Watumishi wa Umma ambao wanataka kuhama kutoka Zanzibar kuja Bara na kutoka Bara kwenda Zanzibar, sasa hivi wanaruhusiwa. Tunaweka utaratibu ili kuhakikisha kwamba utaratibu huu hautakiukwa. (Makofi)

Kwa hiyo, Mpemba akitaka kuhamia Bukoba sasa hivi ruksa kwa Wizara zile ambazo ni za Muungano, ilimradi tu wasichague kwamba naomba mnipeleke Dar es Salaam au Tanga, hapana. Popote pale wawe wafanye kazi. Ndiyo Muungano wenyewe na ndiyo Utaifa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandishwa madaraja, hasa ya Walimu, kama mkiangalia kwenye hotuba yangu, nimesema kwamba Tume ya Utumishi wa Umma kuna Idara ile ya *TSD,* pale tumewaongezea fedha ili waweze kukaa vikao vyao vya Kisheria. Kama mmeona, mwaka huu watakaa vikao vyao vyote vya Kisheria. Wakikaa vikao vyao vya kisheria, ina maana hata *promotion* zitakwenda kwa wakati. Kwa hiyo, hilo tumelizingatia na tumelifanyia kazi. Rai hii ilitolewa na Mheshimiwa Makala na Wachangiaji wengine.

Ndugu yangu Ole-Medeye amesema kuhusu kuharakisha ajira mpya isipokuwa hoja ya Mwajiri hoja kuomba kibali kuajiri badala ya kibali cha Ikama kilichotolewa na Utumishi kiwe ni kibali cha mwisho. Jamani *for the control purposes,* ndiyo maana imeanzishwa Sekretarieti ya Ajira pamoja na kupata vibali kutoka Utumishi. Utumishi ndiyo inayosimamia Watumishi wote wa Umma. Tusipokuwa na utaratibu wa vibali kutoka Utumishi kila mtu ataajiri watu wake anavyotaka. Kwa hiyo, Sheria hii inabidi tuisimamie kuhakikisha kuwa vibali vyote vinatoka Utumishi ili tuweze kuajiri kwa kufuata sheria na utaratibu. Hii ni *control mechanism* ili kila mtu asiajiri kiholela na hata nafasi zile

ambazo tuta-*delegate* katika Halmashauri ni lazima zipate kibali kutoka Utumishi.

Hivyo, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Watumishi na mishahara ili kuhakikisha ukomo wa bajeti iliyoidhinishwa unazingatiwa. Kama tulivyosema tutaajiri Watumishi 61,000, ni lazima kitoke kibali maalum kwa ajili ya watumishi hao. Niyo ni *control mechanism*.

Mheshimiwa Lwanji amesema Sekretarieti ya ajira ina urasimu wa kuendesha huo mchakato. Jamani, ili tupate Watumishi bora ni lazima tuchuje. Wenyewe mmeshasema hapa kuwa kuna vyeti vya ku-*forge.* Ni lazima tuangalie vitu kama hivyo. Nimesoma kabisa kwenye changamoto za Sekretarieti ya Ajira, kuna watu wanao-*forge*, kuna watu wanaotumia sifa za uongo, pale ni lazima tuangalie hizo *factors* zote ili kuhakikisha tunapata Watumishi bora na siyo bora Watumishi. Kwa hiyo, hilo kwa kweli tutaendelea kulisimamia na kuhakisha kuwa tunapata Watumishi bora na kuwaajiri katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niunganishe na suala lile la Mheshimiwa Munde na Mpina ambao wamesema kwamba suala la kukaimu linachukua muda mrefu. Ni kweli suala hili linachukua muda mrefu. Lakini Waheshimiwa Wabunge *vetting* inachukua muda mrefu ili tusiweke Wakuu wa Idara hovyo hovyo, wasio na maadili, wasiofuata Kanuni. Ni lazima *process* ya *vetting* ichukue muda ili kuhakikisha kuwa tunawapa Watumishi wa Umma ambao ni wazuri. Mmeona kuna upotevu wa rasilimali watu, rasilimali fedha na rasilimali vitu, sasa mkisema kwamba tulipue tu, tumweke Mkuu wa Idara ili mradi ni Mkuu wa Idara, tutakwenda kinyume cha sheria na hatutawapata Wakuu wa Idara wazuri.

Rai yangu ni kwamba sisi tutahakikisha kwamba huo mchakato angalau unachukua muda mfupi ili kuhakikisha kwamba tunapata Watumishi bora. Lakini la kusema kuwa tusiwafanyie *vetting* au *vetting* inachukua muda mrefu hilo ni lazima tulifanye na ni lazima tufuate sheria hii, tuwaache

watu wa *vetting* wafanye kazi zao vizuri ili watushauri sisi upande wa Serikali kwamba nani anafaa na nani hafai. Wakati mwingine mchakato huu unachukua muda mrefu kwamba yule waliyemleta hafai. Kama hafai, tunamrudishia mwajiri, tunachukua kundi lingine ambalo tunalifanyia *vetting* na kuwapeleka katika sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Habari na Idara ya Maelezo ilianzisha tovuti ya wananchi miaka michache iliyopita kwa gharama kubwa, kwamba Serikali sasa itoe maelezo ya sababu ya kuingia gharama nyingi ya kutengeneza tovuti nyingine ya wananchi. Sisi tunachosema ni nini? Tunaanzisha tovuti ya Serikali kwa ujumla. Yaani habari zote za Serikali ziweze kupatikana katika mtandao mmoja. Ukitaka mambo ya Uraia unayapata katika mtandao mmoja.

Kwa hiyo, tovuti ya wananchi ilianzishwa chini ya Wizara ya Habari na Idara ya Habari, Maelezo, ni mfumo unaowawezesha wananchi kuwasilisha maoni na hoja kwa Serikali kuhusu utendaji na mambo mbalimbali, kufuatilia majibu na hoja zinazotolewa na wananchi na kuiwezesha Serikali kupokea na kushughulikia hoja na maoni mbalimbali yaliyokuwa yanatolewa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati tovuti hii ilipoanzishwa chini ya Wizara ya Habari, ni mfumo na tovuti kuu ya Serikali ni dirisha, huduma na taarifa zote zinatolewa na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa njia ya mtandao. Kama nilivyosema kwamba, yaani tovuti moja wananchi watakuwa wanapata habari mbalimbali kutoka katika tovuti moja badala ya kuwa na tovuti mbalimbali.

Suala lingine ni kuhusu vipaumbele na Mkakati wa Serikali na nini matarajio ya Watanzania. Hili lilitolewa na Dkt. Mary Mwanjelwa. Tunasema majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake, ni kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya Utawala Bora kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Utekelezaji wa majukumu haya ambayo nimeyaeleza bayana yako katika hotuba yangu ukurasa wa 80 mpaka ukurasa wa 100 ambayo tutayatekeleza kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Munde pia alisema kwamba Sekretarieti ya Ajira inawatesa wale wanaoomba ajira, mpaka *interview* iwe Dar es Salaam na sehemu nyingine. Ni nia ya Serikali kwamba kila Mkoa tuwe na *Branch* ya Sekretarieti ya Ajira. Lakini mpaka sasa hivi hatujaweza kupata fedha za kutosha, kwa mwaka huu tutakachofanya ni kuhakikisha kwamba tunatenga fedha za kutosha ili baadhi ya Vituo viwe Mikoani. Tumeshaanza, baadhi ya Watendaji wa Sekretarieti ya Ajira wanakwenda Mikoani kufanya *interview* mbalimbali. Kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi. Kwa kuanzia mwaka huu tutakuwa na Kituo kule Zanzibar kuhakikisha kwamba nako tunafanya mchakato wa *interview* kwa sababu Wizara yangu ni Wizara ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ambayo yamejitokeza ni kuhusu mmomonyoko wa maadili kwa Watumishi wa Umma. Hilo nimeshasema kwamba lipo na Mheshimiwa Nyambari alisema Askari Polisi wanakula rushwa, labda ni kwa sababu ya maslahi madogo. Lakini niseme kwamba suala la rushwa ni la mtu binafsi, na siyo Askari wote wanakula rushwa na siyo Watumishi wote wa Umma wanakula rushwa. Ni baadhi yao wanaofanya vitendo hivi vya kuvunja maadili.

Kwa hiyo, tusiwanyoshee vidole Watumishi wa Umma, bali wale ambao mnaona kuwa wanapokea na kutoa rushwa, hao ndiyo tuwashughulikie. Serikali imeanzisha Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi Umma ili kuangalia uboreshaji wa maslahi ya Watumishi wa Umma kwa ujumla wake. Ndiyo maana nimesema kwamba tutaangalia maslahi ya Watumishi wote wa Umma bila kuangalia huyu ni wa kada gani na huyu ni wa kada gani.

Mheshimiwa Jafo alikuwa anasema kwamba tuangalie ile *Pay As You Earn* kwa Watumishi wa Umma. Nakubaliana naye kuwa ni mzigo mkubwa, lakini Serikali

mwaka 2007/2008, ilishusha sana kiasi cha *Pay As You Earn* kutoka 18% hadi 14%. Niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kuwa tumekaa vikao na wenzetu wa *TUCTA,* tumeelezana vizuri, tumeeleweshana na hilo wanalisemea kwa nguvu zote na nyinyi Wabunge mmelisemea kwa nguvu zote. Hili kwa upande wa Serikali tumesema kuwa tunaangalia na ile Bodi ya Mishahara na Maslahi kwa kuwa imeanza tu mwaka 2012, nadhani huko tunakokwenda watafanya vizuri zaidi. Watafanya vizuri zaidi kwasababu watakwenda katika nchi mbalimbali kuangalia wenzetu maslahi na mishahara wanatumia mbinu gani au wanawamotisha vipi Watumishi wa Umma. Hilo hatulipuuzi jamani! Hilo tunalifanyia kazi kwasababu mimi ninaguswa, wewe unaguswa na Watumishi wote wa Umma wanaguswa na hiyo *Pay As You Earn.*

Mheshimiwa Soni alisema tuongeze Watumishi wa Kilimo. Tumesema mwaka huu Watumishi wa Mifugo, Kilimo pamoja na Watumishi wa Idara ya Nyuki tutaajiri Watumishi karibuni 4,000. Kwa hiyo, hiyo ni idadi kubwa sana kwa wataalam hao kukidhi haja ya Kilimo Kwanza. Watumishi hao watapelekwa katika *level* ya Kata na *level* ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, niwaase Halmashauri zote hasa za Manispaa na Majiji kuhakikisha kwamba Watumishi wale ambao ni wa Kilimo wasipangiwe Mijini. Wapangiwe Vijijini kwenye mashamba. Pale Mjini hakuna mashamba. Ukimweka Afisa Mifugo nitakuelewa kwasababu tunafuga mifugo *zero grazing,* lakini ukimweka Kilimo pale Dar es Salaam sijui anasimamia nini pale Dar es Salaam. Kwa hiyo, wengi tutawapanga Vijijini kama ilivyo kwa Watumishi wengine.

Suala lingine la Mheshimiwa Kasembe, yeye anasema kwamba Serikali ifanye utaratibu wa kuwachukua wale Watumishi wa JKT na kuwaajiri. Hili ni suala zuri. Naomba tuwaachie wenzetu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama walifanyie kazi ili kuhakikisha kwamba kama ana-*meet* vile vigezo aajiriwe, au iwe kama *added advantage,* kwamba wakitangaza kwamba Watumishi wa Magereza, Polisi na JKT

hao JKT iwe kama *added advantage* kwasababu wameshapitia katika vyombo hivi vya ukakamavu.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine mbayo hatukuyatolea ufafanuzi, naomba nijibu moja tu ambalo Mheshimiwa Mwigulu Nchemba amesema, Serikali ibadilishe mfumo ili kuruhusu wataalam wa kada mbalimbali kwenda kufundisha ili kukidhi mahitaji ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, tunasema kwamba ipo fursa kwa kada yoyote kuajiriwa katika Ualimu, lakini suala la Ualimu ni taaluma inayojitegemea. Hivyo, endapo mtu wa kada nyingine atahitaji kuajiriwa kufanya kazi ya Ualimu, atapaswa kuhudhuria Mafunzo ya Ualimu na mbinu za ufundishaji ili kufanya kazi hiyo kwa ufanisi zaidi.

Wale wengine waliosema kuwa tuliwaajiri Walimu wakati ule tulipokuwa na tatizo la Walimu, wengine walikuwa wanawaita *Voda Faster* wale wa muda mfupi; ile kada imeshaji- *phase out* kwasababu tuliwapa muda maalum wa kujiendeleza na wengi wamejiendeleza. Hata ukiangalia katika mtandao wetu, wamebaki Watumishi wachache sana ambao hawajajiendeleza na wako Vyuoni wanajiendeleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao. Michango yao mingine na hoja mbalimbali tutazijibu na tutazitoa hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge wote na majina yao pamoja na hoja zao na majibu yetu yaweze kuwafikia kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI,OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni sehemu ya hoja, kwa hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, jana Mheshimiwa Halima Mdee aliomba Mwongozo wa Spika kuhusu kazi tunayofanya wakati wa Kamati ya Matumizi. Moja katika maeneo ambayo alisemea ilikuwa ile ya Mshahara wa Waziri.

Sasa Waheshimiwa Wabunge mkisoma hiyo Kanuni kuanzia zile Kanuni tulizobadilisha, Wabunge mna nafasi nyingi sana za kuhoji wakati wa Kamati ya Matumizi. Kamati ya Kanuni iliamua kwamba mshahara wa Waziri tuupe dakika 25 na kwa sababu ni mambo ya kisera, yaani huwezi kuuliza habari ya Kijiji au maji ya sehemu yako, ni mambo ya kisera.

Kwa hiyo, Vyama vinamsaidia Spika kujaribu ku-*identify* watu ambao wanaweza kuuliza sera ambayo inahusu nchi nzima. Siku ile kwa Waziri Mkuu ilifanyika vizuri. Muda anaopewa yule atakayepewa nafasi hiyo ni dakika tano, na muda wote wa Mshahara wa Waziri ni dakika 25.

Kwa hiyo, madhumuni ya kufanya hivyo ilikuwa ni kusudi tuweze kumaliza kitabu kizima kinachohusiana na Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Lakini hakikumyima Mbunge; kwa mfano, mtu amesikiliza tena, hii ni ile ya Mshahara wa Waziri, lakini bado kuna vifungu ambapo Mbunge anaweza kuhoji kifungu baada ya kifungu unaweza kuhoji. Lakini ipo Kanuni inayokwambia, kama yale maelezo ya Waziri hukuridhika, nayo siyo kwenye Mshahara wa Waziri, na kwingineko, unatoa Shilingi.

Ukitoa Shilingi tofauti na ufafanuzi mwingine, ule ufafanuzi mwingine unauliza dakika tano, wanakujibu, basi. Sasa inawezekana Waziri akakujibu na wewe hukuridhika na jibu lake; unayo nafasi ya kutoa Shilingi. Sasa kutoa Shilingi, ni hoja. Kwa hiyo, utatoa dakika zako tano, kama una watu wanaokuunga mkono au wanataka kuungana hapo

wataingia na watapata dakika tatu. Tutajadili, isipokuwa Kanuni haikuweka ni wangapi wanaweza kukuunga mkono. Hiyo haikuweka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya dakika hizo, yule uliyemtolea Shilingi kwa upande wa Serikali atajibu, na bado wewe uliyetoa Shilingi unao muda tena; na kwa Kanuni ya 103(6 na 7) inasema: "Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu ya hoja hiyo." Ya saba inasema: "Mbunge aliyetoa hoja ya kuondoa Shilingi ndiye atakayefunga mjadala wa hoja hiyo." Ya nane inasema: "Muda utakaotumiwa na Waziri na Mbunge kwa mujibu wa tafsiri ya sita ile ndogo na saba utaamuliwa na Spika."

Kwa hiyo, tuna *a lot of time!* Tuna muda sana. Maana yake kwanza Mshahara wa Waziri ni suala la Sera, halihusu eneo lolote. Kwa hiyo, tumeji-*limit* 25 *minutes* za Wabunge kuhoji halafu wanaohusika watajibu. Lakini kuna nafasi ya dakika tano ya ufafanuzi katika kila kifungu ukitaka. Dakika tano, utajibiwa. Kwasababu moja au nyingine yale majibu labda unaona mimi sijaridhika, unasema pale pale baada ya kusimama, unasema naomba kutoa Shilingi. Ukisema naomba kutoa Shilingi, maana yake umeanzisha hoja. Kwa hiyo, hoja yako ile itaungwa mkono na wenzako mbalimbali, siyo lazima wanaokuunga mkono, lakini hata wanakupinga watakuwamo humo humo, lakini wale wanapewa dakika tatu tu.

Wakimaliza hao, basi inakwenda kwa upande wa Serikali kwa Yule anayehusika na hilo jambo. Wewe ndiye utakayefunga hiyo hoja. Sasa kama sisi wenzako hatuwezi kuendelea kubishana, tutapiga kura. Kama tunakubaliana na wewe tunakuunga mkono na kama hatukubaliani na wewe tunakupinga. Kama tunakubaliana na wewe, basi lile fungu litapita kwa kuwa limeondolewa Shilingi moja. Kama tumeikataa, basi tunaendelea na shughuli kama kawaida.

Kwa hiyo, utaratibu huu una nafasi nyingi za kutosha. Kwa hiyo, siyo kwamba hauna nafasi kwa Wabunge kuhoji mambo ambayo wanataka kuhoji, ila msome vizuri, mjiandae vizuri, tusipoteze muda na ukifika sasa utakuwa *specific.*

Ukiondoka kwenye Mshahara wa Waziri mkifika katika vifungu vingine ni *specific* na utapaswa kuwa *specific.* Hii tunapenda ituwezeshe tufike mpaka kwenye *Volume* ya Maendeleo. Tulikuwa hatufiki, ndiyo ilikuwa sababu hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwasababu sina matangazo mengine, naomba nisitishe shughuli mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.20 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipomaliza asubuhi, moja kati ya watoa hoja, Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi alishatoa maelezo. Sasa nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, unayo saa moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine tena ili niweze kutoa maelezo ya kufunga mjadala.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema jambo linalohusiana na hoja iliyopo mbele yetu, ningependa kuungana na wananchi wengi ambao wameonesha kukerwa na mambo yanavyoendelea hapa Bungeni. Hadhi ya Bunge letu inaonekana kuathirika kwa maoni ya walio wengi huko nje. Maoni ya Mheshimiwa Lekule Laiser na Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa yangeweza kutusaidia katika kurekebisha hali kama walivyokuwa wanayatoa leo asubuhi kupitia *TBC1*, na mimi nawaunga mkono ili tuweze kuimarisha hadhi na heshima ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu walinipigia simu leo wakaniuliza, kwanini mimi situmii uzoefu wangu kama ulionao wewe Mheshimiwa Spika kusaidia Bunge letu ili liweze kuendesha mambo kwa kuzingatia Kanuni. Nami niliwaambia

nitajaribu, lakini nikawaambia vile vile uzoefu unategemea kama mambo yenyewe umewahi kuyaona. Haya yanayotokea hapa sijawahi kuyaona. Kwa hiyo, uzoefu wangu inawezekana ukawa hauna msaada sana. Nilichowahi kuona ni utulivu na kuheshimu Kanuni. Hili Bunge la kusukumana humu, mimi sijapata kushiriki.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naamini ukishirikiana na Viongozi wa Vyama vya Siasa vilivyo na Wabunge hapa Bungeni ukawaweka chini, wakutane na kufikia muafaka wa namna ya kurudisha hadhi ya Bunge letu, itakuwa ni jambo zuri. Mimi nadhani wote tungependa kuona Bunge letu linaendeshwa kwa heshima kulingana na mazingira na jinsi wananchi wanavyopenda kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo, sasa katika kujibu hoja, ningependa nianze na masuala mawili ya jumla, tena makubwa, kuyatolea maelezo ya jumla na kisha nitajibu mengine kwa kadri muda utakavyoniruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwanza labda nianze na jambo kubwa ambalo linatatanisha, tena nyeti, linaitwa udini. Kwanza ni lazima nikiri kwamba iko dalili ya kuenezwa udini katika nchi yetu, jambo ambalo kwanza ni geni, lakini vile vile ni baya na ni la hatari.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, udini huo unaojaribu kuenezwa haujavuruga maisha ya kawaida ya wananchi wetu Vijijini na Mitaani. Kule Vijijini wananchi bado wanaishi pamoja, huko Mitaani wanakaa pamoja, wanashirikiana Wakristo kwa Waislamu, wanaishi kwa amani, wanashirikiana katika sherehe na katika misiba bila kujali tofauti zao za imani. Kwa hiyo, kwa hapo hatujaharibikiwa sana. Lakini Wahenga walisema, “Usipoziba ufa, utajenga ukuta.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani wakati wa kuziba ufa ni sasa na lazima niseme. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kusema wakati wa uhai wake, kwamba: “Wanaopaza sauti sana kuhusu udini, ndiyo

wanaoueneza.” Haya siyo maneno yangu, haya ni maneno ya Mwalimu Nyerere. Alisema wanaosema sana udini, udini, udini, udini, lakini ukienda unakuta labda wanaosema sana ndiyo wanaoueneza. Kwa hiyo, tuwe makini. *(Makini)*

Mheshimiwa Spika, labda niseme kidogo kuhusu kauli ya Mheshimiwa Mbowe ambayo aliitoa hapa Bungeni alipotoa hoja wakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Mbowe katika hotuba yake alisema: “Waasisi wa udini hapa nchini ni CCM.” Mheshimiwa Mbowe yeye kwakwe alishamaliza kazi, kwa vile alipata mchawi, na mchawi ni CCM. Mimi nasema hili ni jibu rahisi, jepesi kwa tatizo kubwa. *(Makofi)*

Nadhani ni vizuri tuwe na majibu yanayokwenda kutazama ukweli, na kwa kweli kama Viongozi ni lazima tutoe kauli ambazo zinakemea, kuliko kutoa kauli ambazo zinachochea. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, mimi nimejiunga na Chama cha *TANU* mwaka 1959 nikiwa na umri wa miaka 13. Nilishiriki katika Mkutano uliounganisha *TANU* na *AFRO-SHIRAZI* mwaka 1977 nikiwa na umri wa miaka 32.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya *TANU* tangu mwaka 1954 yalikuwa kuwatayarisha Watanganyika kujitawala na kuondoa ubaguzi wa makabila, dini, rangi na jinsia. Hiyo ndiyo *TANU* niliyoijua. Pamoja na kwamba *ASP* iliongoza Zanzibar yenye Waislamu zaidi ya asilimia 90, hawakuitangaza Zanzibar kuwa Jamhuri ya Kiislamu, ingawa wangetaka wangeweza. Waliunda Serikali baada ya Mapinduzi iliyotambua haki ya watu wasiokuwa Waislamu wanaoishi Zanzibar. Kuwepo kwa akina Isaac Sepetu, Marehemu Brig. Gen. Adam Mwakanjuki na wengine wa Zanzibar ambao ni Wakristo ni ushahidi wa *ASP* kutobagua wananchi wake wasiokuwa Waislamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CCM ni Muungano wa *TANU* na *ASP* na sera zake ni Uhuru na Umoja. Haikuwa ajali nembo ya Taifa iliyoasisiwa na Serikali ya Vyama hivyo kuwa na maneno

Uhuru na Umoja. Udini haujapata kuwa sera ya *TANU, ASP* na CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa umoja umejengwa na *TANU, ASP* na CCM, umoja lazima uwe tunu ya Taifa na iwe ni Sera ya Vyama vyote. Bunge na Rais ndio waliochaguliwa na Watanzania katika umoja wao. Bunge kama Taasisi lina wajibu wa kusimama pamoja, bila kujali tofauti za Vyama, kukemea udini, vinginevyo tutakuwa tunaueneza badala ya kuumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udini katika uchaguzi wa mwaka 2010 ulichochewa na wanasiasa waliotaka kupata madaraka ya dola kupitia mgongo wa dini. Mwasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1995 alisema: "Rais wetu atakuwa Mkristo au Muislamu, lakini tunataka ajue hatumchagui kwa sababu ya Ukristo wake au Uislamu wake. Tutamchagua kwa sababu tunaamini kwamba anajua matatizo yetu na yanamkera." Lakini mwaka 2010 hali haikuwa nzuri sana. Niseme yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niongelee kidogo kauli ya Mheshimiwa Godbless Lema - Mbunge wa Arusha. Kwanza, kwamba Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete sio tu kwamba ni mdini, lakini eti ni mwasisi wa udini.

Nilikuwa nataka kumpa Mheshimiwa Godbless Lema popote alipo ushauri wa bure, kwamba ni vizuri atofautishe hotuba za kijiweni na zile za Bungeni. Hapa Bungeni ni lazima patawaliwe na ukweli na siyo jazba na uwongo usiokuwa na msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lema anamshutumu Rais kwa kuvunja Ibara ya 19 sehemu ya pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo iko katika ukurasa wa 31 katika kitabu hiki, ambayo inasema madhehebu pamoja na dini haviwezi kuwa sehemu ya uendeshaji wa dola.

Mheshimiwa Godbless Lema anasema Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano ni mwasisi wa udini. Kwa

hiyo, anachosema ni kwamba Mheshimiwa Rais anaendesha mamlaka ya nchi kwa kufuata imani ya dini yake. Hii ni kauli chafu kusemwa na Mbunge ndani ya Bunge, tena bila ushahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Naibu Spika alimtaka Mheshimiwa Godbless Lema alete ushahidi na sisi Serikalini tuna hamu ya kupata ushahidi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Urais ni Taasisi, siyo mtu. Mtu anakuwa Rais halafu anakuwa Kiongozi wa Taasisi, inaitwa Urais. Urais ni Taasisi kabisa! Rais haongozi peke yake, anashauriwa. Katika uteuzi wa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, mshauri Mkuu wa Rais ni Waziri Mkuu - Mheshimiwa Kayanza Peter Pinda, ambaye ni Mkristo Mkatoliki. Katika uteuzi wa Watendaji Wakuu wa Serikali, Makatibu Wakuu na Wakuu mbalimbali wa Taasisi nyingine anayemshauri ni Katibu Mkuu Kiongozi. Kwanza, alikuwa Ndugu Philemon Luhanjo na sasa ni Ndugu Ombeni Sefue wote ni Wakristo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anayeteuliwa bila kufanyiwa uchunguzi na Vyombo vya Dola. Sasa huo udini wa Rais anaufanyia nyumbani kwake au wapi? Mheshimiwa Godbless Lema alete ushahidi au aliombe msamaha Bunge na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili limeongelewa vizuri sana na Profesa Mark Mwandosya leo asubuhi alipotoa ushahidi kwamba Ofisi ya Rais karibu yote ukimwondoa Rais mwenyewe ni Wakristo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nieleze kidogo kwa ufupi matukio ya hivi karibuni. Ukiondoa matukio ya mwaka 2010 ambayo yalikuwa yameanza kusahaulika na kupotea, matatizo ya karibuni hapa, yalitokana na Viongozi wa Dini kuwa na kanda zinazosambazwa nchini kote, zikiwa na vitisho na kuahidi mauaji kwa viongozi wa kidini. Kanda hizi zimetembezwa, na kwa kweli waliokuwa wanasemwa sana katika zile kanda walikuwa Maaskofu wa madhehebu ya Kikristo. Ni kanda hizi ambazo zimezusha hofu baina ya

Viongozi wetu wa Kiroho wakidhania kwamba nchi sasa haiwezi tena kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, tumewahakikishia Viongozi wetu wa Kidini kwamba tunachukua hatua na kwamba ulinzi na amani itakuwepo nchini na waendeshe shughuli zao bila kuwa na hofu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ndilo limeamsha hisia za udini uliokuwa umeanza kutoweka baada ya uchaguzi wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, sasa lipo jambo ambalo tumechukua hatua. Zile kanda waliokuwa waliokuwa wanazisambaza tumewakamata. Wamekamatwa Mwanza, wamekamatwa huko Simiyu, wamekamatwa Dar es Salaam, wamekamatwa Tanga na kanda zile zote ambazo zinaeneza udini tumesema yeyote aliyenazo aziwasilishe Polisi na akikutwa nazo, atahesabiwa kuwa na yeye yupo katika mpango wa kueneza udini na uchochezi.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hatua moja. Lakini maeneo yote ambayo yamepata athari kutokana na migogoro hii ya kidini hatua zimechukuliwa. Mauaji yaliyotokea Zanzibar ya Padri yapo Mahakamani, hatuwezi kuyazungumza hapa lakini mtuhumiwa alishakamatwa.

Masuala ya watu waliojaribu kuchoma makanisa kule Zanzibar wamekamatwa. Tatizo lililotokea Dar es Salaam ambako makanisa yalichomwa kutokana na kijana mmoja kujaribu kudhihaki *Quran* Tukufu pale, Polisi Mbagala yote yamechukuliwa hatua, pamoja na hatua zilizochukuliwa kule Buseresere ambako kulitokea tatizo ambalo lilisababisha kuuawa kwa Mchungaji wa Kanisa.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nilieleze Bunge lako tatizo linaloitwa kuchinja ambalo limefanya lionekane tatizo kubwa. Lakini hili siyo tatizo kubwa la ajabu. Hili ni tatizo limekuzwa tu.

Kwanza, hili suala la kuchinja hata sisi hatuelewi limeanzia wapi likawaka kama moto. Lakini ukweli ni kwamba mimi nilipokwenda Mwanza baada ya kuwa limechemka sana, nilizungumza na Viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikristo, nilipokwenda Geita ambako kulikuwa na tatizo limetokea katika Kijiji chao kimoja nilizungumza na Madhehebu ya Kikristo na ya Kiislamu. Niliwaambia sisi ni nchi ya amani.

Tena maeneo yale yanajua sana matatizo yaliyotokea katika nchi jirani kama ile ya Rwanda, ambayo yalianzwa kwa vitu vya namna hiyo vidogo vidogo vinavyofanana na ubaguzi, kwamba mtu anabaguliwa kutokana na urefu au ufupi wa pua yake, kwamba hilo ndiyo tatizo. Kwa hiyo, kama una pua fupi unakabiliwa na matatizo, na ukiwa nalo refu vile vile utakabiliwa na matatizo ya wenye pua fupi. Hilo ni tatizo limetokea.

Nikawasihi Viongozi wetu wa kiroho Wakristo na Waislamu wachukue hatua, wazungumze ili tusije tukaingia kwenye mgogoro usiokuwa na msingi kama ambao umewakumba wenzetu.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Geita walinielewa na wale waliotazama taarifa iliyotokana na ule Mkutano wangu na wao, tulipiga picha pamoja, kuonyesha kwamba wamekubali. Walisema hawataki kuingia kwenye mgogoro kwa sababu mgogoro ule utakuja kuwafikisha mahali ambapo hapana msingi.

Viongozi wetu wa Mwanza niliwasihi kwamba wavute subira ili tuitishe Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Madhehebu yetu ya Kikristo na Kiislamu, wazungumze jambo hili walipatie ufumbuzi. Lakini wakati ule ule isingewezekana kuwaambia kabla Mkutano ule haujafanyika na haujafanyika mpaka leo, kwamba watu wa Mwanza sasa wangeendelea kutokula nyama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukasema, mfumo wenyewe wa kuchinja mbona ulizoeleka huko nyuma, haukuwa hoja, hii ni hoja mpya! Lakini tulikuwa tunachinja, wanakula.

Mheshimiwa Spika, labda niwaambie Watanzania, sisi hatuna sheria inayozuia mtu kuchinja nyama nyumbani kwake, haipo! Hakuna mtu anaambiwa wewe kwanini umechinja hapa? Hamna!

Mheshimiwa Spika, hatuna sheria! Hatuna sheria kwa sababu miaka mingi sana suala hili lilikuwa linashughulikiwa na jamii yenyewe. Wewe unataka kuchinja, ukitaka kumwita Muislamu, anakuchinjia.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka katika kabila dogo hapo Bunda, lilikuwa na Waislamu wawili tu, kabila lote, wawili tu! Wengine wala hawakuwa Wakristo walikuwa wapagani tu siku zile mimi nazaliwa. Lakini walikuwa wananituma wanasema nenda umwite Rajab aje na kisu, mimi sielewi cha nini. Akija anachinja! Kumbe wanachosema ni kwamba, anachinja kwa sababu na yeye atakaribishwa kuja kula. Basi ndiyo ilikuwa hoja; na alikuwa halipwi maana tulikuwa hatujaingia kwenye mfumo wa pesa. Kwa hiyo, alikuwa anapewa shingo, anakwenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo yamekuwa maisha. Sasa leo ni jambo kubwa. Lakini kwa sababu dunia hii na utandawazi unaongezeka, hatuwezi kupuuza, inabidi tulishughulikie kama lilivyokuja, tulipatie ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichosema ni kwamba waendelee na utaratibu uliozoeleka, lakini wakati huo tunafanya mazungumzo na Viongozi wetu wa dini mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Godbless Lema, anasema, nilikwenda sikufanya kazi nzuri ya Serikali, alitaka niende kule nitoe amri. Sasa namwambia, unajua mambo ya hekima haya yanatoka kwa Mungu, inategemea Mungu alinigawia kiasi gani na yeye akampa ngapi. Hekima yangu iliniambia kuwashirikisha Viongozi hawa ndio suala zima la hekima, yeye yake ni amri. Sasa angojee atakapopewa hayo madaraka, sijui lini, ndio aje atumie amri peke yake bila ushirikishwaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua katika jambo hili. Wote waliohusika na uchomaji wa Makanisa, nimesema wanashikiliwa; kote Mbagala, Mahakamani, waliochoma Misikiti huko Tunduma, nao wamekamatwa. Wasambazaji kanda wamekamatwa na wengine waliotoroka watarudishwa, tunajua waliko na tunashirikiana na *Interpol* katika nchi walizokimbilia, ili warudishwe hapa kuja kujibu uchochezi.

Mheshimiwa Spika, tumefunga redio kupitia *TCRA.* Redio inaitwa Kwa Neema ya Mwanza ilikuwa inachochea na Redio inaitwa Imani, ya Kiislamu, ya Morogoro, zote zilikuwa zinachochea na kushindana katika kuleta mgawanyiko wa madhehebu haya. Zote zimefungiwa miezi sita, hiyo ni kazi ya *TCRA,* wenyewe wanajua watakachofanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ningependa nizungumzie suala lingine ambalo nalo ni nyeti na limesemwa sana. Nalo linahusu Usalama wa Taifa, suala la Usalama wa Taifa linatisha kidogo.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanasema Usalama wa Taifa huu na ndio ulipelekea Bunge likachelewa, mpaka wakaandika upya, lakini kwa kweli wali-*paraphrase* na kilichobaki ni kile kile cha kusema kuna Usalama wa Taifa unakamata watu, unawatesa. Sasa nataka Watanzania wajue, kama alivyosema Profesa Mwandosya, leo asubuhi; nchi zote duniani zina Idara ya Usalama wa Taifa. Zile kubwa zenye uwezo kama Marekani, zinayo *CIA* na inafanya kazi

nje ya Marekani; maana Marekani wenyewe wanaamini hatari za usalama wao ziko nje zaidi kuliko zilivyo ndani, lakini ndani kuna kitu kinaitwa *FBI,* zote ni Taasisi za namna hii.

Mheshimiwa Spika, sasa na sisi tangu uhuru tunayo Taasisi inaitwa Usalama wa Taifa. Tofauti yake na Polisi na tofauti yake na taasisi nyingine, hawa watu wanafanya chini kwa chini, hawaonekani. Ndio maana hata hapa Bunge, hawaji; wakija atakuja mkubwa wao tu, lakini wengine wote ni watu wako kwenye kazi za chini kwa chini, ndivyo dunia inavyoendeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza mwanzoni, Idara hii ilikuwa inaendeshwa wala Sheria haikuwepo, lakini wanafanya kazi nzuri, nitawaeleza. Mwaka 1996 ndipo tulitunga Sheria Namba 15, ambayo iliwapa Usalama wa Taifa, jukumu la msingi la Idara hiyo ni kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu nchini na sio kuhatarisha usalama. Hawakupewa kazi ya kuhatarisha usalama badala ya kuulinda, kama wanavyojaribu kupotosha badhi ya watu ambao wanausema sana, wanausema.

Mheshimiwa Spika, Idara imefanya mambo mengi sana mazuri, nitawaeleza. Kwanza katika historia yake, wakati wa ukombozi wa Bara la Afrika, Idara hii ndio ilikuwa mhimili katika kutuwezesha kupata habari ambazo ziliiwezesha Tanzania kuwa nchi ambayo imesaidia ukombozi wa Afrika. Hawa watu walikuwa wanajitoa mhanga, wamekwenda Kusini, wakaleta habari kutoka katikati ya vita, wakaleta habari ili zituwezeshe kujua tunavyoweza kusaidia ukombozi wa nchi zile.

Mheshimiwa Spika, sasa leo watu ambao wamesaidia sana katika kutusaidia kupambana na ukoloni kule Msumbiji, Zimbabwe, Namibia, Afrika ya Kusini na maeneo mengine. Leo sisi hapa tunakuja Bungeni, tunasema hawa ndio wanakata watu vidole; hii dunia itatushangaa, hawa watu walikwendaje tena wakafika mpaka kwenye kukata watu vidole kutoka kwenye ukombozi wa Afrika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana mambo haya kwa sababu ni ya kiusalama, mara nyingi huwa hayazungumzwi katika Bunge wala hadhara. Nchi nyingi huwa mambo haya yanazungumzwa katika Kamati *Level* ya Bunge na hayapewi *coverage,* lakini hapa inabidi tujibu maana mmeyapa *coverage.* Kwanza mmeushtaki Usalama wa Taifa, halafu mmewapa *coverage,* magazeti sasa yote yanasema. Kwa hiyo, inabidi sasa tufuate hivyo hivyo tuwaeleze.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha ukoloni, wamefanya kazi nzuri sana, lakini vile vile mwaka 1980 kuna watu wabaya walitaka kubadili historia ya nchi yetu, wakataka kuleta uhaini. Ni Idara hii ambayo iliwabaini watu hao na ikazuia historia ya nchi yetu isibadilike. Ni hawa hawa, wanafanya kazi yao *quietly,* lakini wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka 2005/2006, wote mnajua kulitokea uhalifu mwingi sana na mabenki yalikuwa yanaporwa miaka ile ya baada ya uchaguzi wa mwaka 2005. Idara hi chini kwa chini ilifanya kazi na kwa kusaidiana na Polisi, mtandao wa majambazi hawa ulikamatwa na amani ikarejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hawa watu wanaitwa Usalama wa Taifa; sasa watu hawa tena waache hii kazi ya kuleta amani waende kukata vidole vya watu, itakuwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hii vita ya dawa za kulevya, wanafanya kazi vile vile chini kwa chini na wanatoa taarifa juu ya mambo haya yanayohusu dawa za kulevya. Hii Idara inafanya kazi, tofauti yake ni kwamba, mafanikio yake hayajulikani kwa sababu, hawatangazi na wala hawajitangazi kwamba, sisi tumeweza, aaa, wao ni kimya kimya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme, hata hayo mambo ya ugaidi ambayo yanafanyika katika nchi nyingine, wao wanafanya kazi, hata mashambulizi yale yaliyotokea hapa nchini kutokana na kushambuliwa kwa

Ubalozi wa Marekani miaka ile, walifanya kazi hao hao, wakagundua watu waliohusika katika jambo hili. Kwa hiyo, hawa watu wana kazi muhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini moja ambalo ningependa niliseme ambalo linatuhusu wenyewe hapa hapa Bungeni, ni kuwa, mwaka 2008, nadhani ilikuwa mwanzoni, Kiongozi wa shughuli za Upinzani hapa Bungeni, alikwenda Tarime kwenda kumzika Marehemu Wangwe. Wakati huo Marehemu Wangwe amekufa na watu wengi kule Tarime wakawa wanaamini kwamba, Mheshimiwa Mbowe na Chama chake wamehusika. Kwa hiyo, alipokuja kwenye msiba kulikuwa na genge la watu wana mapanga, wanasema tunataka kusema naye.

Mheshimiwa Spika, mimi sielewi unavyoweza kusema na mtu na huku una panga, lakini Idara hii ndio iliyotoa Taarifa kwamba, kuna hatari kwa hiyo ikafanya utaratibu kwa kushirikiana na Polisi ikawatorosha Viongozi wale watoke pale salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nauliza, kama wao kweli kazi yao ni kupinga Wapinzani na kuwakata vidole, si wangemwacha Mheshimiwa Mbowe pale, ashughulikiwe na marungu na mapanga ya Tarime. Maana wao wangekuwa hawamo, wangesema ni watu wa Tarime ndivyo walivyo, wamewakata na Mheshimiwa Mbowe amefia pale pale na ingewezekana, maana ilikuwa hatari, mimi nilikuwepo; kwa hiyo, nadhani tuwe makini kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisemi Serikali isilaumiwe, hapana. Serikali inaweza ikalaumiwa mahali ambapo inastahili kulaumiwa, lakini tuwe tunafanya uchunguzi wa kina. Maana unaweza ukajiuliza hivi kweli Idara hii iende imtese Kibanda, lakini Kibanda ni nani katika Upinzani wa Tanzania? Kibanda, anaweza kuteswa kwa nini? Maana wangesema ni Mheshimiwa Mbowe au wakasema ni Dkt. Slaa, ndio Wapinzani wanaojulikana hapa; sasa waende kumtesa Kibanda wa nini na Kibanda ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo hayafai na hatutaki kurudisha lawama tukawa na sisi tunafanya vile vile. Lakini Kibanda huyu, alikuwa Mhariri wa gazeti la Tanzania Daima, ambalo ni mali ya familia ya Mheshimiwa Mbowe. Siku zake za mwisho aliandika *article* ambayo inapingana na Sera ya mwenye gazeti, halafu ndio akahama akaenda gazeti lingine. Sasa Serikali, ingemfuata kwa jambo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisemi na wao walimfuata, lakini tutafute aliyemfuata basi, ili tujue ni nani hasa? Labda alipoona amehama, akataka na yeye afanye, ili wasingiziwe na wao kwamba, alipotoka kwenye gazeti, wao ndio wamemfuata; inawezekana hilo likatokea duniani. Kwa hiyo, nafikiri tuwe waangalifu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie kwa kutoa ushauri tu kwamba, sisi wote ni wanachama wa Vyama vya Siasa na Vyama vya Siasa vyote vina mikakati ya kuchukua dola, hilo halina siri. Ukiunda Chama cha Siasa hatima yake unachotaka ni kuchukua dola, si ndio? Kama huchukui dola unaunda cha nini? Kwa hiyo, unakuwa na mikakati.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu wa CHADEMA nao wamekuwa na mikakati mara Sangara, mara nini; wana majina mengi, yamekuwa yanabadilika badilika, nafikiri Sangara lilishakufa. Sasa ni *M4C, M4C,* nayo sijui kama bado ipo au na yenyewe inaelekea kufa, sielewi, lakini nataka niseme kwamba, kama unafanya kazi yako kwa kuzingatia Sheria na hutaki kufanya siasa za nguvu, hutaki siasa za jazba, siasa za kutaka kuangusha Serikali, Idara ya Usalama wa Taifa haina shughuli na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukifanya njama ya kusema nchi haitawaliki, unataka fujo, Idara ya Usalama wa Taifa itakufuata ndio kazi yake kuhakikisha kwamba, amani inakuwepo. Wewe kama unataka kuindoa, Idara ya Usalama wa Taifa, iache kuja kukuuliza kulikoni? Ikuache tu ufanye fujo mpaka lini? Halafu unasema tunazuiwa siasa, siasa zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana siasa tunapingana kwa hoja, hatuwezi kupingana kwa mabavu, hatuwezi kupigana, hiyo sio siasa. Siasa ni hoja, unakuja hapa unatwambia kwamba, ninyi bwana mliahidi hiki, hamkufanya au ufanyaji wenu hautofautiani na wa kwetu; unasema tungekuwa sisi tungefanya hivi, *alternative.* Aah, sasa *alternative,* hakuna, ni maandamo tu ni fujo na kupigana, sasa usalama wa Taifa lazima utakuja nyumbani kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hilo suala, sasa nizungumze kazi ya maendeleo. Maana na sisi tusije tukawa *driven* na *agenda* ambazo hazipo, tukaacha kuzungumza maendeleo, tukawa tunazungumza haya mambo yanayosemwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango tumepokea mawazo, kwanza kutoka kwenye Kamati, chini ya Mheshimiwa Pindi Chana, yote tunayafanyia kazi, tunayakubali, wala hatuna tatizo; lakini liko jambo moja tu ambalo ningependa kulijibu ambalo limeandikwa kwenye Kambi ya Upinzani. Wao wanasema sisi tumeunda kitu kinaitwa *PEMANDU*. Sisi hatujaunda *PEMANDU,* tumeunda kitu kinaitwa *Presidential Delivery Unit,* lakini tumejifunza kutoka *PEMANDU,* ya Malaysia. Sasa wanasema mbona tumebadilisha malengo?

Mheshimiwa Spika, nataka kuwambia Malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano yamebaki pale pale, hakuna kilichobadilika. Malengo yetu ya Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano, yameelezwa ni miundombinu ambayo ipo, ni kilimo, viwanda, rasilimali watu na huduma za fedha, biashara na utalii. Hii rasilimali watu inajumuisha elimu na kilimo kuna maji. Kwa hiyo, hakuna kitu ambacho kimebadilika. Isipokuwa, labda tunachanganya na hiki kitu kinaitwa *Lab* ambayo ndiyo maandalizi ya kuundwa kwa kile chombo, lakini kazi ya hii inayoitwa *Presidential Delivery Unit* ni tofauti nna kazi inayofanywa na Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa kazi yao ni kufanya *lab,* wanachukua yale mapendekezo ya mpango na

vipaumbele, wanavitazama kiutekelezaji; wanasema kuwa, mwaka huu tunaanza na nini. Kwa mfano, katika *lab* zilizopita wamechukua miundombinu, ingawa barabara zipo, lakini wao wamechukua nishati na uchukuzi kwamba, ndio vipewe kipaumbele kwa mwaka huu kwa sababu, tunataka reli na tunataka kupanua biashara na nchi zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, tunataka umeme uweze kuongezeka ili kufikia lengo la *Megawatt 2,780* au 3,000 kadiri ilivyo. Sasa wanachukua ile wanasema tunafanya nini kufika hapo, ni jambo la kiutekelezaji kabisa na tunashirikisha sekta binafsi na mashirika mengine ya Kimataifa kwenye zile *lab,* ili kupata mawazo halafu tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, kazi yao ni hiyo, kuandaa viashiria na kupima matokeo ya utekelezaji, inaitwa *Key Indicators* na Mfumo Madhubuti wa Uwajibikaji na kuweka mfumo wa utekelezaji na utatuzi wa changamoto. Hii sio *Policy* kwamba, inafuata tu makosa; inakwenda inamuuliza anayesimamia utekelezaji, matatizo yako ni nini, anaeleza, inamsaidia kutatua matatizo yale, utekelezaji unakwenda kwa wakati; hicho ndicho chombo.

Mheshimiwa Spika, sasa wanasema hiki chombo hiki, Rais amekwenda akakiona Malaysia, sasa akienda tena kwingine akiona atafanyaje? Aah, bwana wee, hiki chombo hakiko Malaysia, ukienda *South Africa,* utakikuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Uingereza ya Tony Blair, alikuwa na kitu kinafanana na hiki hiki, kina-*push* tu ile *agenda* kwa wakati, ili kwenda kwa *speed* zaidi. Tunasema miradi iende kwa *speed* na tupate *value for money,* si ndivyo tunavyokubaliana? Hiki chombo kitatusaidia kwa kazi hiyo, hasa kwenye miradi mikubwa. Ile miradi midogo itaendelea kusimamiwa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, halafu tatizo la ajira limeelezwa na tunajua kwamba ni kubwa. Mpango huu unahimiza uanzishwaji wa viwanda, ambao kwa kweli, vikianzishwa viwanda, vinaweza vikatupunguzia tatizo la ajira, lakini ni

tatizo ambalo haliko Tanzania peke yake. Nchi zote zinazotuzunguka, hata zile zilizoendelea zina *problem* inayofanana na hii kwa sasa. Kwa hiyo, hili siwezi kulielezea sana, tunalisimamia.

Mheshimiwa Spika, halafu wachangiaji wengine ambao walisema, hiyo ilikuwa ni Upinzani, akina Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, wote walisema, Serikali huwa inapandisha mishahara kwa ajili, ya kudhibiti mfumuko wa bei. Hii ni sawa, lakini mfumuko wa bei huu ni kitu ambacho huwezi kukizuwia, sio *static;* unapanda na kushuka, kulingana na mazingira.

Mheshimiwa Spika, ukilima chakula kwa wingi sana mfumko unashuka, ukipata ukame mfumko unapanda. Au chakula chenu kikinunuliwa na nchi za nje chote ninyi mkaishiwa, unapanda wa kwenu wa wale waliokinunua unashuka. Kwa hiyo, ni kuongeza uzalishaji tu, ili tuweze ku-*balance equilibrium* ya uzalishaji na mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mabumba, alikuwa anazungumzia Dira ya Taifa, lakini anasema haitekelezeki; hiki kitu kinatekelezeka, ndio inakwenda na Mpango huu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vincent Nyerere, yeye alikuwa anatushauri kwamba, tuwahusishe wananchi katika upangaji wa mipango; tunakubali. Vile vile alikuwa amesema katika kupanga mipango, tuwe tunapanga kwa kuzingatia Ilani za Vyama vingine, sisi tunawashirikisha wenye Ilani zao. Hata huu mpango tunaouzungumza tulishirikisha kila mtu, kwa hiyo, kama una mawazo yanafanana na Ilani, yalete tu, hakuna mtu anakataa Ilani yako, isipokuwa yawe kweli yanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kukataa mawazo, Serikali, inaweza kukataa tabia yako, lakini haiwezi kukataa mawazo yako. Kama tabia yako ni mbaya, lakini mawazo yako mazuri, tutachukua mawazo, tutaacha tabia yako mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chacha Mariba, alikuwa amezungumzia Mpango wa Maendeleo na anauliza vipaumbele ni vipi mwaka huu? Mwaka huu, vipaumbele vitakuwa vile vile vilivyoko katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa sababu, kila mwaka vinaendelea mpaka mpango uishe.

Mheshimiwa Spika, pia aliuliza mpango unasimamiaje rasilimali za Taifa; tunazisimamia kwa kadiri tunavyoweza na kwa kweli, rasilimali ziko nyingi na ni lazima iwepo Sera, inayosimamia rasilimali hizi.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya fedha vya maendeleo vitakuwa ni vile ambavyo siku zote tunavyo. Serikali, Sekta Binafsi, *PPP* na mikopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali, ina mpango gani mahsusi, kuhakikisha rasilimali za Taifa zinawanufaisha Watanzania? Tunatengeneza Sera zinazosimamia migodi, Sera inayosimamia Nishati, Sera zinazosimamia rasilimali nyingi sana ambazo ziko nchini, ili ziweze kutumika. Tulikuwa na migodi hapa ambayo ilikuwa hailipi kodi, sasa wameanza kulipa baada ya kubadili Sera na Sheria, kwa hiyo, tunapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyangwine, alikuwa amesema tunashirikishaje *Great Thinkers* katika utayarishaji wa Mpango? Tunashirikisha watu *private sector,* kwa hiyo, yeyote anayejifikiria kama ni *Great Thinker,* anakuja tu anashiriki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika, alikuwa anasema, yeye alileta kwa maandishi kwamba, ile Sheria Namba 11, marekebisho yake yamechelewa. Nilishaeleza katika Hotuba yangu kwa nini tumechelewa, tunataka kupata mawazo zaidi ili tusipitishe Sheria, halafu kesho tukarudi tena kuja kufanya mapitio mapya.

Mheshimiwa Spika, pia alisema juu ya ombi la kupatiwa majibu mahsusi ya hoja alizozitoa wakati wa kujadili, lakini nataka kumwambia Mheshimiwa kwamba, tulishatoa

kitabu ambacho kilikuwa na majibu yote ya mambo ambayo tuliyasema katika Kikao cha Bunge. Kama hakukipata, nitampa, ili aone majibu gani tulitoa; tena nitampa leo hii hii wala sio kesho, kiko pale, nitampa.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kidogo masuala machache yaliyosemwa na *Opposition* tena, haya yalishajibiwa hasa ya kuhusu mchakato wa Katiba. Wakati wenzetu wa CHADEMA, *CUF* na *NCCR* walipokuja kwa Rais na mimi nilikuwepo na wao wenyewe ni mashahidi, Rais alikuwa *flexible* alisema, haiwezekani tukafika mahali, tukatunga Katiba kabla hatujafanya marekebisho yanayohusu nani anahudhuria kwenye Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, sasa suala ni *timing,* tunafanya lini, lakini kabla Bunge la Katiba halijafanyika, lazima tupitishe sheria ili tujue nani anakuwa Mjumbe katika lile Baraza. Vile vile itabidi tupitishe sheria ambayo inatu-*guide* juu ya *referendum* kwa sababu hatuna sheria ya *referendum* sasa hivi, hiyo ya *referendum* vile vile itapitia hofu zile zilizoko kwamba Tume ya Uchaguzi labda ina upungufu, yote tutayazungumza wakati tunazungumza juu ya *referendum.* Kwa hiyo kama ni hayo, sikuona kama kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu yeye alisisitiza sana uchaguzi wa Mabaraza ya Wilaya ya Katiba kwamba, wanaochaguliwa watakuwa CCM, mimi ni CCM, lakini Bunda wamechagua mimi wala sikushughulika, kwa sababu Tume ilisema hayo siyo mambo ya Chama, ni kwamba mtu yeyote anasimama kwenye kijiji wanamchagua.

Mheshimiwa Spika, sasa sijui tena wana-CCM wangapi wamechaguliwa huko kwetu, sielewi, sijafuatilia maana sikuona kwamba ni jambo la chama, maana lingekuwa la chama, tungesema mgombee, mje kwenye Kamati tuwachuje halafu ndiyo mkapigiwe kura, hatukufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata wale wanaotoa takwimu za

Vyama, wanataka kuiweka ile Tume kwenye matatizo, wala hawakusema mambo ya vyama, wao walisema wasimame watu wagombee na utaratibu wao umewekwa. Sasa kama kuna mahali ambapo mambo hayakwenda vizuri, Tume imeshatangaza kwamba, ikipata habari itarekebisha hapo ambapo mambo yamekwenda vibaya.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo Tume hii kwamba inaweza ikakutana, ninavyoijua inavyo-*comprise,* halafu ikafanya mambo ya CCM ni ngumu, maana kuna wa Vyama vya Upinzani wengi na wengine hawana vyama kabisa na wengine wanatoka Makanisani wako mle. Kwa hiyo, nadhani wamepitisha na nafikiri tuendelee nao hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa yako masuala yanayohusu *TASAF* kwamba watoe elimu kwa wananchi kabla ya kuanza utekelezaji. Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati na sisi tunakubaliana na ushauri wake. Kamati inashauri *TASAF* iweke usimamizi mzuri wa fedha ikiwa ni pamoja na taasisi hii kusimamia fedha zake yenyewe. Hili tunalizingatia, sasa tunaanza kupeleka msimamizi mmoja katika kila Halmashauri ili taarifa ziwe zinawahi kufika Makao Makuu ya *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye alitoa ushauri, amekuwa akifuatilia kwa karibu sana utekelezaji wa miradi ya *TASAF* na sisi tunamshukuru kwa ufuatiliaji wake. Kule kuna jumla ya miradi kama 49 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.9, kati ya miradi 43 ambayo imekamilika. Kwa hiyo, kwa kweli tutaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Ole-Medeye katika kufanya kazi hiyo ya *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Amos Makalla, alisema Jimbo lake kupitia Mfuko wa Jimbo tumeanza kujenga masoko katika vijiji, sasa anasema anataka *TASAF* iingie ili iweze kusaidia. *TASAF* namba mbili imekwisha, *TASAF* namba tatu ina taratibu zake ambazo zitakuja kuelezwa mpaka kwa Kata. Tunatoa semina sasa hivi mpaka kwenye vijiji ili wenye vijiji wajue maana tulikuwa tunatoa semina mpaka Wilayani, wenye Wilaya hawaendi. Sasa *TASAF*

tunaunda mfumo ambao utatoa taarifa kabisa na mafunzo mpaka kwenye kijiji ili wenye kuhudumiwa waweze kuhudumiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ikiwa *TASAF* na masharti yake yataoana na masoko yale yakawa hayajamalizika na kama kweli wananchi wale wanadhani masoko ndiyo mambo muhimu yanayowahusu, basi tutazungumza na *TASAF* tuone cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Lwanji alizungumza *TASAF* inafanya kazi nzuri na sisi tunamuunga mkono katika jambo hili kwa sababu hata *TASAF* yenyewe siyo kwamba haina matatizo, yako matatizo yako maeneo mengine haikufanya vizuri, lakini ukichukua kwa ujumla hivi kwa nchi *TASAF* imefanya vizuri kwa kweli ukiondoa matatizo ya hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Moza amesema *TASAF* imetekeleza miradi mingi ikiwemo ya shule na ya afya, lakini uongozi wa Halmashauri hautoi msaada kwa Kamati za Usimamizi, ndiyo maana sasa tunakwenda kutoa mafunzo mpaka chini ili tuweze kushirikisha watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sylivester Mabumba yeye anasema, mradi unaotekelezwa pale kwake ni mmoja na nadhani kuna haja ya kumsaidia zaidi, hilo nalo linaweza likatazamwa.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nizungumze mambo ya MKURABITA. Mwenyekiti wa Kamati anasema MKURABITA haijulikani na sisi tunakubali tunadhani tutaanza kazi ya kuhakikisha kwamba inafanya kazi vizuri. Lakini tatizo la MKURABITA ni kwamba, kule ambako inakwenda kufanya kazi, yenyewe haina fedha nyingi, bajeti yetu tunayopata ndani kwa mwaka ni bilioni tatu.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani MKURABITA ikapima vijiji vya Tanzania, wao wanakwenda wanapima *sample,* halafu wanaacha vifaa pale kwenye Wilaya ili Wilaya kwa

kutumia wataalam au vijana ambao wamefundishwa pale na MKURABITA waweze kuendeleza. Lakini fedha ndiyo imekuwa tatizo, ndiyo maana tunafikiria sasa kuunda Mfuko wa Maendeleo wa Upimaji yaani *revolving fund* ili iwe ina *revolve,* wanapima wanaendelea na kila mwaka mpaka tufike tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika nadhani yeye alikuwa anazungumza juu ya Kimara Baruti ambako tulianza kupima. Tatizo letu pale Kimara Baruti na kwenye miji ni kwamba, ushirikishwaji ni mkubwa kabisa, kwa sababu sisi hatuna hela za kulipa fidia. Kwa hiyo, ni mpaka tukubaliane na wale watu na wale watu wenyewe waseme mimi nitabomoa nyumba ili barabara ipite, sasa ushawishi huo ni mgumu ndiyo maana. Lakini tumemaliza kazi na sasa hivi tunaandaa hati kwa ajili ya kuwapa watu wa Kimara Baruti.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Moza Abeid alisema, dhana ya Mwongozo wa MKURABITA haijaeleweka. Nafikiri tutaiandika na tutawaambia MKURABITA watoe maelezo zaidi au kwa maandishi au ikibidi watoe hata semina mbalimbali ili kuwafanya watu wengi zaidi wajue tunaelekea wapi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mabumba wa Dole alisema MKURABITA imepata mafanikio mangapi. Urasimishaji wa ardhi mijini na vijiji umefanyika katika Halmashauri za Wilaya 41 na miji minane na jumla mashamba 86,732 na viwanja 9,614 vimepimwa. Aidha, mipango ya matumizi bora ya ardhi imeandaliwa katika vijiji 176 ambapo urasimishaji umefanyika. Vile vile maabara za kumbukumbu za kijiografia zimeanzishwa katika Halmashauri za Wilaya 41 ambapo urasimishaji wa ardhi mijini na vijijini unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Lwanji alizungumzia hati miliki na mabenki yanafanya ngumu, bado jambo hili tunalishughulikia, lakini mabenki mengine yanatoa

kama CRDB, wao hawana matatizo, lakini tunaendelea kuwasiliana tuone kitu gani kinaweza kufanywa kama ni sheria au ni makubaliano na mabenki.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria inasema, Mfuko uongezewe fedha. Sasa hivi hatuna jibu kwa sababu fedha tulizonazo ndiyo hizo. Pia wanasema Mfuko uendelee kukopesha, hapa wanazungumza Mfuko wa Rais wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, huu nao ulikuwa na matatizo, sasa tunaujenga upya na tunataka kubadili kazi zake; badala ya kwenda kutafuta watu vijijini tunataka waende walenge kwa mafundi ambao wamepita *VETA* ili Mfuko huu uwakopeshe wale ambao tayari ni *skilled* ili waweze kujiajiri, ndiyo mpango ambao tunajaribu kuufanya sasa kupitia Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Angellah Kairuki naye alizungumzia masuala ya Mfuko ule, akasema ni muhimu na huduma za kifedha na mafunzo ya wajasiriamali, tunazingatia ushauri.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie mambo ya utawala bora. Kwanza kwa muda huu uliopo sitaweza kueleza nini maana ya utawala bora, maana kwa kweli huo utawala bora ni mrefu, lakini nitazungumzia zaidi hoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge imezungumzia zaidi shughuli zinazohusu Baraza la Mawaziri, kuboresha utendaji kazi na wao wamesema kwamba, ni vizuri tuwe na mfumo ambao unaweka mikataba baina ya Mawaziri, tumeanza. Zile Wizara sita ambazo zimefanyiwa *lab,* zote wamesaini mkataba na Rais kuhakikisha kwamba kazi ile inafanyika na kile chombo kile kinafuatilia. Ukishindwa wanakwambia basi mpango ume-*fail* na wewe una-*fail* nao. Kwa hiyo tumeshaanza, nia ni ku-*push* zaidi kupata kitu kinaitwa *big results now.*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani katika suala hili, inazungumza kwa muda mrefu sana dhana ya

utawala bora imekuwa ikionesha kama inapaswa kutekelezwa kwenye ngazi za Serikali Kuu. Wanachosema ni kwamba, kule chini bado haitekelezeki vizuri. Kwa kweli nataka kukubaliana nao, kule kuna matatizo kidogo, wakati mwingine virushwa rushwa vidogo dogo vile ndiyo vinatuletea shida. Nadhani utawala bora lazima umulike mpaka kule chini kabisa ili tuanze kuona jinsi wananchi wa kawaida wanavyoweza kunufaika na huduma za Serikali zinazokwenda huko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hamadi wa Magogoni yeye alieleza mambo ambayo kwa kweli sina majibu nayo kwa sababu ni kero za Muungano, hizo zitazungumzwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, tunamwachia tena mwenyewe yupo hapa hapa atazieleza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika alizungumza juu ya mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliyotajwa kwenye aya ya kumi na tatu ilishughulikia nyaraka kuhusu mapitio ya tathmini, upembaji na viwanda vilivyobinafsishwa, anataka kujua tunafanya nini, hili tunamwachia Waziri wa Viwanda ndiye anaweza kuja kukupa jibu la kitaalam zaidi kuliko Ofisi ya Rais, Ikulu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika vile vile alikuwa amezungumzia habari ya ujenzi wa Ofisi Kuu ya TAMISEMI, ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Jimboni Ubungo ya kwenda pale, jana alikuwa mkali kweli anasema, hata hili nalo limeshindikana, hii si ni ratiba, mikutano inaahirishwa itakuwa *appointment* na Rais. Kama Rais hayupo sasa utakwenda kuzungumza na nani?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika hili ataitwa tu akae chonjo watamwita. Jambo la maji si ndiyo hilo walilopatana, hilo halina *problem,* tutawaambia watu wanaomsaidia Rais katika *program* kwamba, bado kuna ahadi ya kwenda kufanya mkutano na watu wa maji kule Ubungo.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuongea ni

Mariam Salum Msabaha, amezungumza migogoro ya ubadhirifu na tabia ya Watendaji wa Vijiji kutoheshimu utawala bora, hilo nimeshalieleza kwamba itabidi kwa kweli tutazame zaidi chini ili mambo yaweze kwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Pindi Chana alizungumza kwamba, TAKUKURU iongezewe uwezo wa kifedha. Serikali inatambua kwamba bajeti ya TAKUKURU ni ndogo ukilinganisha na majukumu yake. Hata hivyo, Serikali itaendelea na juhudi za kuwezesha TAKUKURU kupata bajeti ya kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, pia TAKUKURU kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu itahakikisha somo la Uraia na lenyewe linakwenda ili vijana waweze kujua madhara ya rushwa. Serikali itatoa kibali kuajiri watumishi 394 mwaka huu na kibali chenyewe kwa kweli kimeshatolewa tayari na Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, taasisi ipewe nafasi ya kuweza kufungua Ofisi. Ofisi inafunguliwa Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Mkinga kwa mwaka huu na kazi hiyo inaendelea. Taasisi ishughulikie masuala yote ya rushwa kikamilifu na tafiti zifanyike kutoka nchi mbalimbali kuona jinsi chombo hiki kinavyofanya kazi. TAKUKURU wenyewe wanatembelea nchi hizi, kwa hiyo, wanajua kinachoendelea katika nchi hizi.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU itajwe katika Katiba ya nchi. Hilo tunawaachia wasimamizi wa Katiba. TAKUKURU ibuni mbinu mpya za kuongeza juhudi, mbinu mpya zimekuwa zikibunuwa na ndiyo maana tumefungua ofisi katika vituo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kahigi alizungumzia chunguzi za *EPA*, Meremeta, Uchunguzi na Ukaguzi wa Kituo cha Mbasi Ubungo. Kesi za *EPA* ziko Mahakamani, suala la Meremeta limeshajibiwa, uchunguzi wa Kituo cha Mabasi, Ubungo liko Mahakamani, suala la UDA na lenyewe liko Mahakamani, sasa mimi sina cha kuongeza.

Mheshimiwa Spika, maafa ya kuanguka kwa majengo, waliohusika wamepelekwa Mahakamani. Nadhani baada ya hapo TAKUKURU itaingia ili kujua kama kuna rushwa ndiyo iliyosababisha hali hiyo kutokea.

Mheshimiwa Spika, ilisemwa pia umma haujaridhika na juhudi zinazofanywa na Serikali katika utendaji mzima wa TAKUKURU. Hadi kufikia Aprili jumla ya kesi kubwa 54 zinaendelea Mahakamani na ziko katika hatua mbalimbali. Sasa ukishakamata, ukapeleka Mahakamani, inabidi ungoje uamuzi wa Mahakama katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Mnyika tena alisema uchunguzi wa mradi wa maji Ubungo. Nadhani umekamilika, jalada limewasilishwa kwa *DPP,* nadhani hapa alikuwa anazungumza uchunguzi wa madai ya ufisadi katika miradi ya maji na jalada liko kwa *DPP*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha alizungumza kwa nini TAKUKURU inapata taarifa za vitendo vya rushwa, lakini inashughulikia rushwa ndogondogo, wamesema na kubwa zimo humu, kwa hiyo siyo ndogo tu. TAKUKURU yenyewe ni kubwa, haiwezi kungojea ndogondogo peke yake, ndogo zipo nyingi, tena kule vijijini ndiyo hawajafika kabisa, watawaambia watu wao wa Wilayani watie mkazo zaidi kwa zile za Wilayani.

Mheshimiwa Spika, kusema ukweli mambo yaliyosemwa ni mengi na yanajirudia, kwa hiyo ningependa Sekretarieti ya Maadili liwe ndiyo jambo langu la mwisho. Kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inazungumzia suala la maadili lijumuishwe na masuala mengine mbalimbali na siyo masuala ya mali peke yake.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, fungu la 18 labda tutajaribu kurekebisha wakati tunaiunda upya Sekreterieti hii. Sekretarieti hii itakayoundwa upya ni vizuri iwe Tume kuliko kuwa Sekretarieti maana wanasema haina meno na nadhani kweli haina, ingefaa iwe na meno ili iweze kuuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, napenda kutumia nafasi hii kusema kwamba tumejitahidi na tutaendelea kujitahidi, lakini nataka katika masuala ya msingi kama yale ya udini, Bunge lako Tukufu lijielekeze katika kutafuta *solution* zaidi kuliko kuchochea. Bunge hili lazima liwe chombo cha uongozi, kisaidiane na Rais katika kurudisha nchi yetu kwenye umoja. Pia suala la Usalama wa Taifa nadhani nimelieleza vya kutosha na yote ni mambo ya msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge msije mkaingilia mshahara wa Rais hapa, *Vote* 32 ndiyo itahusika na hawa jamaa, lakini mengine ni mambo ya Rais.

**Fungu 9 - Bodi ya Mshahara na Maslahi Katika Utumishi wa Umma**

Kif. 1001- *Administration and Human Resource Management... ... ...* .Sh.1,336,604,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba ufafanuzi tu kwenye kifungu hicho, kasma ya 229900, *other operating expenses* ambazo zimepungua kutoka mwaka wa fedha uliopita milioni 95 mpaka sasa milioni 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba, Bodi hii ni muhimu sana na ndiyo ambayo inahusika na kupendekeza kwa Serikali

mipango yote inayohusiana na nyongeza ya mishahara na maslahi kwa wafanyakazi. Sasa ni wazi Bodi hii ni muhimu ikawezeshwa ili iweze kutimiza wajibu wake ipasavyo. Ningependa kupata ufafanuzi ni kwa nini fedha za matumizi mengineyo ambayo ndiyo zilikuwa zinatumia kutekeleza baadhi ya kazi maalum zimepungua kutoka milioni 95 mpaka milioni 28.

**SPIKA:** Mnyika umesema kifungu gani samahani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kifungu cha 1001, kasma 229900, *Other Operating Expenses.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa gharama zimepungua kwa sababu katika kifungu hiki, tumeweka gharama za mazishi na mambo mengine. Tulikoongeza ni katika *Office and General Supply* ambapo ni ununuzi wa vifaa na vitu vingine. Mwaka jana kama ataangalia ilikuwa mambo yote haya yanakaa kwenye kifungu cha utawala, lakini sasa hivi tumegawanya mpaka kule chini. Akienda kuangalia kwenye *TSD,* tutakapofika huko ndiyo tutaona hela nyingi ambazo ni kwa ajili ya Wilaya mbalimbali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*... ... .Sh. 132,126,000/=
Kif. 1003 - *Planning Unit* ... ... ... ... ... ..Sh. 26,900,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... ..Sh. 33,400,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Legal Services* ... ... ... ... ... Sh. 169,300,000/=

**MHE. CHARLES P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mshangao kidogo kwenye hiyo *sub-vote* 1005 , kasma 220,309, kadri ninavyoijua sekta hii, kuwapangia shilingi milioni

tano kwa mwaka mzima, hayo ni mafuta ya namna gani. Naona ni kiasi kidogo mno kwa kadri ninavyojua miondoko ya watu hawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimepangiwa fedha ndogo kwa sababu Idara hii haina gari, kwa hiyo inaazima gari kutoka kwenye Idara nyingine, wao wanachangia tu mafuta kidogo. Kwa hiyo, mara nyingi wanatumia magari ya Idara nyingine, hasa Idara ya Utawala.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Information Communication Technology* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh.11,500,000/=
Kif. 2001 - *Productivity and Research Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 306,312,000/=
Kif. 2002 - *Remunerations Unit* ... ... ... ... ... .Sh.197,740,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 20 – OFISI YA RAIS, IKULU**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resource Management* ... ... ..Sh.9,248,595,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 30 – OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resource Management* ... ..Sh. 238,219,898,000/=

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 229900, *Other Operating Expenses*, nataka

maelezo, ukiangalia fedha zinazoombwa mwaka huu, zinazidi kwa kiasi cha shilingi bilioni 23, uki- *compare* na *last year*, naomba maelezo ni kwa nini kuna ongezeko kubwa namna hii.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Nchi, umekipata, kifungu kidogo 229900, kinaitwa *Other Operating Expenses*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka kutokana na ongezeko la fedha za uendeshaji; ongezeko la mshahara kwa kipindi cha Julai, 2012 na ajira mpya kwa TAKUKURU katika kipindi cha mwaka 2013/2014 kama tulivyoambiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu hicho hicho, hapa nina vifungu viwili, kimoja ni hicho 229900, wakati Waziri anajibu, amezungumzia ongezeko la mishahara. Sasa nataka nijue, kama analiambia Bunge hili Tukufu; kwamba hizi *Other Operating Expenses* ambazo zimeongezeka kutoka bilioni 192, mpaka bilioni 215, linahusika na mishahara. Kama sivyo, atupe uchambuzi wa hizi fedha, zinatumika kwa kitu gani?

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kifungu 220700, fungu hilo hilo, kuhusiana na *Rental Expenses*. Inaonekana kwamba, hiki kitengo kinakodisha, ama kina hela za pango ambazo zinakuwa ni mabilioni kila mwaka na sasa hivi ni bilioni 5.3. Sasa nataka nijue hizi *Rental expenses* zinaka-*cover* vitu gani hasa na hatuwezi kuwa na majengo yetu ili kuweza kuepuka hizi gharama. Kwa hiyo, naomba *clarification* katika hayo mambo mawili.

**MWENYEKITI:** Hiki cha kwanza 229900, naomba m-*elaborate* swali alilouliza Lyimo, kwa sababu mkisema nimpe huyu mawili nitamkatalia. Naomba mrudie maelezo aliyouliza Lyimo halafu mjibu ya Halima.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, Kifungu hicho sasa

nimekiona, ni kwamba kifungu hicho ni mishahara na pamoja na shughuli za kupambana na rushwa.

**WABUNGE FULANI:** Hapana, hapana.!

**MWENYEKITI:** *Other Operating Expenses!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Ndiyo nawaambia hivi, tumeandika kwamba shughuli za Kitaifa, ukiangalia kwenye randama, lakini ni kwa ajili ya kupambana na rushwa hilo ni moja, lakini na mishahara ipo humo humo. Mishahara ya Usalama wa Taifa haiko kwenye *sub-vote* yoyote ile.

**WABUNGE FULANI:** Aaa!

**MWENYEKITI:** La pili alilouliza Mheshimiwa Halima Mdee!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu *Rental Expenses*, tuna...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti)*

**MWENYEKITI:** Naomba tuwe tunasikilizana, tatizo letu ni hilo, bahati mbaya ukishasema hivi wala hakuna anayekusikiliza. Haya eleza!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Rental Expenses* deni la Taifa, ambapo nyumba za Usalama wa Taifa zilijengwa na *NSSF*, kwa hiyo, tunalipa kila mwaka deni hilo, pamoja na kukodishwa nyumba za wafanyakazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit... ...* Sh. 433,360,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning... ... ... ... ...* Sh. 421,028,000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho, kifungu namba 1003 kasma 227500, *Other Supplies and Services*; mwaka jana hapakuwa na pesa yoyote lakini mwaka huu wametenga milioni moja, ningeomba ufafanuzi kwa nini mwaka jana hawakuwa na hela yoyote, sasa hivi kuna milioni moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Vifungu vya *Other Operating Expenses*, huwa mara nyingi tuna weka kwa ajili ya *fumigations*, *fire* na vitu vinginevyo. Sasa kwa kuwa kila Idara inapangiwa kiasi chake, hicho kifungu ni kwa ajili ya mambo ya *fire*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit... ... ... ... ... ...*Sh. 289,671,000/=
Kif. 1005 – *Information and Communication Technology Unit ... ... ... ... ... ...* Sh. 367,132,000/=
Kif. 2001 – *Cabinet Secretariat ... ... ... ...* Sh. 1,375,808,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Government Communication ...* Sh. 440,270,000/=

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Nauliza pale kwenye *sub-vote* 2002, kifungu 210500, *Personal Allowances In-kind*, imetoka milioni 40 sasa hivi 156. Kwa nini posho hizi zinaongezeka na kama watu wanafanya kazi sana, kwa nini wasiajiri tu watu ili kupunguza posho nyingi?

**MWENYEKITI:** Mmekiona ni cha tatu kutoka juu *Personal Allowance In-kind*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Personal Allowance In-kind* ina vitu vingi; umeme, maji pamoja na simu kwa wale maafisa ambao ni *entitled*. Kwa hiyo, maafisa wale *entitled* wanapewa hizo *allowance* ambazo ni *non-discretion* ambazo pia ziko kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Mkosamali hesabu zilikuwa hazijaongezeka, nadhani ulisoma *figure* ya juu, lakini ya chini haijaongezeka.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Good Governance* ... ... ... ... ... Sh. 514,449,000/=
Kif. 2004 - *Public Service Appeal* ... ... ... ... Sh. 390,197,000/=
Kif. 2005 - *Public Sector Reform Coordination Unit*... ... ... ... ... ... Sh. 329,635,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 32- OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource Management* ... ...Sh. 11,512,779,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Taifa letu rushwa imekithiri kwa kiasi kikubwa na tunatambua kabisa kwamba, rushwa inaathiri maisha ya Watanzania kwa kiasi kikubwa na rushwa imekuwa ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Taasisi ya Kupambana na Rushwa imeshindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa sababu haiwezeshwi vizuri kifedha, lakini kikubwa sana pia Taasisi hii haiko kisheria, kwa maana kwamba haipo kwenye Katiba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kwa maandishi kwamba Serikali, itoe kauli leo kwamba taasisi hii ni lini itawekwa kwenye Katiba, lakini pia Taasisi huu ya Kupambana na Rushwa, iweze kupewa mamlaka ya kusimama yenyewe ikiwa inajitegemea. Kwa maana kwamba iwe na uwezo wa kukamata, kuchunguza na kushitaki. Tofauti na sasa hivi ambapo inakamata, inapeleka kwa *DPP, DPP* ndiyo aamue kwamba yupi apelekwe Mahakamani, yupi asipelekwe.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake sasa, Taasisi ya Kupambana na Rushwa, tunaona ina–*deal* na kesi ndogo ndogo, za dagaa, kesi kubwa za mapapa wanashindwa kuzifanyia kazi kwa sababu kwamba hawana mamlaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba serikali itoe kauli hapa kwamba, ni lini TAKUKURU itasimama kama mamlaka inayojitegemea na ipewe fungu la kutosha ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi ili rushwa iondoke Tanzania kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wote. Ahsante.

**SPIKA:** Naomba mwandike, halafu mtajibu; au mnajibu moja kwa moja? Lakini naomba mwandike.

Sasa namwita Mheshimiwa Profesa Kahigi! Baadaye kila mtu atajua katika eneo lake, nitakapoanza kuita, nitaita kutokana na walivyouliza.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kueleza masikitiko yangu, kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri Celina Kombani ambaye ni rafiki yangu, aliyotoa asubuhi; lakini kwa maadili niliyonayo ambayo wengi humu wanayatambua, sitamjibu. Nitajielekeza kwenye suala moja ambalo nataka majibu kutoka Serikalini, nalo linahusu Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ambao tumekuwepo tunafahamu kazi nzuri ambayo Usalama wa Taifa wanaifanya, hilo wala halibishaniwi. Pia tunafahamu

kwamba, nchi karibu zote, zina usalama wa Taifa ambao unashughulika na usalama nchini pia kulinda mipaka ya nchi, kuhakikisha kwamba, nchi haipati matatizo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Usalama wa Taifa hapa Tanzania inafanyika vizuri sana na kwa kazi hizo kwa kweli sisi tunaisifu na kuipongeza. Tunachokisema hapa, ni matukio ambayo yameanza kujitokeza hivi karibuni ambayo yanahusisha baadhi ya watu katika Usalama wa Taifa. Siyo Usalama wa Taifa kiujumla. Kwa sababu hapa lazima tutofautishe, hata katika Jeshi la Polisi kuna Askari Polisi wachache ambao siyo waaminifu wala siyo waadilifu, sasa huwezi kusema kwamba wote ni wabaya.

Hata katika usalama wa Taifa, kumeonekana dalili za namna hiyo. Kwa hiyo, swali langu ni kwamba, je, Serikali ina mkakati gani wa kisera, kwa watu ambao wametuhumiwa na wametajwa kwa majina? Washughulikiwe hawa, kwa sababu sheria inakataza, Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996, inakataza Usalama wa Taifa kufanya upelelezi wa kiufuatilizi, kwa watu ambao wako kwenye Upinzani au ni wanaharakati na wanafanya shughuli zao kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkakati gani wa kisera wa kuhakikisha kwamba, katazo hilo linafuatwa na Usalama wa Taifa? Ninachosema hapa ni kwamba, watu ambao wametuhumiwa wachukuliwe hatua, hata Profesa Mwandosya hapa alisema asubuhi, kama kuna uhalifu, basi ushughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu nafahamu kwamba, wengi mmechangia kuhusu hili na yote ambayo mmeyasema ni mazuri tu, lakini kama kuna dosari lazima kuwe na mkakati wa kuzisahihisha. Ndiyo tunalosema hilo, hata katika hotuba yetu hakuna mahali popote ambapo tumesema kwamba, Usalama wa Taifa wote umeoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili lichukuliwe kwa

nia njema. Tunataka kusahihisha hizi dosari zilizomo. Kwa hiyo, naomba jibu kuhusu huo mkakati wa kisera ambao Serikali inao na kama jibu haliridhishi nitaondoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Nyangwine!

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jina langu ni Nyambari Chacha Mariba Nyangwine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba katika nchi yetu, tumelelewa tukiamini Tunu za Taifa letu ambazo ni umoja, upendo, mshikamano na amani. Hayo yote yamewezekana chini ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake ya mpaka sasa hivi, lakini inavyoonekana sasa hivi, kuna suala sugu ambalo limejitokeza, hasa suala la udini na Wabunge wengi wamelisema. Hata mimi mwenyewe katika mchango wangu wa maandishi nimelisema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza kwamba, kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo yenye jukumu la kulinda amani ya Tanzania na si mtu mwingine yeyote yule, hawa wanaopiga kelele, wanapiga kelele tu, lakini hawana jukumu hilo, mwenye jukumu la kulinda amani ya Tanzania ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa suala hili la udini linavyoibuka, naomba kauli ya Serikali, hapa hapa Bungeni leo hii, ili Watanzania wapate kujua Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi au hata wa muda mrefu wa kudumisha amani na hasa kuondoa kabisa suala hili la udini katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ningeomba kuuliza, kwa nini TAKUKURU haikamilishi kwa haraka kesi zake za rushwa kubwa kubwa? Pia kwa nini TAKUKURU haijaingizwa rasmi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyo Sekretarieti ya Maadili, kama ilivyo Tume ya Haki za Binadamu na kadhalika, ningeomba kupata jawabu.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumeona ongezeko la Bajeti ya mishahara kutoka trilioni nne hadi trilioni 5.4, ongezeko la asilimia 30 ikilinganishwa na mwaka jana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi ambao ni Watumishi wa Umma, wanalipwa mishahara yao kutokana na ngazi au madaraja walioajiriwa, bila kuangalia mazingira au maeneo wanayofanyia kazi, jambo ambalo limewafanya watumishi wanaopangiwa vijijini kukata tamaa na kuacha kazi kutokana na mazingira na huduma zinakuwa ni hafifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isitoe motisha kwa wafanyakazi wanaopangiwa vijijini ili kuwapa moyo wa kuendelea kufanya kazi, lakini vile vile kuhakikisha Watanzania ambao ni asilimia 75 ya Watanzania wanaoishi vijini wanapata huduma hasa kwenye Afya na Elimu? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa nitamwita anayehusika na swali alilosema Mheshimiwa Sakaya kuhusu mambo ya TAKUKURU.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba radhi jana sikuweza kuwepo, tulipata msiba kule Mtwara, nililazimika kwenda kuzika, kwa hiyo, nawashukuru sana Mawaziri wa Nchi wenzangu ambao wamenisaidia kuelezea na kujibu hoja wakati nimekwenda kuzika kule Mtwara, msiba wa *General* Makame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu dada yangu Magdalena Sakaya, Mbunge Viti Maalum maswali yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anasema, TAKUKURU haipo kisheria kama vilivyo vyombo vingine. Si kweli, TAKUKURU iko kwa mujibu wa sheria, lakini ni kweli kama wewe ulivyosema haikutajwa kwenye Katiba, unaposema kwamba

chombo hakipo kisheria, maana yake kinafanya kazi bila kupitishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya TAKUKURU ilikuwepo, mwaka 2007 tukairekebisha hapa ndani, zamani ulikuwa unaweza kushtakiwa kwa makosa manne tu, tukairekebisha tukaiongezea, sasa yanafika makosa 22. Kwa hiyo, moja hilo kuwa toeni mashaka kwamba haipo kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yeye anachotaka kusema na mimi nataka niungane naye, anachosema ni kwamba, chombo hiki kitajwe kwenye Katiba kama vilivyotajwa vyombo vingine. Sisi ndani ya TAKUKURU tumeliona hilo, tumewasilisha mapendekezo hayo katika Tume ya Marekebisho ya Katiba na mengine mengi yanayohusiana na utendaji kazi ndani ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine alilolisema, nalo pia tumelipeleka kwenye Tume ili likafanyiwe uamuzi, kwamba, katika nchi nyingi, chombo kinachosimamia Kupambana na Rushwa, kinajiendesha chenyewe; Wanapokea malalamiko, wanapeleleza, na wanashtaki.

Kwa hiyo, lile la kutupiana mpira imekwenda kwa fulani, imekwenda kwa *DPP* na nini na nini hakuna. Kwa hiyo, hili tumelipeleka katika Tume, Tume italifanyia maamuzi ili kama itawezekana, Tumetembelea nchi mbalimbali, China, Ghana, wapi, ambazo zina vyombo kama hivi, wao wanajiendesha kwa asilimia mia moja; wanapokea malalamiko, wanapeleleza, wanachunguza na wanashitaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo sasa kama utaratibu tulionao sasa ni mzuri tutaendelea nao, kama si mzuri itajulikana hapo, lakini maoni hayo Mheshimiwa dada yangu, tumeyafikisha kwenye Tume ya Katiba, tukikubaliana na mtazamo wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na hilo likifanyika ndiyo ile uliyoisema kwamba unataka TAKUKURU ipewe meno zaidi na ndiyo maoni hasa na chombo chenyewe kinahitaji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile moja alilosema kwamba TAKUKURU tunakamata wadogo tu si kweli, TAKUKURU tunashughulika na mtu yeyote ambaye tunapata ushahidi kwamba, amekwenda kinyume na maadili ya nchi yetu yaani amejishughulisha na rushwa. Ndiyo maana mpaka sasa kesi zinazoendelea Mahakamani ziko za wakubwa na ziko za wadogo.

Jambo la tatu, nadhani maswali yake yalikuwa mawili tumeyamaliza.

**MWENYEKITI:** Bado, endelea kwa Profesa Kahigi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakwenda kwake.

Mheshimiwa Profesa Kahigi, Mbunge wa Bukombe, anasema, je, Serikali ina mkakati gani wa kisera kwa watu ambao wametuhumiwa? Sasa hapa ndugu yangu, rafiki yangu, zamani alikuwa *TANU Youth League* mwenzangu na mpaka sasa najua tu tuko pamoja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea hapa ndugu yangu Kahigi ni kwamba! Hawa watu wanatuhumiwa, nchi hii inayofuata utawala bora, tutafanya makosa makubwa sana kila mtu aliyeandikwa kwenye gazeti kwenda kumkamata, nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ndugu zetu wanasema, ushahidi wanao na aliyefanya ni fulani! Hivi ni kitu gani kinachofanya wasipeleke mashtaka hayo Mahakamani, kwa sababu kwa mujibu wa nchi hii, chombo kilichopewa madaraka ya kutafsiri Sheria, kusema huyu kafanya, huyu hakufanya, ni Mahakama.

Kwa hiyo, nasema tutakuwa hatuwatendei haki hao wanaotajwa kwenye magazeti, kwa sababu wengine wanatajwa ni kweli, wengine pengine wanasingiziwa. Lakini leo wametajwa watu hao mnaodai kwamba wametoka

kwenye hiyo Idara, kesho kutwa wa Idara ya Maji, kesho kutwa wa Idara ya Madini, kesho kutwa wa wapi, itakuwa kila mtu anayetajwa tumtungie Sera, nadhani litakuwa gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya tumetunga Sheria ambayo inamtawala kila mtu, awe ametoka Usalama wa Taifa, awe ametoka Bukombe au ametoka wapi, nadhani Sheria ni msumeno, inamshughulikia kila mtu, lakini kwamba tukae tutunge Sera kwa ajili ya watu waliotuhumiwa, nadhani *comrade* mwenzangu pale wa zamani, tuendelee kuitana *comrade* tu.

Mheshimiwa Fakharia, dada yangu pale anauliza, kwa nini TAKUKURU haikamilishi haraka kesi kubwa na kwa nini haiingii katika Katiba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la kwenye Katiba nadhani tumelisema, kwamba, tumepeleka hayo mapendekezo, kwa hiyo, majibu yatapatikana baada ya Tume ya Marekebisho ya Sheria kumaliza kazi yake, tukapigia kura za maoni, ikikubalika au haikukubalika tutajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uchunguzi wa kesi kubwa kubwa, tatizo liko wapi? Kijijini pale ikitokezea kwamba Daktari fulani au Mganga Fulani, hapigi sindano mpaka mtu atoe chochote, kukusanya ushahidi ni rahisi sana, maana watu mpo kijijini pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kesi kubwa mara nyingi zinahusika pia na watu waliopo nje ya nchi. Kwa hiyo, lazima ushahidi wa vielelezo upatikane, upatikanaji wa mashahidi wanaotuhumiwa ili waweze kuchukuliwa maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kwamba, TAKUKURU wakitaka kupeleleza nje, lazima wafanye mawasiliano kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lazima afanye mawasiliano na wale watu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Sasa nasema, inawezekana sasa hili la kupokezana, huyu afanye hiki, huyu afanye hiki, ndiyo kunacheleweshа. Ndiyo maana tunasema kwamba, chombo kikiimarishwa na kama mlivyopendekeza, wakiambiwa wafanye wao kila kitu, inawezekana, muda wa kupeleleza ukawa umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mmeshajibu ya Mheshimiwa Fakharia bado ya Mheshimiwa Chacha Nyangwine na Mheshimiwa Sara.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chacha Nyangwine anauliza tu suala la udini na hatua gani ambazo zinachukuliwa za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la udini, ni suala ambalo liko katika mawazo na linaweza likapungua au kuongezeka kutegemeana na viongozi wanavyoshirikiana. Kwa hiyo, katika hatua za mwanzo kabisa za muda mfupi, tunawashirikisha viongozi wa Madhehebu yote ili watusaidie kumaliza tatizo hili. Nataka kusema tu kwamba, tumekwisha kuzungumza na tarehe 13 ya Mwezi uliopita tulizungumza na viongozi wa Madhebu ya Kiislam na tarehe 23, wiki ijayo tutazungumza na Madhehebu ya Kikristo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo tutaitisha Mkutano wa Madhehebu ya Kikristo na Kiislam kwa pamoja, ili kuja kukaa pamoja, waweze kuzungumza na wote tuliozungumza nao wana mwelekeo unaofanana. Wote wanachukia udini, wote ni Wazalendo, hawataki fujo na wanataka amani. Kwa hiyo, kwa kweli tunadhani kazi haitakuwa ngumu sana kwa sababu makundi yote yanataka amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza na Waislam wanataka amani, ukizungumza na Wakristo wanataka amani. Kwa hiyo, hatua ya mwanzo itakuwa ni kuwaunganisha ili tumalize *problem* ambayo ipo, lakini kwa

mustakabali wa hatua ya kati na hatua ya muda mrefu ni ya elimu. Kwanza ni elimu kwa watu wote ili waweze kuelewa kwamba umoja ndiyo njia peke yake ambayo inaweza kufanya mustakabali wa Taifa letu ukaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika Bajeti ambayo tuimeipitisha hapa, tumeweka *provision* ya kuwa na Mikutano ya Madhehebu ya Kidini katika Mikoa yote nchini. Tumesema ni Mikutano 15, lakini inaweza ikazidi hapo, kwenda katika maeneo yote kuwachukua Viongozi wa Dini, wa Kisiasa na kuwaweka pamoja na kujadiliana nao juu ya mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini hatua hizo zinaweza kutusogeza mbele na kupunguza kabisa *problem* ya udini ambayo kwa kweli ni mawazo zaidi kuliko kitu kingine chochote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mwingine wa Nchi, kuhusu swali la Mheshimiwa Sara.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu motisha na mishahara kwa wafanya kazi, tumeanzisha ile Bodi ya Motisha na Mishahara kwa Wafanyakazi na imeshafanya kazi nzuri tu. Imetembelea Wilaya 33 ambazo ziko pembezoni na kugundua matatizo yafuatayo:-

Kwamba hakuna nyumba za wafanyakazi, hakuna visima na hakuna nishati mbadala. Kwa hiyo, hizo Wilaya 33 kwa mwaka ujao wa fedha tutahakikisha kwamba, yale masuala muhimu ambayo yameshakuwa *identified* yanafanyiwa kazi na Bodi yetu ya Mishahara na Motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza katika Wilaya mbalimbali, mambo ya usafiri kwa mfano, mwaka 2009/2010 tulinunua Boti kwa ajili ya Wilaya zile ambazo ziko pembezoni. Tunatoa mikopo kwa wafanyakazi kwa riba nafuu, yaani mikopo hii inatoka Serikalini, nayo ni motisha tosha kwa Wafanyakazi. Pia, tunatafuta namna bora ya kutafuta posho

ya aina gani tuwalipe wafanyakazi na hii itafanyika katika mwaka huu huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunafanya zoezi la *job description,* kuangalia uzito wa kazi kwa kila kada, kwamba Daktari ana uzito wa aina gani, ili uzito wa kazi uendane pamoja na mishahara, hiyo ndiyo mikakati ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Kahigi alitoa taarifa ya hoja kuondoa shilingi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu ambayo nimepewa na Mheshimiwa Waziri kwa kweli nitaondoa shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ni hoja. Endelea, ameomba anaondoa shilingi.

**MHE. PROF.KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kutoridhika na majibu yake ni kwamba, kuna matukio ambayo yametokea, ambayo yanaonesha kwamba watuhumiwa wamefanya...

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza nielekeze. Tunapotoa hoja, lazima liwe jambo moja, linaloeleweka ambalo unaweza kuli-*describe,* lakini ni hoja moja sasa tutakapowahoji watu tunahoji hilo, hatutahoji watu wametuhumiwa na wengine wamefungwa, hoja yako ni nini!

Naomba sana hii ieleweke kwa sababu vinginevyo ukitupa maneno 10, sisi hatutajua cha kupigia kura, kwa hiyo, naomba uielewe namna hiyo. Unaweza kui- *describe*, lakini hoja ni ipi, ndiyo hiyo maana ya hoja.

Mheshimiwa Profesa! Siyo malalamiko, iwe hoja nataka tufanye hivyo.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, hoja yenyewe ni ya kuchukuliwa

hatua watumishi wa Usalama wa Taifa ambao wametajwa kwa majina kwamba, ni watuhumiwa katika matendo kadha wa kadha ya utekaji na utesaji na pia katika kurubuni baadhi ya Maafisa wa CHADEMA kwa kuwapa pesa. (*Makofi*)

Ndiyo hoja hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja ili tuiunge mkono.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Kicheko*)

Mnacheka nini?

**MWENYEKITI:** Katika hoja ya kutoa shilingi hawaungi mkono kwa kusimama, anayetaka kusema atasema, Mheshimiwa Mnyika!

Sasa tukubaliane, mambo yaliyoko Mahakamani tutagombana sasa hivi, haya tuendelee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nichangie hoja hii kwa mambo ambayo hayako Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Dakika tatu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ukurasa wa pili wa hotuba ya Kambi ya Upinzani, ulieleza kwa kina namna ambavyo wapo Watumishi wa Usalama wa Taifa wameshiriki kwenye matukio ya kuteka na kutesa na Mheshimwia Spika anatambua kwamba kwa Bunge letu Tukufu ni ruksa kwa Wabunge kufanya rejea taarifa za kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la Mwanahalisi kabla ya kufungiwa kwake, liliandika habari ambayo ilimtaja mtumishi wa Usalama wa Taifa Ramadhani Igondu, ambalo vilevile Dkt. Urimboka Steven aliyetekwa ambaye mpaka leo hajahojiwa na vyombo vya Dola, ilinukuliwa kwenye vyombo vya habari chini ya kiapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba nikukatishe mimi mwenyewe hata Mwanasheria asiposimama, naomba na wewe ukae, kwa sababu jana tumekaa kwenye Kamati ya Kanuni, Dkt. Ulimboka siyo yeye aliyeshtakiwa, lakini kesi ipo kwa sababu ya matukio yaliyompata Dkt. Urimboka, ndiyo maana tukasema ondoeni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyika, nakuomba tuheshimiane, tufuate utaratibu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba niendelee kuchangia. Ukurasa wa tatu wa Hotuba ya Kambi ya Upinzani, kumeelezwa mawasiliano baina ya watumishi wa Usalama wa Taifa na mawasiliano yaliyotajwa hapa hayahusu jambo ambalo, na sitaingilia jambo ambalo liko Mahakamani, ila nataka kufahamu tu, hatua gani zimechukuliwa na Wizara husika kuhusu watumishi waliotajwa kwenye taarifa hii, ukurasa wa tatu wa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, La tatu na la mwisho, kwenye ukurasa wa nne wa hotuba ya Kambi ya Upinzani...

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ushahidi wowote uliotolewa hapa kuonesha kwamba majina yaliyotajwa hapa ni watumishi wa Usalama wa Taifa, kwa sababu, Sheria yenyewe, inataka Waziri anayeshughulika na mambo hayo ndiye athibitishe, sasa hakuna ushahidi, hakuna mtu anayejua wale waliotajwa kwenye magazeti wala waliotajwa hapa.

**MWENYEKITI:** Baada ya kubadilisha ile hotuba ya Profesa Kahigi, ya pili haikuwa na majina, ya mwanzo aliondoa majina na ndiyo maana ilikuwa *admitted* hapa. Kwa hiyo, tunaomba tunapo-*refer,* tufanye *reference* kwa ile na ile sikumbuki kama ilikuwa na majina. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ndiyo maana naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Prof. Kahigi ya kwamba Serikali ichukue hatua. Serikali ikikubali kuchukua hatua, itatumia hizi taarifa ambazo zimeshatolewa, itakubali kufanya uchunguzi, itakwenda kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na maelezo yaliyotolewa na Waziri, masuala haya ni masuala ya kijinai. Kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, mwenye kipaumbele kikuu cha kuwasilisha mashtaka kuhusiana na masuala ya kijinai ni Jamhuri, leo Jamhuri inakwepa wajibu wa kwenda kufungua mashtaka inahamisha wajibu kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa kwamba kuna fursa ya kuwasilisha mashtaka binafsi. Kwa bahati mbaya kwa sababu ya ubovu wetu wa kisheria, fursa hiyo hata yenyewe mtu binafsi hawezi kuitumia bila kibali cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Ofisi ya *DPP* kwa maana ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Katika mazingira kama haya, ni vigumu kwa watu binafsi kuweza kufungua mashitaka. Ili watu binafsi wafungue mashtaka ni lazima Serikali iseme kwamba imeshindwa kuchunguza na kufungua mashtaka ndiyo watu binafsi waweze kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwanasheria na wewe unajadili?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu...

**MWENYEKITI:** Kwa taarifa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Unaposhtaki, mamlaka ya kushtaki mtu binafsi, huhitaji ruhusa yangu wala huhitaji ruhusa ya *DPP* isipokuwa *DPP* anaweza kuingilia kati akachukua hiyo kesi. Kwa hiyo, asipotoshe Bunge kwenye hilo! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, dakika tatu!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na kuanza kushughulikia vitu ambavyo vinaongelewa au hisia bila kuwa na *evidence* lakini naona Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu amenisaidia vya kutosha kwa sababu mtu ambaye anatakiwa kufungua shtaka, ni vyombo husika vinapojiridhisha kwamba je tuhuma hizi zinafaa kupelekwa kwenye vyombo vya dola au lah! Si tu mtu fulani labda akisema, tukiendelea na taratibu za kufanyia kazi hisia, nchi yetu haitafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninachoshauri ni kwamba vyombo vinavyosimamia masuala ya kisheria wamesikia, wao watafanya uchunguzi, kama wanaona kuna haja ya watu hao kufikishwa Mahakamani watafikishwa lakini siyo tu kwa sababu imesemwa basi lazima watu hao wafikishwe Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu ni kwamba mtu anaweza akatuhumiwa na kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi, ushahidi hautolewi siku ambapo mtu ametuhumiwa, ushahidi huwa unatolewa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muajibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, Waziri wa Mambo ya Ndani yupo hapa na Mawaziri wote, sisi tumewatuhumu hawa watu na Waziri anafanya kazi kwa niaba ya Askari wote kwa mujibu wa *principle* ya *Constitutional Law* inayoitwa *Eagle Theory,* anafanya kazi kwa niaba ya Askari wote. Kwa hiyo, kama kuna mtu yeyote ametuhumiwa humu ndani, Waziri ana uwezo wa

kuchukua tuhuma ile na kuipeleka Mahakamani. Pia kifungu cha 90 cha sheria hiyo, kinaeleza kwamba *DPP* ndiye anaye *prosecute* kesi, kesi gani hapa zimeendeshwa na *Private Prosecution?* Mwanasheria atuambie *private prosecution* imefanywa na watu wangapi? Labda afanye *delegation*, amefanya kwa *private people* wangapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simbachawene.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama ili kuunga mkono maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri na pengine kwa kuwa jambo hili ni la kisheria lakini tunayo bahati kwamba Bunge hili Mwanasheria Mkuu ni mtu ambaye amewahi kuwa Jaji na Mawakili wenzangu lazima tuheshimiane kitaaluma pamoja na nafasi zetu za uwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna aliyewahi kwenda Polisi kufungua kesi, maneno haya yamesemwa ndani ya Bunge, sasa mnasema nani anakwenda kushtaki yaani Serikali inachukua wapi hilo shitaka? Kuna yeyote ambaye amekwenda Polisi akasema fulani amefanya hivi, ushahidi ni huu na Polisi wakashindwa kufungua kesi dhidi ya mtu huyo, huo ndiyo utaratibu wa kesi za jinai. Hapa ni maneno yameandikwa magazetini, hapa ni Waheshimiwa Wabunge wamechangia michango yao, sasa haiwezekani ukawa ndiyo utaratibu wa kesi za jinai Waheshimiwa Wanasheria wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri kama kuna yeyote ambaye ana ushahidi, aende kwa utaratibu wa jinai zilivyo, kesho au hata sasa hivi toka nenda Polisi pale, kaseme mimi nimesema fulani amefanya hivi na vile na uone kama hatua hazitachukuliwa. Sasa mnataka Mwanasheria Mkuu atoke hapa aanze kuwakamata watu ambao hamjafuata taratibu zinazotakiwa au hiki ni kituo cha Polisi? *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Halima Mdee, halafu Serikali!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoona *deal duly* zinapigwa hapa naanza kuona Serikali inajua mchezo mzima. Nasema hivyo kwa nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, Wabunge watumie lugha ya Kibunge na Mheshimiwa Halima Mdee, ni Mwanasheria, anajua sheria na anajua heshima ambayo Wanasheria wanayo kwa watu ambao si Wanasheria. Naomba tufuate taratibu! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, twende tu kwenye hoja maana mkianza vijembejembe, tuseme ule ukweli kisheria ni nini tunachotaka.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kupitisha shilingi takribani bilioni 215 ambazo hazijapambanuliwa zaidi ya kuambiwa mishahara ya Usalama wa Taifa, TAKUKURU na vitu vinavyofanania na hivyo. Sasa leo kuna tuhuma hapa ambazo zinaonyesha kwamba kuna nyaraka za watumishi wa Ikulu, wakiongozwa na Bwana Michuzi, wakitoa taarifa kwa wenzao kina Rweyemamu kwamba kuna mkakati wa kihalifu wameufanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi matarajio yangu siyo kwamba sisi tunahukumu mtu hapa lakini Serikali ituambie tuleteeni ushahidi wa hao watu wa Usalama wa Taifa ambao mnadhani wanahusika na huu uhalifu tuwashughulikie, tufanye uchunguzi. Kuna mkanda kwenye *YouTube* umetengenezwatengenezwa mmekamata watu, sisi tunawaambia kuna nyaraka kwenye mtandao, za Ikulu, kwa nini mnakataa wakati wengine *YouTube* ziliunganishwaunganishwa mmembeba mtu yuko ndani

mpaka sasa? Kubalini tuwasaidie kazi, tuwape ushahidi, *simple*! Mkikubali sisi hatuna maneno na ninyi, tutawaletea mambo! *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria unajibu au yupo Waziri wa Sheria? Waziri wa Sheria halafu mtoa hoja!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kujaribu tu kutoa ufafanuzi wa mambo haya yanavyotakiwa kuendeshwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhuma inapotokea, lazima anayelalamika aende Polisi hasa kama ni jinai. Unakwenda kupeleka taarifa Polisi kwamba nina malalamiko fulani dhidi ya kitendo fulani kilichotokea kinachoniathiri mimi ama kinachoiathiri jamii. Polisi wanachukua hatua kisha kesi itaendeshwa lakini huwezi kuchukua gazeti limeandikwa maoni ya mtu, ameamua anavyotaka kuandika halafu unasema sasa twende tukamkamate sijui nani. Hii Waingereza wanasema hivi, *it is a case of giving a dog a bad name and then shut it! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wenyewe ndiyo wanaosimama wanasema hivi na vile halafu wanasema sasa kakamateni kwa sababu sisi tumesema, haiwezekani! Mwenye malalamiko anatakiwa kwenda Polisi na mimi nawashauri sana, nawashauri sana, mwenye malalamiko ambayo ni *criminal* aende Polisi na Polisi watachukua hatua siyo ndani ya Bunge, humu hatuwezi kuamua kesi wala hatuwezi kuchukua maamuzi ya kukamata watu humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tujielekeze hivyo, Wanasheria wenzangu wanajua, ninavyojua ni kwamba malalamiko yanapotokea ni Polisi tunaanzia, unapata pale *RB* halafu kesi itaendelea, sasa humu ndani ya Bunge tunafanyaje? Mimi kama Waziri wa Sheria niende wapi, nifanyaje? Nimwambie *DPP* kamkamate mtu, hawezi kwa

sababu kwanza *DPP* hakamati watu, nimwambie nani akakamate mtu na akamkamate kwa sababu gani?

**MBUNGE FULANI:** Kwa sababu yeye kasema!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kwa sababu imesemwa ndani ya Bunge? Haiwezekani! Malalamiko yana utaratibu wake, anayetaka aende Polisi! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Kahigi, sasa ni zamu ya mtoa hoja kwa sababu Serikali imeshajibu halafu tunapiga kura. Mheshimiwa mtoa hoja, *Professor,* wewe ndiye mwenye hoja hujamaliza...

**WABUNGE FULANI:** Haelewi. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hiyo ni hoja yako wewe.

*(Hapa baadhi Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea)*

**MWENYEKITI:** Naomba tusikilizane!

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi ninavyofahamu ni kwamba humu Bungeni Wabunge huwa wana *raise issues,* hata *EPA* ilianzia hapa Bungeni, Serikali ikachunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninachoomba ni kimoja tu na ni kidogo sana, hizi tuhuma zimeshasemwa humu Bungeni, Serikali fanyeni kazi yenu chunguzeni. Vyombo vya kuchunguza vipo, wala siyo jambo kubwa sana. Kwa hiyo, naendelea kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Sasa tunawahoji, Mheshimiwa tunachokifanya ni hivi, wewe umetoa hoja ya kutoa shilingi na umeeleza, ukaungwa mkono au ukapingwa na wenzako, sasa kinachotakiwa ni kwamba Serikali ikishajibu wewe mwenye hoja unamalizia.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya Kuondoa Shilingi iliyotolewa na Mhe. Prof. Kulikoyela Kahigi ilikataliwa na Bunge)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* .... ... ... ... ... ... Tshs. 216,269,000/=
Kif. 1003 - *Government Communication Unit*... ... ... .. Tshs. 168,673,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit*... ... ... ... .. Tshs.156,682,000/=
Kif. 1005 *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... Tshs.100,886,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Wakati wa Kamati ya Matumizi mnatulia chini kwa sababu mimi sijui nani anasimama au nani anafanya nini.

Kif. 1006 - *Planning Division* ... ... ... ... ... Tshs. 239,133,000/=
Kif. 1007 - *Information and Communication Tech. Unit* ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 57,423,000/=
Kif. 2001 - *Policy Development Division* ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 436,287,000/=
Kif. 2002 - *Management Service Division* ... ... ... ... ... Tshs.371,733,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa Kamati ya Matumizi ni wakati wa maamuzi, wote tunakaa chini wanaosimama ni wale wanaotaka kupata ufafanuzi au vinginevyo, siyo tena mnazurura katika ukumbi. Tuendelee!

Kif. 2003 - *Establishment Div.* ... ... ... ... ..Tshs. 768,209,000/=

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 2003,* kifungu namba 221400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili mfululizo kifungu hiki kimekuwa kikipata fedha takribani shilingi milioni 3,600,000/= lakini kwa mshangao safari hii ni shilingi milioni 13,200,000/=. Sasa naomba Waziri atueleze mbona kuna ongezeko kubwa sana katika kipindi hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtutura, kifungu ulichokisema kinaitwa *Hospitality Suppliers and Services...*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Sawasawa.

**MWENYEKITI:** Mwaka mmoja sifuri, mwaka mwingine sifuri...

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Hapana, ni *Communication and Information.*

**MWENYEKITI:** Basi ni 221200.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Ndio ni 221200. Sasa miaka miwili takribani mfululizo kifungu hiki kimekuwa kikipata fedha shilingi milioni 3,600,000/= lakini mwaka huu wa fedha kimeombewa shilingi milioni 13,200,000/=. Sasa tunaomba maelezo kwa nini kumekuwa na ongezeko kubwa kiasi hiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka kwa sababu kutakuwa na machapisho mengi sana katika Idara hii kwa ajili ya habari na miongozo mbalimbali ya Serikali.

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2004 - *Ethic Promotion Div.* ... ... ... ...Tshs. 222,833,000/=

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Subvote 2004,* kasma ndogo ya 210500*, Personal Allowance - In Kind.* Mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 13,852,000/= lakini sasa hivi ni shilingi milioni 38,340,000/= kuna ongezeko la shilingi milioni 24,488,000/=.

**MWENYEKITI:** Soma vizuri *figures,* naona kama umekosea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *Subvote 2004,* kasma ya 210500, *Personal Allowance - In Kind.*

**MWENYEKITI:** Hesabu yake inasemaje?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni 13,852,000/= lakini mwaka huu ni shilingi milioni 38,340,000/= ambayo inatoa ongezeko la shilingi 24,488,000. Nataka kujua mbona imeongezeka kiasi hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha maadili kulikuwa na watumishi wachache lakini sasa watumishi wameongezeka kama unavyoona kwenye *subitem* 210100*.* Sasa watumishi wakishaongezeka hata wale *entitled officer* ambao wako *entitled* kwa umeme, simu, maji, pango na kadhalika wanaongezeka pia, ndiyo maana kifungu kimeongezeka.

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimesema wakati wa Kamati ya Matumizi tunatulia. Tuendelee!

Kif. 2005 - *Human Capital Management Division* ... ... .. ... ... ... ... Tshs. 1,058,273,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo, tunasimama baada ya kusoma *figure*, Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuelewa katika *subvote 2005*, kasma namba 210400 ambayo inaonekana kama kuna *variation* imeongezeka mara kumi zaidi kutoka shilingi milioni 52 mpaka shilingi milioni 561. Naomba kupata ufafanuzi katika eneo hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kimeongezeka kwa sababu, hiyo ni Idara ile ninayosema kwamba ina *process payroll* yaani ule mfumo wa *Human Capital Management Information System.* Sasa kwa ajili ya ku-*process payroll* wanafanya kazi usiku na mchana. Kwa hiyo, fedha zake lazima zitaongezeka ili waweze kufanya kazi usiku na mchana. Kwa hiyo, wakati wa *payroll system function* ni lazima lazima watakula pale, watapata posho ya *extra duty* na posho nyinginezo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, ndiyo maana kuna ongezeko kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nauliza kwa sababu kifungu cha chini ya hichohicho yaani 210500 pia imeongezeka kutoka shilingi milioni 58 mwaka jana na mwaka huu ni shilingi milioni 150 na inaonekana kwenye kila Idara ya Wizara hii posho zimeongezeka kila mahali, kila mahali yaani posho zimeongezeka, sababu ni nini? Kama watu wanafanya kazi usiku kwa nini wasiwaajiri watu ili hizo kazi ziishe mchana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ni kati ya Waheshimiwa Wabunge ambao walitakiwa kutembelea ule mfumo, maana Kamati ya Katiba na Sheria ilitembelea Idara hiyo na kuuona huo mfumo. Huo mfumo unafanya kazi sana usiku, mchana

unafanya kazi polepole sana. Kwa hiyo, wanafanya kazi hizo usiku, lazima tuwalipe hao watumishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 2005, kasma 220100, *Office and General Supplies and Services,* mwaka jana ilikuwa takribani shilingi milioni 166 na mwaka huu ni shilingi milioni 14.5 tu na tofauti hapa ni milioni 152, nilikuwa naomba maelezo kuhusu hii.

**MWENYEKITI:** Kwa nini imepungua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu umeanza rasmi mwaka jana, kwa hiyo mwaka 2010/2011, ulikuwa unatengenezwa, mwaka 2011/2012 ulikuwa unatekelezwa ndiyo maana ulikuwa na fedha nyingi. Sasa hivi mfumo huo umekamilika ndiyo maana fedha zake zimepungua.

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3001 - *Human Resources Development Division* ... ... ... ... ... ... ... ...TShs. 3,228,060,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu hicho, kasma ya 270300 *Current Grant to Non- Financial Public* Units (*Academic Instutitions).* Hiki ni kifungu cha ruzuku kwa ajili ya Taasisi za Elimu. Mwaka jana kilikuwa na shilingi bilioni 3.2 mwaka huu kimeshuka mpaka shilingi bilioni 2.8 hapa ndipo ambapo Chuo cha Utumishi wa Umma pale Magogoni kinapewa pesa zake pamoja na Taasisi muhimu sana ya Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao. Ningependa kupata maelezo kutoka kwa Serikali, ni kwa nini Taasisi hizi muhimu za kielimu kiwango cha mgao wa ruzuku kimeshuka kutoka shilingi bilioni 3.2 mpaka shilingi bilioni 2.8.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopewa *ceiling,* tunaangalia vipaumbele. Kwa hiyo, tunagawana hizo fedha kulingana na mahitaji yetu. Kwa hiyo, hapa zimepungua kwa sababu mwaka jana walifanya vitu vingi sana na mwaka huu tumewaambia watumie fedha zao ambazo wanazipata kutokana na ada mbalimbali, ndiyo maana kifungu hiki kimepungua.

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3004 - *Diversity Mgt. Unit* ... ... ... .... Shs.152,799,000/=

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi tu. Katika kifungu 3004, eneo la *Utilities Supplies and Services* ambayo ni 220200 ambapo kwa kiwango kikubwa sana tunajua kwamba kuna madeni makubwa sana huwa Serikali inaingia kutokana na ulipaji wa maji halikadhalika huduma za simu. Sasa hapa naona kuna namba sifuri, je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kwamba Idara hiyo itakuwa inafanya matumizi yake katika *utilities?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki cha *utilities* ni malipo ya umeme, maji pamoja na simu. Jengo letu la Utumishi ni moja linalipiwa na Utawala. Mheshimiwa Mbunge akiangalia pale kwenye *subvote* 1001 atakuta kwenye *utilities* zipo fedha nyingi kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, hizo kidogo ambazo tunawawekea ni kwa ajili ya malipo ya simu ambapo kila Idara wanalipa pekee yao.

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 4002 - *Management Information System Division* ... ... ... ... ... Shs. 4,167,703,000/=

**MWENYEKITI:** Naomba msimame hivyohivyo. Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nauliza cha 270600 *Current Grant to Non-Financial Public Units (Agencies).* Mwaka jana ilikuwa millioni 674 na mwaka huu ni bilioni 3,723,600,000 imeongezeka bilioni tatu na milioni karibu mia moja, sababu ni nini ya kuongezeka bilioni tatu zote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ni kwa ajili ya Serikali Mtandao yaani *E-Government. E-Government* imezinduliwa mwaka jana na ni Taasisi mpya kwa hiyo, lazima ipewe fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza kazi zake. Kwa hiyo, utaikuta hapa na pia kwenye *development* tumewapa fedha nyingi kwa ajili ya kuimarisha Wakala ya *E-Government*.

**MWENYEKITI:** Mtu asirudie kifungu kilichoulizwa. Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P.GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi japo kifungu ni hicho lakini maelezo hayajaniridhisha.

**MWENYEKITI:** Toka lini, sio suala lako kifungu hiki kimekwisha. Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4002, kasma 220200, *Utilities Supplies and Service.* Mwaka huu wanaomba shilingi milioni 9.1, nataka kujua kwa nini miaka miwili ya nyuma kulikuwa na sifuri, sifuri na wakati huu wanaomba shilingi milioni 9.1.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Wakala wa Serikali Mtandao ulikuwa

haupo na mwaka huu upo kwa hiyo tumewapa fedha hizi kwa ajili ya kulipia umeme na maji katika jengo lao ambalo wamepanga.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma ileile 270600. Kwa mwongozo uliotoa maana yake limekwisha.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Kimesemwa na msemaji wa kwanza, ahsante.

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 4003 - *Records and Archives Division* ... ... ... ... ... ... ... Shs.706,938,000/=

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma ndogo 221400, *Hospitality Supplies and Services* mwaka jana ilikuwa milioni mbili, *this time* ni shilingi 11,400,000, ongezeko hili ni la nini naomba nipate maelezo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo, kwamba utilities, naomba nikipitie vizuri kifungu hicho, amesema kifungu...

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Kifungu 221400, *Hospitality Supplies and Service* kimeongezeka kutoka milioni mbili mpaka milioni 11.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimekiona ni kwamba *hospitality* ni pamoja na viburudisho, chai na kadhalika na sisi tunafungua ofisi mpya hapa Dodoma ambayo ni ya *record*, mmeona jengo pale. Kwa hiyo, tutaajiri watumishi kwa ajili ya ofisi hiyo ndiyo maana

mambo hayo ya viburudisho pamoja na chakula vimeongezeka kutokana na ofisi ambayo tumeianzisha hapa Dodoma.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* ... ... ... ... ... Shs. 2,056,194,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 220700, *Rental expenses,* mwaka jana zilitengwa shilingi milioni 500 na mwaka huu zimetengwa shilingi 200, sina tatizo na fedha kupungua lakini nataka kupata ufafanuzi kwa sababu *commitment* ya mwaka jana ilikuwa ni kwamba kutaharakishwa ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ni kwa nini mwaka huu tena tunaendelea kutenga fedha za kodi badala ya kuelekeza nguvu kwenye kuhakikisha Ofisi ya Sekretarieti inajengwa ili kuepukana na kutumia gharama kubwa kwa ajili ya kodi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana katika kifungu hiki pia kulikuwa na fedha za ukarabati ndani yake. Mwaka huu tunalipia pango tu, kwa hiyo, hizi ni kwa ajili ya pango ya Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nauliza kifungu 210300, *Personal allowance* zimeongezeka shilingi milioni 100, lakini nataka kujua sera ni nini kwa sababu mishahara ni kidogo kuliko posho, yaani mishahara ya Idara hii ni shilingi milioni 383, lakini posho ni shilingi milioni 397, kwa hiyo, posho ni nyingi zaidi ya mishahara. Sera ni nini kuhusu ulipanaji wa posho nyingi kuliko mishahara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekretarieti ya Maadili kuna posho maalum ambazo wanalipwa kwa ajili ya kazi muhimu na kwa ajili ya vikao mbalimbali, ndiyo maana posho hii imeongezeka ili kukiwa na mtuhumiwa akiitwa kuhakiki mali zake, kuna kikao maalum kinakaa ili kusikiliza maelezo yake. Kwa hiyo, lazima posho hii iongezeke ili kukidhi mahitaji ya vikao mbalimbali ambavyo ni vya kisheria na posho muhimu kwa ajili ya wale wanaokaa kwenye kikao hicho maalum.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ...TShs.237,185,100/=
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring and Evolution* Unit ... ... ... ... ... ... Shs. 171,045,200/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1004 – *Government Communication Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..TShs.124,466,300/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* 1004, kifungu kidogo cha 221100, *travel out of country,* tunaona shilingi 240,000, hivi kweli hizi fedha zimewekwa kwa ajili ya kusafiri kwenda nje au zimewekwa kama *figure?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Sakaya arudi nyuma kwenye *subvote* 1001, *Subitem* ambayo ni ya *Travel foreign,* ataona imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, fedha zote za kwenda nchi za nje, nyingi zinawekwa katika *vote* ya utawala. Hizo nyingine ni kwa ajili ya kutafuta *visa* na vitu vingine vidogo vidogo.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1005 - *Procurement and Management Unit* .. ... ... ... ...TShs 151,522,000/=
Kif. 1006 - *Internal Audit* ... . ... ... ... ... TShs. 150,017,400/=
Kif 1007 - *Information and Communication Tech. Unit* ... ... .... ... ... ... ...TShs.104, 002,100/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit* ... .. ... ... ...TShs. 360,836,300/=
Kif. 2001 - *Public Service Leaders Div.* ... ... .... ... ... . TShs. 589,688,000/=
Kif. 2002 – *Political Leaders Div*... ... ... ... TShs.497,316,000/=
Kif. 2003 – *Zonal Office* ... ... ... ... ... TShs.1,723,610,600/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 66 - Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* ... ... ... ...TShs. 1,329,794,200/=
Kif. 1002 - *Finance and Account* ... ... ... ... ... ... ... TShs. 242,665,800/=
Kif. 1003 - *Planning and Monitoring Division*... ... ... ...TShs. 308,277,600/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit* ... ... ... ... ... ... ...TShs. 332,236,800/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit*... ... ... ... TShs. 217,290,800/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*... ... ... ... TShs. 254,410,000/=
Kif. 1007 – *Library and Documentation Unit* ... ... ... ... ... ... ... ...TShs. 122,497,200/=
Kif. 1008 – *Management Information Syt*... ..... ... ... TShs.195,783,200/=
Kif. 2001 – *Macro Economy Cluster* ... ... ... ... ... ... ... TShs. 814,869,800/=
Kif. 2002 – *Productive Sector Cluster* ... ... ... ... ... ... ... ..TShs.529,761,600/=

Kif. 2003 – *Infrastructure and*
*Service Cluster* ... ... ... ... ... TShs. 508,745,600/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2004 – *Social Service and Demographic*
*Cluster...* ... ... ... ... ... ... .... TShs. 529,040,400/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 2004, kasma 220900, *Training Foreign*. Nataka kujua ni aina gani ya *training* ambayo ina-*cost* shilingi 500,000 na kama kuna *amount* nyingine labda ambayo inafidia hii, ni kwa nini sasa hapa imewekwa shilingi 500,000?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *training* kama nilivyosema zipo katika Idara ya Utawala. Kwa hiyo, huko kwingine ni kwa ajili ya kushughulikia mambo madogo madogo ya *visa* na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Hakusimama mwanzo.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2005 – *International Trade and*
*Econ. Relastic C* .... ... ... ... TShs. 474,682,000/=

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika vifungu vyote vya *basic salaries* utaona kwamba mishahara imepanda na hii naamini ni kwa sababu ya gharama za maisha kupanda lakini katika kifungu hiki tunachokiongelea...

**MWENYEKITI:** *Sub-item* gani?

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** *Subvote* 210100, *basic salaries.*

**MWENYEKITI:** Aaah!

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Katika Kitengo hiki imepungua kwa takribani shilingi milioni 20. Nilikuwa naomba maelezo ni kwa sababu gani katika kifungu hiki *basic salaries* zimepungua.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na baadhi ya watumishi kuhamishiwa Utawala. Ukiangalia kule Utawala wapo watumishi wengi zaidi na ukiangalia *basic salaries* imeongezeka kwa kiasi kikubwa, ndiyo maana hapa pamepungua wamehamishiwa kwenye Idara nyingi.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko *subvote* 2005, kasma ya 221100.

**MWENYEKITI:** Rudia tena.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Kuna ongezeko**...**

**MWENYEKITI:** Rudia kwanza tena *subitem***.**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** *Subvote* 2005, kifungu 221100 *Travel out of country*.

**MWENYEKITI:** Sawasawa**.**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Kuna ongezeko la shilingi milioni 76, sasa naomba kupata ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama atakumbuka ni kwamba kimeanzishwa Kitengo kipya cha *Monitoring and Evaluation* ambacho Mheshimiwa Wassira amekieleza kwa urefu sana. Kwa hiyo, katika kufuatilia

miradi, hizo ndizo fedha zitakazotumika katika *Monitoring and Evaluation* katika sehemu mbalimbali.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 3001 - *Social Service and HR Development* ... ... ... ... ... ... ... Tsh. 0/=

*(Kifungu Kilichotwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management* ... .... ... ... ... Tsh. 1,141,286,200/=

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko katika kifungu hicho, *item* ya 230200 (*Routine Maintenance and Repair of Buildings).* Mwaka jana kulikuwa na shilingi 3,000,000 na mwaka huu ni shilingi 138,600,000/= ni ongezeko la shilingi 135,000,000. Ongezeko hili ni la nini, naomba ufafanuzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hebu rudia.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Kifungu kidogo cha 230200.

**MWENYEKITI:** *Routine Mintenance and Repair of Buildings.*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mwaka jana zilitengwa shilingi 3,000,000 safari hii ni shilingi 138,600,000, nafikiri tumefahamiana, tatizo ni nini, mbona ongezeko ni kubwa sana?

**MWENYEKITI:** Sawasawa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyofahamu, Sekretariet ya Ajira iko pale Maktaba. Kwa mwaka wa jana tulikuwa hatujalipa deni la pango. Kwa hiyo, fedha hizi zimeongezeka ili kulipa deni la pango la mwaka jana pamoja na mwaka huu.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... Tshs.151,672,800/=
Kif. 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation* ... ... ... ... ... ... Tshs.73,975,000/=
Kif. 1004 - *Government Communication Unit*... ... ... ... ... ... ... ... .... Tshs. 51,680,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1005 – *Legal Service* ... ... ... ... ... ... ... Tshs.0/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, unataka kujua kwa nini hakikutengewa fedha?

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitendo cha kuwa hakikutengewa fedha ndio nataka kujua. Kwa sababu mwaka wa juzi hakikutengewa, mwaka jana kilikuwepo na haya ni mambo ya sheria. Sasa ni vizuri tupate ufafanuzi kwa nini kisitengewe fedha au kuna tatizo gani, hebu tupate ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki hatujampata *Legal Officer*, kwa hiyo hakuna Mwanasheria katika Idara hiyo.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1006 - *Procurement Management* ... ... ... ... ... ... .Tshs.51,078,000/=

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naulizia kasma ya 220300, *Fuel, Oils and Lubricants.* Kwa miaka miwili haijapata mafuta, naomba *clarification.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba waangalie tu pale Utawala kwenye *Fuel, Oil Lubricant* ndicho kifungu ambacho kinahudumia Idara nyingine ambazo hazina magari, kwa hiyo wanaazima kutoka sehemu nyingine.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1007 - *Management Information Systems* ... ... ... ... ... ... ... Tshs.77,885,000/=

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo 220900, *Training Foreign.* Hakuna fedha iliyotengwa tangu mwaka wa jana na mwaka huu pia hakuna fedha iliyotengwa, je *training* hizi zimekatishwa au la?

**MWENYEKITI:** Ipo Utawala.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Fedha hizo ziko katika Fungu la Utawala na nyingine ziko kwenye mradi ambapo tutaziona kule kwenye *Development, Volume IV*.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 1007, kasma 221200, *Communications and Information.* Kuna ongezeko la mara kumi kwa bajeti ya mwaka huu, naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Nimekiona, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki mara nyingi ni kwa ajili ya magazeti, machapisho mbalimbali ili kujitangaza. Kwa hiyo, Sekretariet ya Ajira watakuwa na machapisho mengi kwa ajili ya kujitangaza na pili kwa ajili ya matangazo mbalimbali.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1008 – *Internal Audit* .. ... ... ... ... ..Tshs.52,419,000/=
Kif. 2001 – *Recruitment Management Division* ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 919,351,000/=
Kif. 2002 – *Quality Control* .. ... ... ... ... ...Tshs. 410,936,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais,**
**Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management*... ... ... ... ... Tshs.2,431,738,000/=
Kif. 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation* Unit ... ... ... ... ... Tshs.636,586,000/=
Kif. 2001 - *Civil Service* ... ... ... ... ... ... .. Tshs.251,902,000/=
Kif. 2002 - *Local Gvt. Service*... ... ... ... ...Tshs.255,432,000/=
Kif. 2003 - *Teacher's Service*... ... ... ... ... Tshs.7,092,753,000/=
Kif. 2004 - *Fire and Immigration Service*... ... ... ... Tshs.176,888,000/=
Kif. 2005 - *Health Service* ... ... ... .. ... ..Tshs.219,327,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* .... ... ... ... ... ...Tshs. 59,587,357,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 – *Adminstration and HR Management* ... ... ... ... Tshs. 2,675,000,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 6284 Maboresho ya Utumishi wa Umma, hiki kiwango cha shilingi bilioni1.7 fedha za nje na shilingi 880,000,000/= fedha za ndani, kinajumuisha masuala ya ununuzi naamini hivyo, Mheshimiwa Waziri atanirekebisha, wa magari mawili ya maboresho shilingi 300,000,000/= na vilevile gharama za Wataalam Elekezi kama sehemu ya hizo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi tu, kwa kuwa Serikali iliamua kupunguza gharama za ununuzi wa magari, ni kwa nini kwenda kununua magari mawili kwa shilingi 300,000,000/=. Kwa nini fedha hizohizo zisitumike kununua magari mengi zaidi yakatumika kuisaidia hii programu na kwa nini kiwango cha kugharamia Wataalamu Elekezi kisipungue ili kuelekeza fedha kwenye maeneo ambayo yataweza kusaidia maboresho kwa upana wake. Ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Idara imekosa kabisa magari, hakuna njia nyingine ambayo tunaweza tukawasaidia, ila ni kuyanunua magari hayo. Kwa hiyo, tunanunua kwa sababu hawana gari lolote pale sehemu ya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mtaalamu Mwelekezi ni kwamba hizo programu zinatakiwa zipewe mrejesho na tuone nini tumefanya, tulipo ili tuweze tukajenga hoja tuweze kupata fedha zaidi. Kwa hiyo, lazima kuwe na Mtaalamu Mwelekezi ili afanye hiyo *review* itusaidie katika kupata fedha nyingine.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs.50,000,000/=
Kif. 1003 - *Government Communication Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs.104,452,000/=
Kif. 1004 - *Procurement Management Unit* ... ... ... ... ..Tshs.100,000,000/=
Kif. 1006 - *Planning Division*... ... ... ... ..Tshs.1,484,975,000/=
Kif. 1007 - *Information and Communication Tech Unit*... ... ... ... ... ... .. Tshs.403,863,000/=
Kif. 2001 - *Policy Development Division*... ... ... ... ... ... ... Tshs.1,354,650,000/=
Kif. 2002 - *Management Service Division*... ... ... ... ... ... ... Tshs. 650,000,000/=
Kif. 2003 - *Establishment Division*... ... ... ... ... ... ... ... Tshs.417,400,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2004 - *Ethic Promotion Division* ... ... ... ... ... Tshs. 442,084,000/=

**MHE HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi kidogo katika hiki kifungu kidogo cha 6284 cha Uhamasishaji wa Maadili katika Sekta ya Umma, kimeongezeka sana kutoka shilingi 180,000,000/= mpaka shilingi 442,000,000/= na kumekuwa kuna malalamiko kwamba maadili yamepungua kwa kiwango kikubwa sana lakini vilevile zinaonyeshwa kwamba ni fedha za nje. Sasa

nilitaka nipate ufafanuzi juu ya ongezeko ni za nini na kwa nini zinatoka nje na kama wafadhili wasipoleta maana yake kazi hazitafanywa au kuna utaratibu mwingine?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya Mpango na Programu yenyewe. Kwa hiyo, tunajenga hoja, tunapata fedha kutoka kwa wafadhili, lakini hata Serikali inachangia kwa njia moja au nyingine na utakuta fedha nyingine *local* ziko katika vifungu vingine vya maendeleo.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2005 - *Human Capital Management Division* ... ... ... ... ... ... .Tshs. 1,186,401,000/=
Kif. 3001 - *Human Resource Development Division*... ... ... ... ... ... .... Tshs. 1,050,000,000/=
Kif. 3004 - *Diversity Management Unit*... ... ... ... ... ... ... .... Tshs.177,032,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 4002 - *Management Information System Division*... ... ... .... ...Tshs. 7,025,000,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 6284 Maboresho ya Utumishi wa Umma Awamu ya II *(Public Service Reform Program II)*. Kuna fedha hapa zimetengwa mwaka huu wa fedha shilingi bilioni 6.2 fedha za ndani kutoka shilingi 463,000,000 mwaka jana. Sasa hizi ni kwa ajili ya mradi wa Serikali ya Mtandao kwa maana *E-Government.* Sasa wakati wa majibu Mheshimiwa Waziri nashukuru alijibu, alizungumzia kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kuanzisha pamoja na mambo mengine tovuti ya Serikali lakini ukisoma ukurasa wa 10 wa hotuba ya Waziri, sehemu ya nne, inasema kwamba "Serikali inakamilisha uanzishaji wa Tovuti ya Wananchi (*Citizen Portal)".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nina tatizo hapa, miaka michache iliyopita kuliwahi kutengwa tena mabilioni ya shilingi kuanzisha Tovuti ya Wananchi kupitia Idara ya Habari Maelezo. Sasa hivi kunaanzishwa tena Tovuti nyingine ya Wananchi na kunaanzishwa vilevile Tovuti ya Serikali halafu tunatumia shilingi bilioni sita za fedha za ndani ambapo kuna uhaba sana wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ni kwa nini hizi fedha zisihamishwe kutoka kwenye huu mradi na kuelekezwa kwenye miradi mingine. Ningeomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri sababu hasa ya mradi huu, umuhimu wake sana kwa Taifa kwa kiwango ambacho tutenge shilingi bilioni sita za fedha ndani kwa ajili ya mradi huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kabla hujajibu, kwa kutumia Kanuni 104, naongeza muda wa dakika thelathini baada ya muda wake kupita.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mnyika angeipongeza Serikali kwa kutenga fedha za ndani shilingi bilioni sita kwa ajili ya Serikali Mtandao. Hatutegemei wafadhili kutoka nje, hilo kwanza angetupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi kwa kuwa hiyo ni taasisi mpya, ni kwa ajili ya ununuzi wa magari, ununuzi wa *boundwidth*, ununuzi wa *software and hardware*, kwa hiyo, una mambo mengi, pia kusimika tovuti mbalimbali za Serikali katika Taasisi za Serikali hamsini. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 4003 - *Records and Archieves Division* .... ... ... ... ... ... Tshs. 2,199,143,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

**Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi**

Kif. 1001 - *Administration and General*... ... ... ... ... ... ...Tshs. 1,500,000,000/=

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 1001, *item* 6389, *Construction of Office Building*. Kuna fedha za ndani shilingi 1,500,000,000/=. Nataka kuelewa ni ujenzi upi uliokusudiwa na wapi?

**MWENYEKITI:** Uliza tena swali.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** *Subvote*, 1001, *item* 6389, *Construction of Office Building,* fedha za ndani za mwaka huu ni shilingi 1,500,000,000/=. Nakata kujua ni ofisi gani na eneo gani?

**MWENYEKITI:** Tuko kwenye voti 33, ni *Ethics Sekretariet.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili ni kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Kanda Mtwara. Mkandarasi yuko *site,* mwaka jana hazikutolewa fedha zozote na mwaka huu ndio imetengwa kiwango hiki.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi niko kwenye *subvote* ndogo 6208 ambayo kama naelewa Kiingereza vizuri, *Tackling Corruption Project* maana yake ni mradi wa kupambana na rushwa lakini najaribu kuangalia hapa sioni fedha yoyote sio ya ndani wala sio ya nje wakati tunajua kabisa kwamba *corruption* katika nchi yetu ni tatizo. Nilikuwa naomba maelezo*, unless* hiki kifungu maana yake ni nyingine?

**MWENYEKITI:** Hakina hata senti na pale juu ni *Ethics Secretariet*. Naomba maelezo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nilisema kwamba Sekretariet ya Maadili pamoja na TAKUKURU pamoja na Taasisi nyingine kwa pamoja wanafanya mikutano pamoja na wadau mbalimbali ili kupambana na rushwa. Kwa hiyo, fedha zao zitakuwa kule TAKUKURU ila huwa wanashirikiana kwa pamoja katika kupambana na rushwa. Kwa hiyo, kazi hii inafanyika kama kawaida.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit* ... ... ... ... .... Tshs. 825,490,000/=
Kif. 1004 - Government *Communication Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 240,100,000/=
Kif. 1008 - *Legal Service Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 0/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2001 - *Public Service Leaders Division* ... ... ... ... ... ... ... Tshs. 256,734,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali. Vifungu vilivyopita hamna, nilichosema hamna hela, hakuna basi. Mheshimiwa Susan wewe unauliza kifungu gani, kifungu kisichokuwa na hela? Nilikataa chenyewe hicho. Mheshimiwa Mkosamali ulisimama kifungu gani, kisichokuwa na hela?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI**: Hapana sio kisichokuwa na hela, ni hiki chenye fedha.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Nauliza kwa nini kifungu hiki hakijatengewa fedha za ndani na kumekuwa na malalamiko mengi sana.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani, sema vizuri kifungu gani? Kuna *subvote na sub-item.*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote 2001, subitem 6212,* kiko kimoja tu. Nauliza hivi, kwa nini hiki fungu hakijatengewa fedha za ndani kwa sababu tatizo la maadili kwa viongozi limekuwa kubwa. Sekretarieti hii inashindwa kuhakiki fomu zile tunazojaza. Mwaka jana imehakiki fomu 300 kati ya fomu 10,000 ambazo zimejazwa. Ndiyo maana mchangiaji wa jana Mheshimiwa Tundu Lissu alisema hakuna kiongozi aliyewahi kukutwa hana maadili maana hawapitii zile fomu. Sasa kwa nini hamtengi fedha za ndani ili hawa watu waweze kufanya kazi? Mnatenga tu fedha za *capacity building*, *awareness*, kuliko fedha za kuja kuhakiki mali za watu ambazo wamezipata kwa njia ya ubadhirifu na njia ambazo sio sahihi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopata fedha kutoka kwa wafadhili, huwa wanaainisha sehemu ambazo wao wanaona kwamba wajenge uwezo kwa viongozi wa umma ili waelewe ni nini kinafanyika katika Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa hiyo, fedha nyingine ambazo ni za ndani ni zile za matumizi ya kawaida, ameona tumetenga fedha nyingi tu kwenye kitabu kilichopita kwenye *recurrent*. Kwa hiyo, fedha nyingi ambazo zinatumika kwa ajili ya uhakiki, ziko kule kwenye *recurrent* huku ni kwa ajili ya *awareness*.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote*)

Kif. 2002 – *Political Leaders Division* … … … ... ... ... ... Tshs. 261,220,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitisha na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote*)

**Fungu 66 – Tume ya Mipango**

Kif. 1003 - *Planning and Monitoring Division* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Tshs.0/-
Kif. 2002 - *Productive Sector Cluster* ... ... ... ... ... ... ... Tshs.1,257,600,000/-

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote)*

Kif. 2003 – *Infrastructure and Service Cluster*... ... ... ... ... ... ... Tshs.29,964,300,000/-

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa Halima Mdee. Tunaanza na Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusu kasma 6294 na iwapo ufafanuzi hautaniridhisha, nitaomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili eneo limeandikwa *Big Results Now*, kwa maana ya jina unaweza kuona lina mvuto kwa maana ya matokeo makubwa sasa lakini fedha hizi ni kwa ajili ya kuanzisha chombo kinachoitwa *Presidential Delivery Bureau.* Kimetengewa shilingi bilioni 4.9/- pesa za ndani, shilingi bilioni 25 pesa za nje, kwa ujumla ni takribani bilioni 29 kwa ajili ya ki-Idara hiki au chombo hiki. Kazi zake kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri mwenye dhamana, inaonyesha zaidi ni vikao, kama inafanya *labs* kwa maana ya zile maabara pamoja na umuhimu wa sekta ambazo hiki chombo kinashughulikia na sekta zile kwa maana ya kipaumbele ni kipaumbele muhimu, sijui nishati, maji na kadhalika. Kwa maana ya mfumo ambapo hiki chombo kinakwenda kutumia kufanya kazi ni mfumo ambao hauwezi kuleta tija inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya kazi ambazo zinakwenda kufanywa na hiki chombo ni kazi ambazo sasa zinafanywa na Tume ya Mipango kwenye

muundo wake wa kiutekelezaji. Ni kwa nini tunaanzisha chombo kingine, tunapanua ukubwa wa Serikali wakati hatujamalizia kushughulikia kuboresha ufanisi wa Tume ya Mipango, tunaunda chombo kingine pembeni kwa gharama kubwa ya mabalioni ya shilingi ambayo imetajwa hapa. Ni kwa nini hizi fedha badala ya kutumika kwenye vikao sijui vinavyoitwa *lab* au kwa jina lingine zuri litakaloitwa zisitumike kwenye miradi ya maji, umeme na miradi ya barabara ili hayo matokeo yakatokea sasa badala ya matokeo yakawa kwenye vitabu na kwenye vikao ambavyo viongozi wanakaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi ili jambo hili liweze kurekebishwa, Serikali ipunguze matumizi hasa Ofisi ya Rais, kwa sababu hii iko Ofisi ya Rais, Mwenyekiti wa Tume ya Mipango ni Rais, chombo hiki ni cha ofisi ya Rais. Ofisi ya Rais ionyeshe mfano wa kupunguza matumizi, pesa zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo. Ninaomba ufafanuzi na iwapo sitaridhika nitaomba niondoe shilingi ili nipate ufafanuzi zaidi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninajibu hoja hapa nilikwishatoa maelezo kwamba kimeanzishwa chombo ambacho hakiingiliani kazi zake na Tume ya Mipango. Chombo hiki kitakuwa kinashughulikia kufuatilia utekelezaji wa miradi. Sasa Mheshimiwa Mnyika anasema tupunguze matumizi lakini kutofuatilia miradi vilevile ni kuongeza matumizi kwa sababu hatuna uhakika kama fedha za miradi hiyo zitakuwa zinatumika bila kuwa na ufuatiliaji. Kwa hiyo, kufuatilia ni sehemu ya kuzuia na kuendeleza zaidi utekelezaji.

## HOJA YA KUONDOA SHILINGI

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika unaondoa shilingi, haya.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na umuhimu wa ufuatiliaji yaani *monitoring and evaluation...*

**MWENYEKITI:** Sasa unaongea kwa mara ya pili ama unaondoa shilingi au tayari umeshajibiwa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Ndio nataka kutoa hoja ya kuondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Unaondoa shilingi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Naondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Haya, endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ninachosema ni kwamba sina tatizo na umuhimu wa ufuatiliaji ili miradi itekelezwe kwa ufanisi lakini ukiangalia muundo wa Serikali yetu, kwenye Hotuba ya Waziri mwenyewe alipokuwa anaelezea mafanikio ya kazi zilizofanywa na Tume ya Mipango, ameelezea kwamba Tume imefuatilia miradi, imechambua miradi, ufanisi wa utekelezaji wa miradi. Sasa wakati Tume ya Mipango inapanga na kufuatilia utekelezaji kinaundwa chombo kingine tena Ofisi ya Rais na Tume ya Mipango na yenyewe iko ndani ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Tume hiyo ni Rais yuleyule halafu kinaundwa chombo kingine cha utekelezaji wa ahadi ni *dublication* ya majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayoitoa hapa ni kwamba Serikali isimamishe kwanza zoezi hili la kuunda *Presidential Delivery Bureau*, itekeleze kwanza ahadi ilizotoa kwa Bunge kurekebisha ufanisi wa Tume ya Mipango na kuiongezea pesa za kutosha na kuitungia Sheria ili Tume ya Mipango itekeleze wajibu wake vizuri wa kupanga na kufuatilia badala ya kutumia fedha za Serikali shilingi bilioni 29 badala ya kuzipeleka kwenye maji, umeme, barabara zitumike eti kukaa vikao vya kuangalia unafuatiliaje maji, umeme na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hili siliungi mkono kabisa na kama Serikali ikilazimisha basi walau kidogo

iunganishe hii mifumo, iunganishe marekebisho ya muundo wa Tume ya Mipango na masuala ya ufuatiliaji wa ahadi ili yaende sambamba badala ya kuunda chombo kingine na kutumia gharama kubwa ambazo hazina tija kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Umeondoa shilingi, hoja ni nini? Unataka maji, unataka chombo, unataka ni nini? Hoja ni nini na lazima iwe moja *focused*.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba kasma hii iliyopo hapa ifutwe fedha zake zielekezwe nyingine kwenye miradi ya maendeleo na nyingine kwenye kuboresha ufanisi wa Tume ya Mipango.

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Humu ndani Wabunge wote kila siku tumekuwa tukilalamika suala la miradi kutokamilika kwa wakati na kila siku tunalalamika hata hizo Halmashauri zetu zimekuwa hazifuatilii vizuri ahadi za Rais. Sasa leo kinaundwa chombo cha kuhakikisha kinafuatilia miradi mbalimbali na hauwezi ukawa na chombo kama hauna fedha za kuanzia na tumeambiwa hiki ni chombo kipya, sasa tatizo liko wapi? Hebu tutoe fursa kwa Serikali ifanye kazi yake halafu mwaka ujao kama hakutakuwa na umuhimu wa hiki chombo kwamba hakijafanya kazi yake vizuri ndiyo tuanze kuhoji. Sisi wenyewe humu ndani tunalalamika, miradi haifuatiliwi mara hivi mara vile, tufanyeje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ngoja niangalie wasiozungumza, Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeenda moja kwa moja kwa kusema kwamba hizi fedha zingeenda kwenye miradi mingine kwa sababu suala la usimamizi wa miradi lipo katika ngazi ya Halmashauri na siku zote kwenye hotuba zetu tumekuwa tukiisisitiza Serikali iende kuwafundisha kama ni Madiwani iwaelekeze utendaji mzuri wa Serikali ili waweze kuisimamia. Sasa tunapotengeneza timu mpya, mambo yatakuwa ni yaleyale na tumekuwa tukiona katika miradi mingi. Tumekuwa na MKUKUTA I, umeshindwa kabla haujashindwa tukaleta MKUKUTA II ukashindwa. Sasa ndiyo umekuwa huu mfumo kwamba jambo moja linaposhindwa tunakwenda jambo la pili. Kwa hiyo, sisi tungesisitiza kwa sababu matatizo ya maji nchini, barabara na afya bado ni makubwa kuliko kutengeneza hiki chombo, basi hizi fedha ziende katika miradi ya maji kwa wananchi wetu wote. Naomba hizi fedha zihamishwe ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Itabidi mtoe semina sasa, Mheshimiwa Eng. Ramo!

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitoe ufafanuzi kidogo kuhusiana na suala la *projects implementation* au utekelezaji wa miradi. Usimamizi wa miradi sio vikao. Usimamizi wa miradi ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi katika hatua zote. Mradi ukiwa na hatua kumi za utekelezaji basi utafuatilia utekelezaji wake katika hatua zote kumi. *Presidential Delivery Unit,* ni hatua ya kuhakikisha kwamba fedha za Serikali zinazotengwa ambazo tumekuwa tukilalamika siku zote kwamba kutenga bajeti ni jambo moja lakini utekelezaji wa bajeti kwa maana ya *value for money* ni jambo jingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tumetafuta dawa ya kuhakikisha kwamba *value for money* inatekelezwa basi hiyo itakuwa ni hatua nzuri sana ya kuipongeza Serikali. Kwa hiyo kwa sasa hivi naomba tuipe nafasi *Presidential Delivery Unit* iweze kuonekana ita-*deliver*

namna gani halafu tunaweza kuja kuboresha baadaye kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani ni vile tu kwa kuwa hakuna *consistence* katika maoni ya wenzetu. Mara wanasema hatutekelezi na kutoa matokeo ya miradi tunayopanga, tukifanya mbinu za kuweza kutekeleza yale mambo tuliyopanga, wanasema mnatenga fedha ya nini? Mimi siamini kama wanaweza wakatushauri tufanye jambo jema maana wao wanapenda tukosee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningeshauri tu hapa kwa sababu jambo liko wazi kabisa, fedha hizi ambazo mtoa hoja Mheshimiwa Mnyika anazisema ni shilingi bilioni 29 lakini angalia zinaenda kusimamia miradi yenye thamani gani. Miradi ya vipaumbele tuliyopanga inakwenda kwenye *trillions,* sasa *trillions* sita ukisimamia kwa shilingi bilioni 29, uwiano ule wa usimamizi na uzito wa miradi hiyo; tunazungumzia bomba la gesi tunataka matokeo sasa ili tuweze kufika kwenye malengo yetu ya Ilani yetu. Kwa hiyo, mimi siamini Mheshimiwa Mnyika anaweza kutuunga mkono tunapoweka chombo cha kusimamia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Wale wasioongea sana, Mheshimiwa Kiwanga?

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tatizo kubwa la nchi yetu ukiangalia kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kwa miaka miwili mfululizo, ni kutokuwa na hela au zinachelewa kupelekwa na nyingine hazipelekwi kabisa. Kwa hiyo, tatizo sio chombo cha ufuatiliaji kutoka Ofisi ya Rais. Kwa hiyo, ukiuliza kwenye Halmashauri zote tatizo kubwa ni ucheleweshwaji au kutopelekwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naunga mkono kauli ya Mheshimiwa Mnyika kwamba hizo hela

zipelekwe huko ili zikamalize miradi ya maendeleo katika maeneo yetu. Kwa mfano, kuna maeneo mbalimbali miradi haijakamilika kabisa na inaharibika na inatakiwa ianze upya. Kwa hiyo, mimi naona wafuatiliaji wapo ambao ni watendaji katika Halmashauri na katika Mikoa wapo na sasa ni wakati wa kutoa hizo fedha kupeleka kwenye miradi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** *Big Results Now,* Mheshimiwa Kandenge, kuna watu ambao sijawasikia, lakini sitaruhusu mjadala maana naona mnajizungusha tu hapa. Haya Mheshimiwa Kandege, sijakusikia.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kila muda tunaambiwa kwamba tulianza pamoja na nchi kama Malaysia lakini sisi hatuendelei sasa Serikali inakuja na tiba kwamba tunataka matokeo ya haraka sasa. Sasa mtu anakuja anasema kwamba hili hatulitaki maana yake nini, ni ili ionekane Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kufanya kazi. Tusikubaliane na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoongelea sio miradi ya kwenye Halmashauri ni ile miradi ya kitaifa. Sasa tuelewane kwamba kuna miradi ya kitaifa ambayo lazima chombo hiki kisimamie na tupate matokeo makubwa sasa. Kwa hiyo, naunga mkono Serikali na nia yake njema sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ataongea Mheshimiwa Halima na ndio atakuwa wa mwisho.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, napata faraja ya kuona kwamba Serikali inakiri yaani hiyo ni *failure of leadership*. Tunasema hivyo kwa sababu, kwanza, tuna mfumo wa Serikali mpaka kule chini wenye wataalam. Mfumo wa kutosha, ukizungumzia ahadi za Rais, kuna Mkuu wa Mkoa na Ofisi yake na wataalam wake. Tuliwaambia basi tufute Ma-*DC* na Wakuu wa Mkoa kwa sababu hawana kazi, ndiyo hivi vitu mnavyovisema hapa. Tuna Tume ya Mipango

amesema Mheshimiwa Mnyika. Tume ya Mipango ina wataalam na wana majukumu yao. Unavyosema ujenzi wa mabomba ya gesi, kuna utaalam wa kupata makandarasi lakini vilevile Wizara ina wataalam wake ambao wanashuka hadi katika ngazi ya Halmashauri. Leo tunatenga fedha hizi, mimi nilitarajia Wabunge wangesema wanaungana na Mheshimiwa Mnyika hizi fedha zipelekwe hata umeme vijijini, zitolewe hapa kwa sababu mfumo wa utendaji kazi na usimamizi kuna vyombo. Tuna matatizo ya kubadilisha majina, siasa ni kilimo, kilimo kwanza, sijui nini mambo yaleyale. Tunachotakiwa tupeleke fedha kwenye miradi husika. Tatizo sio vyombo vya usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba, msi-*copy* na ku-*paste* kila kitu wanachofanya Malysia na nyie mfanye. Wao wana mfumo wao na sisi tuna mfumo wetu, tuchukue vizuri vingine tuviache twende na mfumo wetu. Hizi shilingi bilioni 29, nyie ni wengi mnaweza mkaamua lakini hili ni chaka la ulaji tu hakuna *issue* hapa...

**MWENYEKITI:** Maneno yasiyokuwa na msingi ya nini, umeshamaliza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa hiyo, naungana na Mheshimiwa Mnyika. *(Makofi)*

**MWENYEKIT:** Serikali, maana ni kuzungushana maneno na hotuba mmeshasahau ilisemaje, aah. Majibu Serikali. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani tumesaidiwa sana na wale wote ambao wameongea kuunga mkono hoja hii. Tunachosema hapa sio kwamba tunaenda kusimamia miradi katika *local government,* kuna miradi ambayo imewekwa katika Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya *level* ya Taifa na imechaguliwa miradi katika maeneo sita. Hata hayo maji anayozungumza yamo katika mpango ule lakini lazima yafuatiliwe. Katika mpango wa maji kwa mfano, tumekubaliana kwamba *priority* itakuwa

kufufua miradi yote ya maji ambayo sasa ipo lakini haifanyi kazi na kwa kufanya hivyo tutaweza kuwapa huduma watu wapatao milioni 15 kwa kurudisha mfumo wa maji ambao ulikuwa haufanyi kazi lakini kazi hiyo inahitaji kufuatiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza juu ya nishati, tunajenga bomba la gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam, tunataka mpango ule usichelewe. Kwa hiyo, tunaweka chombo cha kuhakikisha kwamba kazi ile inafanyika na hakuna kusema fedha imekosekana. Tunazungumza habari ya kujenga reli na kuimarisha reli kwa ajili ya kufungua *central corridor,* tunahitaji chombo hiki kufuatilia kuhakikisha kwamba kazi hiyo inafanyika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea)*

**MWENYEKITI:** Acheni kuongea maneno ambayo hayana maana, sikilizeni anachoongea Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Huwezi ukasema kwamba ni *failure of leadership*, hii ni *innovation* na *innovation* huwezi kuikataa. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa hivi namwita mtoa hoja ambaye ni Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *innovation* ya kutoka Malaysia na nimepata bahati ya kufahamu kwamba ilikuwaje hili wazo likakubaliwa na Serikali. Mheshimiwa Rais alialikwa kwenye *retreat* kule Malaysia na Serikali ya Malaysia ikatoa maada kuhusiana na namna gani inavyojiendesha. Sasa mimi hoja yangu hapa ni nini? Hii ni mara ya pili tuna *copy* mawazo kutoka Asian Tigers.

**MWENYEKITI:** Hoja yako ni kwamba hiki kifungu kiondoke.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa hoja Serikali imefafanua sasa nataka nijibu.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza. Hoja tuliyonayo hapa ni ile uliyoweka wewe kwamba kifungu hiki kisitumike hapa kiende kufanya kazi nyingine, hiyo ndiyo hoja. Sasa kama unajibu ya hawa jibu, kujibu ni tofauti lakini hoja ndiyo hiyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni hiyo na nashukuru sana kwa maelekezo yako. Kwa hiyo, nataka kueleza ni kwa vipi majibu yaliyotolewa hayajakidhi haja ya hii hoja kwa hiyo ni muhimu sana hii hoja bado ikapitishwa, ndicho ninachotaka kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema tu kwamba kwenye nadharia ya *project cycle* kwa maana ya mzunguko wa mradi na nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Eng. Makani kwamba mzunguko wa mradi una hatua nyingi, kwenye hatua hizohizo anazozungumza Mheshimiwa Eng. Makani, kuna hatua ya ufuatiliaji kwa kila mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiuchukua mradi kwa mfano wa kitaifa wa maji Dar es Salaam, ukichukua pesa za *MCC*, ukichukua pesa za India kila pesa ina *component* ya ufuatiliaji wa mradi ambapo ni mabilioni. Ukichukua mradi wa bomba la gesi kwenye mkataba wa mradi kuna kipengele cha ufuatiliaji wa mradi, ukichukua miradi ya reli kuna kipengele cha ufuatiliaji wa mradi. Sasa kama tuna vipengele vya ufuatiliaji wa miradi kwenye *individual projects*; ni kwa nini tutumie shilingi bilioni 29 kufuatilia miradi kwenye Ofisi ya Rais, ndiyo hoja inalala hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kwenye mfumo wa Serikali wa sasa, Wizara ya Fedha ina mfumo wa kufuatilia miradi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina mfumo wa kufuatilia miradi, Ofisi ya Rais yenyewe kupitia Tume ya Mipango ina mfumo wa kufuatilia miradi. Kwa nini tutumie shiilingi bilioni 29 kutengeneza mfumo mwingine wa kufuatilia miradi? Ndiyo hoja ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili hayo unayoyasema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu yatekelezwe haraka; kama *labs* zimeshabaini kwamba miradi mingi imekwama na ndiyo ilikuwa msingi wa hoja yangu binafsi ya maji, kwamba miradi mingi imelala, chukua pesa kafufue miradi. Sasa unachukua pesa unaelekeza tena kwenda kukaa vikao sijui kufuatilia, sijui kufanyaje, hatuwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha tu kwa kusema kwamba mkiipitisha hii kwa kiwango hiki bila kwenda kupunguza, ndiyo mnathibitisha udhaifu na vilevile ishara ya *failure of government*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya Kuondoa Shilingi ya Mhe. John J. Mnyika ilikataliwa na Bunge)*

*Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote*)

**MWENYEKITI:** Hoja imetoka, tuendelee.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaongea)*

**MWENYEKITI:** Nyie midomo, midomo ya nini, mmeshapiga kura bado mnaendelea, *why!* Tuendelee.

Kif. 2004 - *Social Service and Demographics* … … ... ... ... Tshs.615,029,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko Yoyote*)

*(Bunge lilirudia)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kila chombo kina *traditions* zake. Anapokuja huyu kuweka Siwa pale kila mtu anasimama na kunyamza. Si wakati wa kila mtu kuongea maneno yake. Jamani kila chombo kina *culture* yake, anapoweka Siwa wote mnanyamaza ndiyo maana mimi nasimama pale, mpaka aweke ndiyo nije hapa, naomba tuzingatie haya. Mheshimiwa Mtoa hoja, taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati imepitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Fungu 20 na 30 - Ikulu, Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 66 - Tume ya Mipango, Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 94 – Tume ya Utumishi na Fungu 09 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

*(Hoja iliyotolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwapongeze Wizara, Ofisi ya Rais, watendaji wake wote katika sehemu mbalimbali kwa kazi nzuri, tunachoomba muendelee na hii iwe ofisi ya mfano na fedha za Serikali zilizotolewa zitumike vile inavyopaswa.

Ninaomba nitoe taarifa kwamba nilisema mwongozo alioomba Mheshimiwa Mbowe nitautoa leo; lakini naomba nitoe kesho asubuhi kwa sababu ushauri nilioupata sijaufanyia kazi, niko *busy* na ninyi kwa hiyo nitautolea maelezo kesho asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.05 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 19 Aprili, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*